**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | **Mhe. Zubeir Ali Maulid** | - | **SPIKA** |
| 2. | **Mhe. Mgeni Hassan Juma** | - | **Naibu Spika/Nafasi za Wanawake** |
| 3. | **Mhe. Mwanaasha Khamis Juma** | - | **Jimbo la Dimani** |
| 4. | **Mhe. Shaaban Ali Othman** | - | **Jimbo la Mpendae** |
| 5. | **Mhe. Hemed Suleiman Abdulla** | - | **MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais** |
| 6. | **Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman** | - | **MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu.** |
| 7. | **Mhe. Masoud Ali Mohammed** | - | **MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole.** |
| 8. | **Mhe. Haroun Ali Suleiman** | - | **MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala** |

**Bora/Jimbo la Makunduchi.**

**9. Mhe. Jamal Kassim Ali - MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni.**

**10. Mhe. Dkt Khalid Salum Mohamed - MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge.**

**11. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan - MBM/Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje**

**12. Mhe. Simai Mohammed Said - MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu**

**13. Mhe. Tabia Maulid Mwita - MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais**

**14. Mhe. Riziki Pembe Juma - MBM/Waziri wa Ardhi na**

**Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake**

**15. Mhe. Rahma Kassim Ali - MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake**

**16. Mhe. Suleiman Masoud Makame - MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga**

**17. Mhe. Abdulla Hussein Kombo - MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani**

**18. Mhe. Lela Muhamed Mussa - MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake**

**19. Mhe. Abdalla Abasi Wadi - Jimbo la Nungwi**

**20. Mhe. Ali Abdulgulam Hussein - Jimbo la Jang'ombe**

**21. Mhe. Ali Suleiman Ameir - Jimbo la Pangawe**

**22. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Jimbo la Mwanakwerekwe**

**23. Mhe. Anna Athanas Paul - Uteuzi wa Rais**

**24. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Mahonda**

25. Mhe. Azza Januar Joseph - Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
27. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Jimbo la Wawi
28. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafas iza Wanawake
29. Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) Nafasi za Wanawake
30. Mhe. Habibu Ali Muhamed - Jimbo la Mtambwe
31. Mhe. Haji Omar Kheri - Jimbo la Tumbatu
32. Mhe. Haji Shaaban Waziri - Jimbo la Uzini
33. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura
34. Mhe. Harusi Said Suleiman - Jimbo la Wete
35. Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani
36. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
37. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir - Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Jimbo la Mtoni
39. Mhe. Juma Makungu Juma - Jimbo la Kijini
40. Mhe. Juma Ali Khatib - Uteuzi wa Rais
41. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu - Jimbo la Chwaka
42. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe - Jimbo la Wingwi
43. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
44. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
45. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Jimbo la Mwera
46. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

47. **Mhe. Mohamed Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile**
48. **Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Jimbo la Malindi**
49. **Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini**
50. **Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani**
51. **Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake**
52. **Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Nafasi za Wanawake**
53. **Mhe. Mwanajuma Kassim Makame - Nafasi za Wanawake**
54. **Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji - Mwanasheria Mkuu**
55. **Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Jimbo la Chaani**
56. **Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni**
57. **Mhe. Nassor Ahmed Mazrui - Uteuzi wa Rais**
58. **Mhe. Omar Said Shaaban - Uteuzi wa Rais**
59. **Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake**
60. **Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Jimbo la Amani**
61. **Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake**
62. **Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum - Uteuzi wa Rais**
63. **Mhe. Saidi Saleh Salim - Jimbo la Tumbe**
64. **5Mhe. Sabiha Filfil Thani - Nafasi za Wanawake**
65. **Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake**
66. **Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake**
67. **Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani**

**68. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman - Jimbo la Kiembe Samaki**

**69. Mhe. Sulubu Kidongo Amour - Jimbo la Mkwajuni**

**70. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake**

**71. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Jimbo la Micheweni**

**72. Mhe. Shaib Hassan Kaduara - Jimbo la Chake Chake**

**73. Mhe. Yahya Rashid Abdulla - Jimbo la Kwahani**

**74. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni**

**75. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake**

**76. Mhe. Zawadi Amour Nassor - Jimbo la Konde**

**Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu**

**Kikao cha Tano – Tarehe 16 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 12 Februari, 2021 Mhe. Issa Haji Ussi na Mhe. Miraji Khamis Mussa waliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 49 na Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini aliahidi kujibu swali hilo kwa maandishi.

Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini asome jibu la swali lililoulizwa na Wajumbe hao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, Naomba kuwasilisha kwa maandishi jibu la swali la nyongeza la Mhe. Issa Haji Ussi Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka na Mhe. Miraji Khamis Mussa kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa uhuishaji na uimarishaji wa mfumo wa maji Zanzibar unagharamiwa kwa mkopo wa USD 92.18 milioni kutoka *Exim Bank* ya India. Mradi umegawika katika Lot 3 kwa mchanganuo ufuatao:-

1. LOT 1 M/S MEGHA – USD 26,167,200.33
2. LOT 2 M/s AFCON – Vijeta JV USD 27,740,731.71
3. LOT 3 M/S L&T – USD 35,829,919.60

Lot 3 za mradi huu zimegawika kwenye scheme tatu ambazo ni:

Lot 1 inafanya kazi scheme ya Mfenesini na Dole
Lot 2 inafanyaka kazi scheme ya Mkorogo, Dimani na Maungani
Lot 3 inafanyakazi scheme ya Kidatu na Masingini pamoja na kazi ya Ujenzi wa Jengo la Afisi Kuu ya Mamlaka ya Maji ZAWA eneo la Mwembe Madema.

Maeneo ya Mradi ni:

- Wilaya ya Magharibi A
- Wilaya ya Magharibi B
- Wilaya ya Kati
- Miji midogo ya Fumba na Tunguu.

(b) Kwa upande gharama ambazo serikali itachangia na Serikali ya Mapinduzi Zaznzibar, zitajumuisha ulipaji wa fidia kwa maeneo yatakayoathirika na

mradi lakini kwa sasa hakuna hesabu ya moja kwa moja kiwango ambacho kitalipwa na Serikali.

**TAARIFA**

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita muulizaji wa swali naomba nitoe taarifa tu kwamba kuna baadhi ya Wajumbe *mic* zao hazifanyi kazi. Kwa hiyo, kwa wale ambao watajigundua kwamba *mic* zao hazifanyi kazi wanaweza wakasogea mbele kidogo kwa ajili ya kuweza kuzungumza, ni maeneo ya huko nyuma zaidi huku mbele nafikiri hakuna shida sana. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed ili aulize swali lake.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 86**

**Athari za Uchimbaji Mchanga Kiholela**

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed -** Aliuliza**:-**

Katika maeneo ya Mwanakwerekwe kuna shimo limezidishwa kuchimbwa mchanga na kusababisha wakaazi wa karibu kuwa na wasi wasi mkubwa kutokana na ardhi yake ya mmong'onyoko.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa shimo hilo ambalo linaweza kuleta madhara zaidi hasa katika kipindi cha mvua za masika.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi katika kudhibiti tabia hizi za uchimbaji ovyo wa mchanga ambao unasababisha madhara makubwa hasa katika kipindi cha masika.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi na Utawala Bora) -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 86 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa serikali wa shimo la Mwanakwerekwe ni kuliendeleza shimo hilo ili lipokee vizuri maji ya mvua yasiweze kusababisha mafuriko na yasaidie kuongeza upatikanaji wa maji ya chini ya ardhi ambayo yamekuwa ndio mhimili mkubwa wa maji safi na salama hapa Zanzibar. Katika kufanikishwa lengo hilo, Serikali imefanya mambo yafuatayo kupitia Mradi wa Huduma za Miji ya Zanzibar (*Zanzibar Urban Service Project – ZUSP*) imefanya mambo yafuatayo:-

1. Kubomoa na kujenga upya barabara ya Mwanakwerekwe eneo la shimoni kwa kuinua barabara hiyo ili iweze kupitika wakati wote ikiwa ni pamoja na wakati wa mvua.

2. Kuchimba na kuongeza kina cha shimo la Mwanakwerekwe kwa kutoa tope zilizokuwepo eneo hilo ambazo zilipungua kina cha shimo hilo na uwezo wa kupitisha maji kwenda chini ya ardhi. Hivyo, uchimbaji wa mchanga katika shimo hilo ulifanywa kwa ajili ya kuliwezesha shimo hilo kupokea kiwango kikubwa cha maji ya mvua ili yasiweze kuleta athari kwa wananchi wa eneo hilo na mali zao.

(b) Katika kudhibiti tabia za uchimbaji ovyo wa mchanga, Serikali imefanya mambo yafuatayo:-

1. Kuelimisha jamii juu ya athari za uchimbaji ovyo wa mchanga na maliasili nyengine zisizorejesheka.

2. Kuunda Kamati ya Wataalamu chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya kubainisha maeneo maalum yanayofaa kuchimbwa mchanga ili kuongeza wigo wa uchimbaji rasmi wa mchanga kwa kufuata vigezo vinavyokubalika.

3. Kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji wa vibali vya mchanga ambapo muombaji anapaswa kulipa gharama za kibali hicho kupitia Benki.

4. Kuhamisha shughuli zote za uchimbaji wa mchanga kutoka Idara ya Misitu na kwenda Idara ya Nishati na Madini ili kuongeza ufanisi wa usimamizi wa shughuli hizo.

5. Kufanya doria za mara kwa mara za kuwabaini wale ambao wanachimba mchanga kiholela na kuchukuliwa hatua husika za Kisheria. Doria hizo hufanywa kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mashirikiano na vyombo vya ulinzi na usalama.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hizo za serikali zinazochukuliwa kwa ajili ya kudhiibiti uchimbaji holela wa mchanga, naomba nitoe wito kwa wananchi wanaochimba mchanga ovyo kuacha tabia hiyo mara moja, kwani watakaokamatwa kujihusisha na tabia hiyo, hatua kali za Kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mnamo mwaka 2018 serikali iliunda Tume ya kuchunguza sehemu ambazo huathirika na mvua za masika. Kwa mfano, maeneo ya Mwanakwerekwe ambapo kuna nyumba kadhaa zilikaribia kuzama.

Je, tume iliyoundwa imefikia wapi na inatwambia nini maana ni muda mrefu sasa tunaona kimya na pia tume imegundua nini.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi na Utawala Bora):** Mhe. Spika, kazi ya tume ilimalizika kwa wakati fulani lakini hata hivyo utafiti wa pale bado unaendelea.

Lakini la msingi zaidi ni kwamba baada ya kutokea matokeo yale na ile tume ilipoundwa serikali ikaona kuna haja ya kupatengeneza pale mahali kwa sababu athari za nyumba zinaendelea na pale hapawezi kupitika. Kwa hivyo, serikali ikachukukuwa hatua ya kwanza kupatengeneza ili kwanza papitike halafu taarifa zitatolewa.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa kuwa serikali inachimba mchanga katika maeneo mengi na mara zote ukichimba mchanga kimazingira maana yake inatakiwa ile ardhi irejeshwe na iko tozo maalum katika tozo ambazo ile serikali inachukuwa lakini iko maalum ya urejeshaji wa ile ardhi yenyewe.

(a) Mhe. Waziri kwa mwakwa wa fedha 1919/1920 maana tunataka kupima ule uhalisia. Serikali katika eneo lile katika maeneo yaliyochimbwa mchanga Kaskazini Unguja ilibahatika kukusanya kiasi gani.

(b) Kwa mwaka huo huo marejesho yake ya ile ardhi kimazingira nakusudia yale maeneo yaliyochimbwa mchanga na tozo yake imeshachukuliwa hatua ya serikali katika kurejesha imefikia wapi na kama bado hamjaaza lini serikali itaanza hatua hiyo.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi na Utawala Bora):** Mhe. Spika, Mhe. Miraji Khami Mussa swali lake nimelifahamu ingawa alikuwa anapiga dana dana kidogo huku na huku lakini nimelifahamu.

Kimsingi ni kwamba linahitajia kuwa na takwimu lakini *in shaa Allah* tukijaaliwa jibu lake la mapato na kila kitu nitamletea kwa maandishi tukijaaliwa.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Spika, kwa kuwa mashimo hayo au mapango huwa yanatokea na maeneo mengine hasa maeneo ya Mutondooni na kupokea maji mengi yanayotoka ziwa Maboga. Je, serikali ina mpango gani wa kulifanyia utafiti shimo au pango hilo na kujua maji yanaendea wapi ili yasilete athari kwa wananchi wa maeneo hayo.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi na Utawala Bora):** Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mwakilishi kwamba serikali inafanya jitihada kubwa ya kuwaondoshea kero wananchi katika maeneo mbali mbali. Mashimo haya yanayojaa maji yanaleta athari kubwa wananchi hawawezi kufanya shughuli zao kimaendeleo yanaharibu majimba na wakati mwengine hata kupita hapapitiki.

Kwa hivyo, serikali imeanza na Mwanakwerekwe jambo lolote linahitajia shubira na twende kwa hatua. Kwa hiyo, tumeanza na Mwanakwerekwe na serikali itaendelea na sehemu nyengine zile ambazo zinaleta athari kama hizo, kama pale penye daraja la Dr. Ali Mohd Shein tunajua kwamba pale tulikuwa hatuwezi kupita pale. Wakati ule serikali ikafanya jitihada likajengwa daraja la kisasa kabisa.

Kwa hivyo, hizo ni baadhi ya juhudi na maeneo mengine vile vile tutaendelea kufanya juhudi hizo. Kwa hivyo, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma serikali iko makini na tutafanya kila jitihada kushirikiana na nyie viongozi katika majimbo yenu ili kuhakikisha kuwa maeneo hayo yapo katika hali nzuri.

**Mhe. Zaina Abdalla Salum:** Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ya ufasaha kuwa tumeweza kufahamu changamoto hizi ni nini kinachokuwa kinasababisha.

Mhe. Waziri katika majibu yako uliyojibu kuhusiana na mambo ya mashimo. Changamoto hii Mhe. Waziri imekuwa kadhia hii inapata maeneo mengi ambayo hususan katika kijiji cha Bungi katika minara ya *ZBC*.

(a) Je, Mhe. Waziri na mashimo haya yameshazungumziwa kwa muda mrefu sana. Serikali inasababu gani za msingi ambazo zinapelekea kushindwa kurejesha uhalisia wa maeneo haya. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi na Utawala Bora):** Mhe. Spika, unajua mashimo yapo mengi na maeneo ni mengi na athari za mazingira haya zinaonekana na maeneo mengi yaliharibiwa na watu wakachimba, kazi iliyoko mbele yetu sasa ni kuyarejesha uhalisia wake kwa kupanda miti ambayo inaweza ikakidhi maeneo ya mahitaji yale na ikaweza kuota vizuri.

Nimepata taarifa kwamba maeneo kama yale ambayo yanachimbwa mchanga unaweza kupanda mishokishoki na miti ya aina mengine kama hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa mashimo yote yaliyokuwa katika hali kama hiyo.

Tunatoa wito kwa viongozi wa Wilaya, Mikoa na Waheshimiwa wa Baraza la Wawakilishi kusaidiana na wananchi katika kuyarejesha katika uhalisia wake.

**Nam. 84**

**Ukosefu wa Kituo cha Afya Chuo cha Kiislamu Micheweni**

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis -** Aliuliza**:-**

Chuo cha Kiislamu Micheweni kinakabiliwa na changamoto nyingi katika kuwapatia vijana elimu na mengine yanayohatarisha maisha ya wanafunzi wakati wanapopata

matatizo hasa nyakati za masomo pamoja na usiku kulazimika kutembea masafa kufuata huduma za kiafya Hospitali ya Micheweni.

Je, ni lini kutaanzishwa kituo kidogo cha afya katika chuo hicho ili kuwaondoshea usumbufu wanafunzi hao.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Halmshauri ya Wilaya ya Micheweni haina mpango wa kujenga kituo cha afya katika eneo la Chuo cha Kiislamu Kiuyu - Mbuyuni kwa mujibu wa sera ya afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2011 inayotoa muongozo kwenye masuala ya ujenzi wa vituo vya afya. Sera inaelekeza kutoka kituo kimoja hadi chengine sharti ni masafa baina ya vituo hivyo viwili yafikie kilomita tano. Kwa mnasaba huo kutoka Chuo cha Kiislamu Kiuyu - Mbuyuni hadi kituo cha afya Kiuyu - Mbuyuni masafa baina yao ni kilomita moja na nusu pekee. Hivyo wanafunzi wanaosoma hapo pamoja na wananchi kwa ujumla wanaombwa waendelee kukitumia kituo hicho kilicho karibu nao kupata huduma za afya.

Mhe. Spika, utakumbuka kuwa moja ya ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi wakati wa Kampeni ni kujenga vituo zaidi vya afya ili kuwapunguzia wananchi masafa ya kufuata huduma za afya katika vituo vya mbali. Hivyo, katika utekelezaji wa ahadi hii suala la ujenzi wa Kituo kidogo cha afya katika eneo la Chuo cha Kiislamu Kiuyu litazingatiwa ili kuondosha usumbufu kwa wanafunzi na wananchi kwa ujumla. Aidha, kwa kutambua changamoto iliyopo ya upatikanaji wa huduma za afya chuoni hapo, hatua za muda mfupi tutakazozichukua ni kuhakikisha kuwa angalau siku mbili kwa wiki huduma ya afya inatolewa wakati mpango wa muda mrefu wa kujenga kituo ukiendelea.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri pia naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mhe. Spika, Waziri kama unavyojua Chuo cha Kiislamu kimeasisiwa mwaka 2001.

Lakini pia tukitizama Chuo cha Kiislamu kina Kituo cha Afya kilichopo Kiuyu Mbuyuni kama unavyojua pale kuna wanafunzi wanawake pana na wanafunzi ambao wanasoma ualimu, karibuni tu Mhe. Waziri palitokea tatizo la wanafunzi ambao wanasoma Chuo cha Ualimu pale mzazi akazaa kwenye gari. Je, taarifa hii unayo.

(b) Mhe. Waziri umesema kuwa ahadi ya Mhe. Rais ni kweli lakini kama
tunavyojua maeneo ambayo wanaishi wanafunzi huwa panatokea tatizo la
wanafunzi ili kuumwa usiku na chuo kile hata hakina gari. Je, una mpango gani wa
kupeleka wataalam wa afya kwenye kituo kile.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

(a) Mhe. Spika, taarifa hii ya mwananchi ambaye alijifungua tunayo.

(b) Mhe. Spika, mpango wa kupeleka wataalamu kama nilivyoahidi katika jibu langu la msingi kwamba tutapelekea wataalamu kama nilivyoahidi kwenye
jibu langu la msingi kwamba tutapeleka wataalamu wa afya *at list* mara mbili kwa wiki na kama itaonekana haitoshelezi tutafanya jitihada za kuweza kupeleka kama mara tatu au zaidi ya hiyo kadiri ya hali italavyokuwa.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Mhe. Spika, lengo la Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema kwamba kila penye kilomita tano pawepo na huduma za mwanzo za afya, lakini kuwepo kwa kituo cha afya ni hatua ya kwanza na kutoa huduma ni hatua ya pili na wanaohudumiwa ni hatua ya tatu. Vituo vingi vya afya hapa Zanzibar mara nyingi hukosa dawa hata *panadol* na ushahidi juzi tumesikia *ZBC* kuna kituo cha afya kimekosa hata *panadol*. Ni sababu gani inayopelekea vituo vya afya na Zanzibar na bohari letu la dawa kukosa huduma hizi za mwanzo za afya zikiwemo hizi *panadol*.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwanza nikubaliane na yeye tunazo changamoto katika vituo vyetu vya afya. Vituo vya Afya ambavyo tuko navyo Zanzibar ni 158 ambapo Unguja tunavyo 93 na Pemba 65. Vipo vituo vya afya ambavyo vinaonekana kwamba upatikanaji wa huduma hizi uchache wa madaktari na upatikanaji wa dawa ni mdogo. Swali lake ni kwa nini hali iko hivi.

Mhe. Spika, jibu la swali hili ni mipango ya bajeti na tumhakikishie kwamba kwa sababu suala hili tunalifahamu tutachukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba bajeti tunayokwenda nayo inakwenda kutoa ufumbuzi wa tatizo hilo.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja lenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwenye jibu mama Mhe. Waziri ametwambia kwamba sera inaelekeza kutoka kituo kimoja hadi chengine sharti ni masafa na tukiangalia kisiwa cha Uvinje na Fundo masafa ni makubwa na tukiangalia vyote ni visiwa je, Mhe Waziri ni lini utakuja kutembelea kisiwa cha Uvinje ili kujua changamoto ambayo wanapata wananchi wale.

b) Kwa kuwa tumeona visiwa hivi Kojani wamejengewa kituo cha afya, Tumbatu na Fundo ni lini unatuhakikishiaje na wananchi wa Uvunje kujengewa kituo kidogo cha afya ili wasipate shida ya kuja Wete kwa kufuata matibabu na huduma nyengine.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Ahadi ya lini nitakwenda kutembelea Visiwa vya Uvinje na Ufundo nimuahidi kwamba muda wowote nitakaopanga na yeye kama Mwakilishi wa eneo hilo tutakwenda pamoja.
b) Swali la pili ambalo aliuliza je, tuna mpango gani kujenga vituo vya afya katika visiwa hivi, tumuhakikishie tu kwamba Visiwa vya Uvinje, Fundo kama livivyo visiwa vyengine Kojani na Tumbatu ambao kwa ukaribu huduma nyingi za kijamii zimeshasogezwa ikiwemo maji, umeme tumuhakikishie na visiwa hivi kwa sababu huduma za umeme zimeshafika, huduma za maji tayari na pia huduma za afya tutazipeleka vikiwemo vituo vya afya.

**Nam. 72**

**Ajira Kupitia Uwekezaji wa Ndani na Nje ya Nchi**

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum - **Aliuliza:-

Moja kati ya maeneo ambayo yanatarajiwa kutoa ajira nyingi ni sekta ya uwekezaji kupitia wawekezaji binafsi wa ndani na nje ya nchi.

(a) Je, ni utaratibu gani ambao Serikali unaufuata kuhakikisha kuwa ajira za wenyeji zinapatikana.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kunapatikana ufanisi mzuri kupitia uwekezaji wa ndani na nje.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Serikali ya Awamu ya Nane kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi moja ya mikakati yake ni kuzalisha ajira zipatazo 300,000 ifikapo mwaka 2025. Ajira hizi zitazalishwa kupitia vyanzo mbali mbali ikiwemo uwekezaji wa ndani na nje. Ajira hizi ni kwa ajili ya wazawa na taratibu tunazozifuata ni pamoja na kuhakikisha tunatekeleza kwa

vitendo lengo la kuanzishwa uwekezaji wa mitaji binafsi hapa nchini ambapo pamoja na mambo mengine ni kutengeneza ajira kwa wananchi kama ilivyoelekezwa katika Sera ya uwekezaji ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, Mwekezaji tokea anapoanzisha uwekezaji huwa anaongozwa na Sheria inayo muelekeza kuwa kipaumbele cha ajira ni kwa wazawa. Na hii inathibitishwa na kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji namba 14 ya mwaka 2018.

Miongoni mwa taratibu zinaotumika ni wawekezaji kuwekewa kiwango maalumu cha kuajiri wafanyakazi wa kigeni hasa katika nafasi maalumu za kitaaluma (*key positions*) kwa kutegemea ukubwa wa mradi na makubaliano baina ya *ZIPA* na Kamisheni ya Kazi. Taasisi zinazohusika na maombi ya vibali (*ZIPA*, Kamisheni ya Kazi na Uhamiaji) zinao utaratibu maalum wa kuyapitia kwa pamoja maombi yote ya uajiri wa wageni kabla ya kuyakubali au kuyakataa kupitia kituo kimoja cha huduma kwa wawekezaji (*One Stop Cente*). Hata baada ya kutoa vibali, Serikali kupitia Kamisheni ya Kazi hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha kwamba Sheria na taratibu zinafuatwa.

Mhe, Spika, Sheria ya Ajira namba 11 ya mwaka 2005 chini ya kifungu cha 36 inampa muongozo Kamishna wa Kazi juu ya mazingira ya kutoa vibali kwa wafanyakazi wa kigeni. Mazingira hayo ni:-

i) Endapo hakuna mfanyakazi ambae ni raia wa nchi yetu mwenye sifa zinazotakiwa kwa nafasi hiyo,

ii) Endapo nafasi hiyo ni ya uongozi ambayo muajiri anaruhusika kuajiri mtu anayemtaka chini ya Sheria ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi ya Zanzibar.

Mhe.Spika, Muwekezaji anapotaka kuajiri mgeni katika nafasi ambayo Serikali inahisi kuwa zinaweza kufanywa na wazawa, mwekezaji huyo huzuiliwa kupewa kibali na kutakiwa kuitangaza nafasi hiyo katika magazeti ya hapa nchini. Pale ambapo atakosa kumpata mfanyakazi mzalendo mwenye sifa zilizoainishwa, mwekezaji ataruhusika kuajiri mfanya kazi wa kigeni. Serikali hufanya tathmini ya maombi hayo na kujiridhisha kwamba nafasi hizo haziwezi kujazwa na wazawa ndipo hutolewa vibali husika. Aidha, Muekezaji akiajiri mfanyakazi wa kigeni anatakiwa kufuata masharti ya kuwafundisha/kuwajengea uwezo wazawa ili kuwaandaa kushika nafasi hiyo.

(b) Mhe. Spika, Jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kunapatikana ufanisi kupitia uwekezaji wa ndani na nje ni pamoja na kufanya marekebisho ya Sera na Sheria zinazohusu Uwekezaji nchini zenye changamoto ili ziweze kuleta ufanisi katika masuala ya uwekezaji.

Kuweka Mfumo mmoja wa utoaji wa huduma kwa wawekezaji (*One Stop Center*) ili kupunguza na kuondosha urasimu wa utoaji pamoja na kuimarisha uratibu wa utekelezaji kwa taasisi zote zinazosimamia masuala ya uwekezaji nchini. Huduma za *One Stop center* zinaendelea kuwanufaisha wawekezaji kwa kuwaondolea kero na usumbufu wa ufuatiliaji vibali na leseni mbali mbali katika taasisi tofauti.

Uimarishaji wa utoaji wa elimu kwa jamii na wawekezaji ili kuwa na uwekezaji wenye tija utakaoleta manufaa na maendeleo kwa nchi na wananchi wenyewe.
Kuimarisha upatikanaji wa miundo mbinu ya kisasa na huduma mbali mbali kama vile barabara, maji, umeme na mawasiliano ili kuimarisha ufanisi katika sekta ya uwekezaji

Kujenga uwezo wa taasisi kutoa huduma imara na endelevu pamoja na kuwajengea uwezo vijana kuweza kupata fursa mbali mbali za ajira katika miradi ya uwekezaji ni miongoni mwa jitihada za Serikali.

Serikali imeweka Sheria maalum kwa ajili ya kuwawekea mazingira mazuri ndugu zetu wana Diaspora kuja kuwekeza nchini na tayari muitiko mkubwa umeanaza kuonekana.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri jibu ni refu sana yaani jitahidi sana msijibu kama hutuba, Mhe. Dkt. Sada Mkuya Salum swali la nyongeza.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza, ninayo maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Waziri. Mhe. Spika, nadharia ya mambo yalivyo (*theory*) ni nzuri sana lakini shida inakuja katika utekelezaji wa nadharia ambayo sisi tumeipokea.

a) Nimulize Mhe. Waziri tathmini ya faida ya uwekezaji kwa Zanzibar katika kipindi cha miaka 10 iliyopita imefanyika lini.
b) Lakini swali la pili Mhe. Spika, wakati tunachangia ya Mhe. Rais *specifically* nilichangia kuhusiana na uwekezaji ambao umefanywa na wenzetu hapa ndani sehemu ya *airport* yetu ya Zanzibar na nilimuliza sana Mhe. Waziri wale waajiriwa pale kwa maana ya wazawa wana mazingira mabaya ya utendaji kazi

pamoja na changamoto nyengine na Mhe. Waziri aliyewatembelea lini utangalia kwa kina na kuwapelekea majibu ya maswali yao ambayo walikutaka wewe kuyafatilia.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Samahani Mhe. Spika, naomba arejee swali la pili.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Mhe. Spika, wakati tunachangia *speech* ya Mhe. Rais ambayo aliitoa hapa mimi nilipokuwa nimechangia nilimuomba Mhe. Waziri kwamba kutokana na uwekezaji ambao umefanywa katika *airport* yetu ya Zanzibar kimataifa wazawa ambao ni wafanyakazi wa pale wana mazingira magumu na mara ulikwenda ukawaona na ukawahikikishia kwamba madai yao ambayo wanayadai utayafanyia kazi na majibu yatapatikana sasa lini majibu yatapatikana kwa yale madai ambayo wewe uliwahidi kwamba utayafuatilia.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Saada Mkuya salum maswali yake kama ifuatavyo:-

a) Kuhusu tathmini ya uwekezaji na faida ambayo tumeipata mpaka sasa hivi kama nchi, miradi ya uwekezaji ambayo tumeweza kuekeza mpaka sasa hivi katika nchi inafika zaidi ya kiradi mia saba na, ambapo mia nne ipo katika hatua ya utekelezaji lakini *capital* ambayo imekuwa *injected* katika uchumi wetu kutokana na miradi hio ni zaidi ya hiyo SD Bilioni 7 ambazo zimengia mpaka sasa hivi na kuzalisha ajira zisizopungua 70,000 kwa hivyo, katika kipindi cha miaka 10 ambacho tumekiona tangu tuanze kualika wawekezaji kuna *huge capital injection* ambayo tayari imengia katika nchi na ajira zilizotolewa ziwe za kutosha.

   Vile vile kama tunavyofahami sehemu kubwa uwekezaji ambayo inafanyika katika visiwa vyetu asilimia 60 inaenda katika sekta ya utalii na tunaona ni kwa kiasi gani sekta ya utalii inavyoajiri vijana wetu kiasi cha kwamba hata ugonjwa wa corona ulipopiga umeona juinsi gani uchumi wetu ulivyotetereka. Kwa hivyo, uwekezaji huu una tija na tuna kila wajibu kama serikali kuendelea kuhakikisha kwamba tunajenga mazingira rafiki kwa wawekezaji wetu kuendelea kuja kuekeza. Jambo la msingi kabisa pia ni sisi kuweka ile miundombinu ya kuweza kuwavutia zaidi wawekezaji hao na kuleta wawekezaji ambao wana tija zaidi katika nchi yetu na kuwajibisha katika kulipa kodi lakini kuna tija kubwa sana ambayo tunaipata kutokana na uwekezaji huo.

b) Kuhusu swali lako la pili juu wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika Shirika la *ZATI* ni kweli kwamba tulitoa ahadi ya kushughulikia tatizo lao na hiyo kazi imeshaanza tumeshafanya vikao visivyopungua viwili na *management* pamoja na wafanyakazi na tume *direct management* ya

*ZATI* kuhakikisha kwamba wana- *address* zile *issue* zao ambapo miongoni mwao ni kuboresha mazingira ya kazi kuhakikusha kwamba wanavitendea kazi salama, kuhakikisha kwamba wanalipwa malipo yao ya *over time,* kuhakikusha kwamba wanalipwa stahiki zao zile za *night shift allowance* lakini wanawekewa masuali yao vizuri ya *ZSSF* pamoja na Bima. Na nitowe taarifa tu kwamba uongozi wa *ZATI* tumeshakaa nao sana tu kuyajadili mambo hayo kwa sababu ni uongozi ambao kimsingi ulikuwa kama vile haupo kulikuwa hakuna hata *HR manager* lakini sasa hivi wana *HR manager*. Kwa hivyo, nina imani kwamba kadri siku zinavyoendela matatizo yao yatazidi kuratibiwa nah ii kazi tayari imeshaanza.

**Mhe. Ali Suleiman Ameir:** Nakushukuru Mhe. Spika, nashkuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri lakini nitaomba kumuliza swali dogo moja lenye kitoto (a) na (b).

a) Ni utaratibu gani ambao serikali unauchukua kwa kuhakikusha wataalamu wageni wanarisisha ujuzi kwa wataalamu wazalendo ili fursa ya ajira za wataalamu wageni ziweze kurithiwa na wataalamu wazalendo baada ya kumaliza muda wao kwa sababu tumeona sheria ya ajira na sheria ya *ZIPA* inaruhusu wataalamu wa kigeni waajiriwe kuna sababu fulani baada ya kumaliza zile sababu je, ujuzi huo hatua gani serikali unachukua ili kurudisha kwa wazalendo.
b) Sababu ambazo zinapelekea wageni kutotoa fursa nyingi za ajira kwa wazalendo ni uwepo wa tozo au kodi nyingi. Je, wizara yako inachukua hatua gani ya kuwasaidia wawekezaji hawa kuwapunguzia kodi au tozo nyingi ili waweze kutoa fursa nyingi kwa wazalendo.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

a) Kuhusu ku-*transfer skills* kwa wenyeji utaratibu ambao upo kwa sasa hivi nikuhakikisha tu kwamba kunakuwa kuna usimamizi mzuri wa kutekeleza ile programu ambayo imewekwa na kuna programu maalum ambazo tumeziweka kwa ajili ya kufanya jambo hilo. Jambo kubwa ni usimamizi wake tu na ku-*make sure* kwamba linatekeleza vile ambavyo imepangwa na serikali.

b) Kuhusu suala la tozo ambazo tunazitoa kwa wawekezaji ni zile ambazo kimsingi zimewekwa kisheria kwa hivyo *revision* ya tozo manake lazima tuje tuijadili humu ndani ili tuweze kuzirekebisha. Lakini tozo zote zilizokuwepo ni zile ambazo zipo kisheria lakini tunahitaji kuweka mazingira ambayo itakuwa ni rafiki mwisho wa siku kwa sababu tunataka wawekezaji lakini tuweke mazingira ambayo serikali itanufaika na wao vile vile watanufaikia.

**Mhe. Sulubu Kidongo Amour:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza nashkuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini nataka nimuulize swali la nyongeza ndani ya jimbo langu bahati nzuri tumepata nafasi ya uwekezaji mwingi sana wa mahoteli, lakini Mhe. Waziri, unasimamia vipi utendaji wa mahoteli katika hoteli kwa sababu kwenye hoteli kuna *swimming pool*, *swimming pool* zinakuwa zikishachoka maji maji yale wanayamwaga baharini lakini wakimwaga maji baharini wananchi wangu wanakosa kulimwa mwani kwa sababu yale maji yaka *calcium* na mwani umeshapotea kutoka Kilimajuu mpaka kigomani hakuna mwani sasa hivi kwa sababu ya *swimming pool* ambazo zinafanyakazi na hao wawekezaji. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Mhe. Spika, naomba mjunbe aniambie jimbo lake ni la wapi.

**Mhe. Spika:** Naam.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Jina la jimbo lake.

**Mhe. Spika:** Mkwajuni, endelea Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Kuhusu usimamizi wa mahoteli na utendaji wa kazi zao tuna maofisa wetu kazi ambao kimsingi wao jukumu lao ni kufuatilia utendaji wa waajiri na namna ambavyo wanahusiana na waajiriwa. Lakini vile vile kwa sababu wamezungumzia suala la mazingira na haya maji ambayo yanakwenda katika bahari kwa ajili ya kuwakwaza wakulima wa mwani, niseme tu kwamba maafisa wale wanaosimamia usalama kazini wao ndio jukumu lao sasa kuja kuhakiki masuala ya mazingira na kuhakikisha kwamba hoteli zile zina-*compile* zile *standard* zetu ambazo tumeziwekea.

Kwa hivyo, hatua za kuchukua ni kuhakikisha kwamba maafisa wetu wanafika katika hayo maeneo kukagua kuhakiki kuzungumza na *management* na kama hakuna *compiles* basi ni kuchukua hatua za kisheria zinazostahiki kwenye zile *violation* ambazo zimefanyika.

## Nam. 7

## Kuimarisha Maeneo ya Hifadhi Zanzibar

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis -** Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kwa kuimarisha Maeneo ya Hifadhi ya misitu na kuweka utaratibu mzuri wa kunufaisha vijiji vilivyopo jirani na maeneo hayo.

Ni faida gani iliyopatikana katika vijiji vilivyomo katika maeneo hayo na vijiji vingapi vimeweza kunufaika Unguja na Pemba.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye kipengele a, b na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka kweli imeimarisha maeneo ya Hifadhi ya Misitu na kuweka utaratibu mzuri wa kunufaisha vijiji 9 vilivyopo jirani na maeneo hayo vikiwemo Kitogani, Bwejuu, Pete, Michamvi, Ukongoroni, Charawe, Chwaka, Cheju na Unguja Ukuu ambavyo vinavyozunguka Hifadhi ya Jozani kwa Unguja na vijiji 10 vya Hifadhi ya Ngezi Pemba vikiwemo Makangale, Jiwe Moja, Kijini, Tondooni, Mkia wa Ng'ombe, Bandari Kuu, Kiuyu kwa Manda, Kiuyu Kipangani, Msuka Gombani na Mji Mpya ambavyo vinanufaika na utaratibu huo.

Mhe. Spika, utaratibu huo unategemewa kuendelea kwa maeneo mengine ya uhifadhi na faida iliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Spika, upo mgao unaotokana na faida ya utalii wa kimaumbile ambayo wanapatiwa wanajamii wanaozunguka maeneo hayo kwa kufanyia miradi tofauti ya kujiongezea kipato na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

2. Mhe. Spika, wanavijiji kupatiwa mafunzo ya uanzishaji wa miradi hiyo ya kujiongezea kipato ikiwemo, ufugaji nyuki kibiashara, vitalu vya miche, ufugaji wa vipepeo, kilimo mseto mashamba ya miti kwa kuwapatia mafunzo pamoja na vitendea kazi. Jumla ya wanajamii 568 (wanawake 237 na wanaume 331) walipatiwa mafunzo hayo na vitendea kazi vya ufugaji nyuki, ikiwemo mizinga, vifaa na zana za kuvunia pamoja na vifaa vya kuchakatia mazao ya nyuki, vyenye thamani ya Dola 10,181 na vitendea kazi vya uzalishaji wa miche ya misitu na matunda ikiwemo mbegu na vifuko. Jumla ya mizinga 180 ilitolewa na wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

3. Mhe. Spika, kuanzisha miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa vyoo 2 (Kiuyu cha kwa Manda) na ujenzi wa majiko 2 Mkombozi yamejengwa (Kiuyu Kipangani) pia ujenzi na ukarabati wa shule, Msikiti na madrasa.

4. Mhe. Spika, kupatikana kwa ajira za moja kwa moja kwa wanajamii 43 (wanawake 13 na wanaume 30) kwa utembezaji wa wageni na ulinzi wa msitu wa Jozani na Pemba kumeanzishwa mfumo wa ugawaji wa mapato yanayopatikana Ngezi.

5. Kwa kupewa vibali huruhusiwa kukusanya ukindu, madawa na matunda.

6. Vile vile kuuza bidhaa zao kwa watalii kupitia kwenye duka lao.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini hata hivyo naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa wananchi wengine wa maeneo ya hifadhi ambao bado hawajanufaika na hifadhi wana hamu kubwa ya kuona na wao wananufaika na utaratibu huo. Katika majibu ya Mhe. Waziri alisema kwamba utaratibu huo unategemewa kuendelea kwa maeneo mengine ya uhifadhi.

Je, Mhe. Spika, ni maeneo gani hayo ambayo yanatarajiwa kuendelea na utaratibu huo, ili wananchi wa maeneo hayo waweze kukaa tayari na kujipanga kwa kusubiri neema hiyo ahsante.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Spika, naomba nimjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis wa viti maalum. Mhe. Spika, katika maeneo ambayo tunatarajia kuanzisha tena Kijiji cha Kiwengwa, Masingini, Kisiwa cha Vundwe ambacho kimepakana na Uzi Ng'ambwa na Msitu wa Muyuni Jambiani. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, nakushukuru naomba nimuulize Mhe. Waziri mwalimu wangu swali la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Jimbo la Micheweni ni eneo ambalo kuna fursa nyingi za hifadhi za misitu zile za asili, pamoja na hifadhi za jamii ambazo kwa jina la kitaalamu wanasema Hifadhi za Koko, lakini kwa kule kwetu Hifadhi za Mikandaa. Maeneo hayo hifadhi hizo ni nyingi.

Kwa mfano, Shumba Mjini, Kiumbuyuni kwa Moga, Maziwa Ng'ombe, Mitambuni na Zangale. Hayo ni maeneo ambayo hifadhi zake ni kubwa na ambazo zinapendeza kwa sasa.

Je, Mhe. Spika, ni lini wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa kuwa na wao wameanzisha hifadhi nyingi na ambazo zimeonesha tija sana, utafika angalau kuwapa taaluma na wao waweze kufaidika na mpango huu ambao wenzetu wa kule Jozani na maeneo ya Makangale wanaendelea kufaidika nazo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Ahsante Mhe. Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Shamata Shaame Khamis wa Jimbo la Micheweni. Kwa kweli ninafurahi sana, unajua mwalimu unapoulizwa swali na mwanafunzi wako kwa kweli unapata faraja kwamba unajua kuwa kweli mwanafunzi wangu ameiva na wewe unapata sifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kweli nimueleze Mhe. Mjumbe, kwamba niko tayari kukaa pamoja na yeye kwa kushirikiana pamoja na kuweza kuwapa elimu ili wajuwe kuna faida gani ya hifadhi ya misitu ambazo kama nilizozitaja hapo, kwamba kwanza watapata mgao na kuona ni jinsi gani tunaweza kufanya huu utalii wa maumbile ambao katika maeneo yote yanayozunguka kwenye maeneo hayo kufanya miradi na kuongeza kipato kwa maeneo ya jamii kwa jumla, kwa vivyo tutashirikiana kwa pamoja. Ahsante.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Msitu wa Ngezi una uharibifu mkubwa unafanyika wa mazingira, ikiwemo ukataji wa miti. Lakini pia vile vile inasemekana kwamba kunapikwa gongo mule ndani yam situ.

Je, unalijua hili na kama hulijui ni lini utalifuatilia ili kuhakikisha kwamba msitu ule tunaendelea kuulinda na kuuenzi.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Mhe. Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Suleiman Makame Ali, namwambia kwamba niko tayari kushirikiana na yeye katika kuhifadhi msitu huo. Vile vile nimueleze kwamba kila msitu basi tuna walinzi wetu ambao wanaiangalia ili kuhakikisha kwamba uharibifu haufanyika kwa kuhifadhi mazingira ambayo yanazunguka katika maeneo hayo. Ahsante Mhe. Spika.

**Nam. 34**

**Utaratibu wa Kuimarisha Upatikanaji wa Elimu Bora Zanzibar**

**Mhe. Hassan Hamad Omar** – Aliuliza:-

Katika malengo ya maendeleo endelevu (*SDGs*) Nam. 4 imeelezwa kuwa kuhakikisha kuna elimu bora inayotolewa kwa usawa na kutengeneza fursa za kujiendeleza kwa wote.

(a) Je, kwa nini katika wizara yako imekuwa na ubaguzi wa Uunguja na Upemba katika kusimamia mitihani.

(b) Je, kwa nini inapodhaniwa kuvuja mitihani kwa baadhi ya maskuli, wanafunzi huadhibiwa kwa kufutwa matokeo lakini waliovujisha hawachukuliwi hatua yoyote.

(c) Je, utalitatua vipi janga la uvujaji wa mitihani maskulini.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi: (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 34 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, suala la ubaguzi wa Uunguja na Upemba katika kusimamia mitihani ya Taifa halina ushahidi wowote, na kwa herufi kubwa Mhe. Spika, sikubaliani kabisa na madai hayo. Wasimamizi wa Mitihani ya Taifa huteuliwa kwa kuzingatia Miongozo ya Mitihani ya Baraza la Mitihani la Zanzibar na Baraza la Mitihani la Tanzania ambapo sifa za Msimamizi zimeainishwa bila ya kubagua Muunguja au Mpemba. Mwalimu yeyote

anaweza kuwa Mtungaji, Msimamizi na Msahihishaji wa Mitihani ikiwa atakidhi vigezo vilivyowekwa na mamlaka inayoratibu shughuli hizi vikiwemo uaminifu, uadilifu pamoja na uzoefu wake wa kazi.

(b) Mhe. Spika, Wanafunzi wanaobainika kufanya udanganyifu na kuthibitishwa, hufutiwa matokeo yao kwa mujibu wa Kanuni za Mitihani za Baraza la Mitihani la Zanzibar za mwaka 2015 Kifungu Namba 58(1). Kwa uvujaji wa Mitihani, Mamlaka zinazohusika hufanya uchunguzi kutafuta aliyehusika na ikithibitika kuwa amefanya kosa hilo, Sheria huchukuwa mkondo wake.

(c) Mhe. Spika, wizara inajitahidi kwa kiasi kikubwa kuhakikisha uvujaji wa mitihani hautokei. Miongoni mwa hatua inazochukuwa kutatua janga hili ni kutoa elimu kwa jamii ili waelewe athari za uvujishaji wa mitihani kwa wanafunzi, wazazi na Taifa kwa jumla. Kutafuta mianya inayopelekea uvujaji wa mitihani na kuweka mikakati ya kuziba mianya hiyo na kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaobainika kuhusika na uvujaji wa mitihani na kuwafikisha katika vyombo vya kisheria. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Nakushukuru Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza dogo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kusimamia mitihani kuna watu wanaitwa *supervisor*, hawa wanapata kiwango kidogo cha fedha kuliko waliokuwa chini yao.
Je, suala hili unalijua, na kama unalijua ni lini usumbufu huu utaondoka ili kila mtu apate haki yake anayostahiki.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Mhe. Spika, samahani naomba arudie kidogo sijafahamu vizuri. Yaani *supervisor* halafu sikumpata vizuri.

**Mhe. Spika:** Rejea swali la mwanzo akusikie Mhe. Waziri.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Waziri swali la nyongeza liko hivi. Katika usimamiaji mitihani kuna mtu anaitwa *supervisor* ambaye ni mkuu kuliko wote, na kuna wengine wako chini yake. Lakini utaona huyu mkuu anapata kiwango kidogo cha fedha kuliko wengine walioko chini.

Je, suala hili unalijua, na kama unalijua usumbufu huu utaondoka lini.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza napenda nimshukuru kwa swali lake na kama alivyomuita *supervisor*, maana yake ndio keshakuwa *super*, maana yake ukisema kitu *super* maana yake hicho kinakuwa ni kikubwa zaidi ya chengine.

Kwa hivyo, *supervisor* katika taratibu kwa sababu katika malipo ni kwamba kuna viwango vyake, sio wote wanalipwa sawa sawa. Kwa hivyo, *supervisor* kwa sababu yeye anakuwa ndio *overall*, kwa hivyo malipo yake yeye yanakuwa makubwa kulikoni wale walimu wengine.

Kwa hivyo, suala hili nalijua kwa sabab ndio utaratibu ulivyo na sio kama ni kosa, kwamba kwa sababu yeye labda ndio *supervisor* kapendelewa, hapana, ndio utaratibu Mhe. Mjumbe ambao unatumika.

Mhe. Spika, katika hili na kwa sababu *supervisor* ana-*supervise* walimu wote ambao wanasimamia mitihani. Lakini mwalimu ambaye anasimamia mitihani yeye akimaliza darasa lake ana-*submit paper* anampa *supervisor, supervisor* mengine yote yeye ndiye ambaye anamalizia. Kwa hivyo, anakuwa na kazi kubwa ya ziada ya kuhakikisha kwamba hili jambo linakwenda vizuri. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Mihayo Juma Nhunga:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza na mimi nitumie fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili la uvujaji wa mitihani linakwenda sambamba na stahiki za walimu wanaokwenda kusahihisha mitihani, na sasa kuna kilio kikubwa cha walimu cha kusikitika kwa kutokulipwa pesa zao tokea kumaliza kusahihisha mitihani ya Kidato cha Pili.

Je, ni lini sasa serikali itakwenda kulikamilisha hili ili tupunguze ule ukakasi wa kuwa tunasingiziana suala zima la kuvujisha mitihani. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mihayo Juma Nhunga Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mwera swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.
Mhe. Spika, serikali kama ambavyo inahimiza ni kwamba kuona kila ambaye anatoa jasho lake, basi analipwa kabla jasho lake halijakaula. Katika miaka yote kwenye Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inahakikisha kwamba mwalimu hata kabla hajamaliza kusimamia mitihani ama kusahihisha basi fedha zake anakuwa anazipata. Kama hilo limetokezea basi itakuwa ni katika yale mapungufu ambayo tunazungumza kutokana na hali kidogo ilivyo.

Kwa hivyo, kama liko hivyo basi nimuombe Mhe. Mjumbe, kwamba serikali itafanya kila jitihada ili kuhakikisha kwamba zikiingia tu basi na walimu nao wanapewa kipaumbele katika kuona wanapata fedha zao. Nakushukuru Mhe. Spika,

**Mhe. Habib Ali Mohamed:** Mhe. Spika, ahsante sana. Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kunakuwa na malalamiko mengi ya walimu wakati wa usahihishaji wa mitihani ya kitaifa.

Je, ni vigezo gani ambavyo vinatumika kuwapata walimu ambao wanakwenda kusahihisha mitihani ya Darasa la Kumi na Mbili na Kumi na Sita ya Tanzania Bara.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mhe. Habib Ali Mohamed Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kuhusiana na malalamiko mengi ya walimu, maana yake bora angetuambia ni malalamiko ya aina gani, hapo ingekuwa ni rahisi zaidi kuweza kusema malalamiko yako vipi. Lakini kusema tu kwa ujumla malalamiko mengi. Mhe. Spika, malalamiko yako mengi kweli katika jamii yetu, kila mmoja analalamika kwa namna yake.

Kwa hivyo, suala la walimu kuchaguliwa ni kwamba Baraza la Mitihani la Tanzania... Samahani Mhe. Spika, maana yake nilikuwa nimepotea kidogo. Suala la vigezo vya walimu ambao wanasahihisha mitihani ni kwamba Baraza la Mitihani la Tanzania kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, sambamba na Baraza la Elimu la Zanzibar kwa sababu lile ni mpaka *Form II,* Baraza la Elimu la Tanzania Bara mpaka *Form IV* na *Form VI.*

Mhe. Spika, ni kwamba wanapokuwa wanawataka walimu wanakuwa wanatoa *specification* zao za walimu kwa mujibu wa masomo husika. Ikiwemo sifa za mwalimu, uzoefu wake katika kazi na uzoefu katika lile somo ambalo analifundisha. Kwa hivyo, hicho ndio ambacho kinatumika.

Lakini Mhe. Spika, hatuwezi kuwachukua walimu wetu wote wakenda kusahihisha mitihani, kwa sababu hazitotosha hizo nafasi. Kwa hivyo, wanaokwenda ni miongoni mwa walimu, lakini katika kila somo ambalo linapaswa kuwe na mwalimu, basi walimu wanapelekwa kwa Unguja na Pemba yake. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Wahudumu wetu msiwapelekee vi-*note* mawaziri wakati wanajibu, vyenginevyo iwe hicho ki-*note* kinasaidia katika hilo jibu lenyewe, mbali na hapo msiwapeleke kwenye *podium.*

**Nam. 80**

**Changamoto za Ufaulu kwa Wanafunzi wa Sekondari kwa Upande wa Zanzibar**

**Mhe. Aza Januar Joseph -** Aliuliza:-

Naelewa kuwa Elimu ya Msingi hadi Sekondari si suala la Muungano, bali Baraza la Kutunga Mitihani *(NECTA)* na Elimu ya Juu ni ya Muungano.

(a) Je, ni changamoto zipi zinazokabili skuli zetu hasa za serikali kutokufanya vizuri katika mitihani ya kidato cha nne na cha sita huku tukielewa kwamba tunamitaala mmoja kwa Tanzania nzima.

(b) Je, serikali imejipanga vipi kuhakikisha wanafunzi wetu wanaofanya mitihani yao vizuri kama vile wanavyofanya wanafunzi wa Tanzania Bara.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kweli zipo changamoto mbali mbali zinazokabili skuli zetu kutofanya vizuri katika mitihani ya Kidato cha Nne na cha Sita huku tukielewa kwamba tunatumia mtaala mmoja kwa Tanzania nzima. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa mwamko mdogo wa wanafunzi katika kufuatilia masomo yao, uchache wa walimu hasa wa masomo ya Hesabati na Fizikia na upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, ikiwemo maabara zilizokidhi viwango vinanvyohitajika. Aidha, kuwepo kwa wanafunzi wengi katika Darasa moja inanyima mazingira bora ya kujifunza, baadhi ya wazazi na jamii kutokushiriki katika kusimamia elimu ya watoto wao na utoro kwa baadhi ya wanafunzi.

(b) Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tayari imepanga mikakati mbali mbali ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wanafanya vizuri katika mitihani yao, kama vile wanavyofanya wanafunzi wa Tanzania Bara. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na:-

i. Kufanya makongamano na wadau wa elimu wakiwemo wazazi, walezi, kamati za skuli, walimu na jamii kwa jumla katika kuwasaidia watoto masomo yao,
ii. Kuimarisha uwezo wa walimu kwa kuwapatia mafunzo kazini,
iii. Kuimarisha huduma za dahalia na kuhakikisha kila Mkoa unajengewa skuli ya kisasa yenye huduma za dahalia, ili wanafunzi wapate muda mzuri wa kukaa pamoja na kusaidiana katika masomo.
iv. Kuzizawadia skuli zinazofanya vizuri katika mitihani yao na walimu wanaoonesha jitihada katika ufaulu mzuri wa wanafunzi wao.
v. Kutumia Vituo vya Ubunifu wa Kisayansi katika kuwaimarisha wanafunzi na walimu katika Lugha ya Kiingereza, ili kuongeza ufahamu wa masomo katika ufaulu wa mitihani yao hiyo.
vi. Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia,
vii. Katika ambayo nimeyasema miongoni mwao ni kujenga majengo ya skuli yenye huduma zote na vifaa vya masomo ya Sanaa na Sayansi vya kisasa. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Azza Januar Joseph mwenyewe naona ameridhika. Mhe. Shaaban Ali Othman kwa swali la nyongeza.

Aaa! Mhe. Azza Januar Joseph amenyanyuka mwenyewe naona, haya. Lakini Waheshimiwa Wajumbe, tujitahidi kama una swali la msingi na unahisi unataka kuuliza swali la nyongeza.

**Mhe. Aza Januar Joseph:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize...

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, *microphone* inyanyue vizuri kwa sababu husikiki, waziri hakusikii.

**Mhe. Aza Januar Joseph:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekubali changamoto.

Je, wizara ina juhudi gani za kuhakikisha wanapata walimu na maabara zenye viwango ili kuondosha tatizo hili.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Aza Januar Joseph swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumza katika jibu mama ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inahakikisha kwamba inajenga skuli ambazo zina miundombinu ya kisasa, maabara za kisasa ili kukabiliana na tatizo hili.

Lakini katika suala la walimu, upungufu wa walimu hasa wa sayansi ni kwamba tunawahamasisha wanafunzi wetu kusoma masomo ya sayansi lakini kusomea masomo ya ualimu ili kupata walimu katika masomo haya.

Katika hatua za haraka haraka pia Mheshimiwa ambalo tunalifanya ni kwamba tunapozidiwa tunaazima walimu kwa masomo haya kutoka kwa ndugu zetu wa Nigeria katika ule urafiki wa nchi yetu ya Tanzania na Nigeria tunakuwa tunazima walimu ili kuweza angalau kusaidia nguvu katika suala hilo nakushukuru Mheshimiwa.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya serikali lakini naomba nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, hivi karibuni kumesikika tangazo kutoka kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kuanzishwa na kufundishwa kwa somo la historia ya Tanzania. Sasa kwa mnasaba wa Muungano wetu na hoja ya kutumika kwa mtaala mmoja Tanzania nzima nataka majibu ya serikali inafahamu kwa kiwango gani uwepo wa suala hili na SMZ imeshiriki kwa kiasi gani katika kuandaa somo hilo.

b) Kupitia maslahi ya Zanzibar au kwa kuzingatia maslahi ya Zanzibar serikali imejiandaa vipi kuhakikisha historia yake inaandikwa inahifadhiwa na kufundishwa vyema pamoja na kuingizwa katika somo hilo ili kuepuka upotoshaji wa historia kubwa na nzuri ya Zanzibar. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Shaaban Ali Othman, Mwakilishi wangu wa Jimbo Mpendae swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Nina imani kwa sababu jana alikuwa juu kwa hiyo inawezekana hili swali pia hakulisikia vizuri, lakini jana tulizungumza swali hili la historia katika maswali yetu.

a) Mhe. Spika, ni kwamba kuanzishwa kwa somo la Historia kwa Tanzania nzima Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar inalitambua imeshirikishwa na hivi ninavyozungumza miongoni mwa watendaji wetu ambaye ni Mkurugenzi wa Mitaala wa Taasisi ya Zanzibar yuko Dodoma pamoja na wadau wa Tanzania Bara wanaendelea katika kuzungumza na katika kupanga kuhusiana na zile mada ambazo zimo katika Mtaala huo wa Historia.

   Labda naomba niseme kwamba bado haijathibitishwa ile mitaala kwamba kuanza kutumika ni katika yale maandalizi lakini Zanzibar tumo na katika hilo ni kwamba mada ambazo zinahusu Zanzibar kwa maana kwamba historia ya Zanzibar maana yake itakuwa ni miongoni mwa hiyo historia ambayo itaingizwa. Lakini Mhe. Spika, kama ambavyotunajua Mitaala yetu kwa kidatu cha kwanza mpaka cha nne Mitaala yetu inafanana isipokuwa kwa msingi ndio ambayo tunakwenda katika ngazi tofauri.

   Kwa sababu hili bado halijamalizwa kuthibitishwa, kwa hiyo, watakapomaliza mpango mzuri utaandaliwa twende vipi katika ngazi za sekondari au na msingi je, iwe vipi hayo yote ni masuala ambayo yatazungumzwa. Niwaombe sana waheshimiwa kwamba tulisubiri limalizike ili tuweze kupata ufumbuzi mzuri sana.

b) Mhe. Spika, ni kwamba katika kuhakikisha historia ya Zanzibar inahifadhiwa vizuri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa sasa inaendelea katika kupitia mitaala yake ya Maandalizi pamoja na Msingi. Kwa hiyo, katika upitiaji wa mitaala hii inaangalia masomo yote likiwemo na somo la historia na katika kuweka mkazo kuhakikisha kwamba ile historia yetu basi inaendelea kufundishwa vizuri ili vijana wetu wazidi kujenga ule uelewa wa kizalendo kwa nchi yao. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante. Waheshimiwa nitatoa maswali mawili zaidi hapa ya nyongeza moja atauliza Mhe. Hassan Khamis Hafidh na la pili atauliza Mhe. Zawadi Amour Nassor. Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kuniona asubuhi hii. Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali anayekaimu maswali mawili ya nyongeza yenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tarehe 23/09/1964 Mzee Abeid Amani Karume alitangaza Elimu Bila ya Malipo na tarehe 23/09/1989 tulikutana Amani tunaimba robo karne imefika kwamba kusoma kwa matabaka tajiri na maskini sasa tunafaidika sote tulio nchini.

Mhe. Spika, lakini sasa tunaona kama watoto wa wakwezi na wakulima wanyonge wanaosoma maskuli ya serikali hawafaidiki kwa sababu ndio maskuli mengi yanayofelisha. Mhe. Spika, Zanzibar tumeona juzi mitihani skuli iliyopasisha ni skuli kama Feza na nyenginezo ambazo zinalipiwa. Sasa Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwa nini watoto wengi wamefeli katika mitihani yetu iliyopita.

Halikadhalika Mhe. Spika, tunafuata mtaala wa Bara na Bara mwisho darasa la saba sisi mwisho darasa la sita. Hatuoni kama tunaji-*confuse ourself* tunasababisha watoto wetu kufeli ambao wasiohusika.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli sote tunafahamu kuwa elimu ndani ya Zanzibar ni bure kama ambavyo Mhe. Rais wetu Mzee Abeid Amani Karume muasisi *Allah* amrehemu huko aliko alitangaza Elimu Bila ya Malipo tarehe 23/09/1964. Katika hili Mhe. Spika, kusema kwamba watoto wa wanyonge hawafaidiki sisi tuliomo humu ndani wengi wetu ni watoto wa wanyonge na tumefaidika katika hizo hizo skuli ambazo Mhe. Rais Karume aliziasisi na kutangaza elimu bure, tumo humu ndani katika nafasi zetu ambazo tulizonazo na wengine wapo nje ambao pia wamefaidika.

Sasa changamoto ambayo imetokezea kutokana na ufaulu Mhe. Spika, naomba sana tusi- *generalize* tukasema kwamba watoto hawafaidiki tutakuwa tunaikosea serikali yetu na tutakuwa tunayakosea Mapinduzi yetu Matukufu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiri kwamba kweli changamoto ya matokeo imetokezea ya vijana wetu kwamba baadhi yao kutokufanya vizuri na hii kama ilivyo jina lake mtihani ni mtihani hakuna aliyekuwa *king* kwenye mtihani. Mtihani unawezekana ukawa rahisi jawabu yake ikawa ngumu lakini vile vile inawezekana ikawa jawabu ngumu swali likawa rahisi.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, katika kuhakikisha kwamba hili linafanyika vizuri katika jawabu yetu mama tulisema mikakati mbali mbali ambayo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaipitia ili kuhakikisha kwamba ubora wa ufaulu kwa vijana wetu unafanikiwa.

Katika hili azma ambayo Mhe. Rais wetu aliianza kuita wadau wa elimu wote kwa pamoja kutoa maoni yao ili kuhakikisha kwamba tunakwendaje ili kuona changamoto hizi nazo tunazipiga na tunaziweka pembeni ili kuona vijana wetu wa Kizanzibari wanang'ara na wanafanya vizuri zaidi katika masomo yao. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Hassan Hafidh Khamis:** Kuhusu utaratibu Nam. 64

**Mhe. Spika:** Hapana Mheshimiwa naomba ukae. Mhe. Zawadi Amour Nassor kwa swali la nyongeza.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lako la awali ulisema kwamba miongoni mwa njia zinazotumika kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi ni ujenzi wa madakhalia inavyoonesha ni kwamba Skuli ya Sekondari Madungu ilikuwa imo katika mpango wa ujenzi wa dakhalia. Napenda nikuulize swali langu linalosema kwamba ni kitu gani kilichopelekea Skuli ya Madungu isijengewe dakhalia hadi sasa.

Lakini kwa sasa wizara ina mpango gani kuhakikisha imejenga skuli yenye dakhalia ukizingatia wanafunzi wanaopelekwa pale wanatoka mikoa tofauti ya Pemba.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwalim Zawadi Amour Nassor swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli nilisema katika jawabu yetu mama kwamba miongoni mwa mambo ambayo yanapelekea ufaulu mzuri ni kuwepo kwa dakhalia katika skuli zetu, na tulisema kwamba tunahakikisha katika kila mkoa tutajenga skuli hizi. Skuli ya Madungu si skuli ya dakhalia wala ilivyojengwa mwanzo haikuwemo katika miongoni mwa skuli za dakhalia hili naomba niliweke bayana.
Sasa kilichopo Mhe. Spika, ni kwamba Skuli ya Madungu ni skuli ya michepuo kama zilivyo skuli nyengine za Ben Bella na Tumekuja kwa Unguja lakini vile vile kwa baadhi ya skuli ambazo zipo Pemba.

Kwa hiyo, skuli ya michepuo kama ilivyo ni kwamba wanafunzi wanakwenda na kurudi nyumbani kwao, kinachotokezea kwa Madungu kutokana kwa juhudi ambazo zipo katika ile skuli ni kwamba wazazi wengi wanapenda kuona watoto wao wanasoma katika ile Skuli ya Madungu. Kwa hivyo, kutokana na hali hiyo wanatoka katika maeneo mbali mbali wanataka wasome pale. Kwa sababu inavyotakiwa wale ambao wapo karibu ya lile eneo ndio wasome lakini wengine wanakwenda wizarani kuomba mwanangu naomba apelekwe Madungu.

Mhe. Spika, serikali yetu ni sikivu mzazi akija kuomba serikali inakuwa haina hiyana ya kumnyima. Kwa hivyo, wazazi wengi wanapata fursa hiyo ya kuacha watoto wao kusoma katika Skuli ya Madungu. Lakini yenyewe si dakhalia, lakini nini labda kifanyike kuona kwamba tunapata dakhalia ni kwamba tukiona bajeti ikiwa vizuri tukipata fedha basi serikali vile vile itafikiria kuweka dakhalia katika eneo ambalo litakuwa lipo karibu ya Madungu. Lakini kwa upande ule pale wa Chake Chake ni kwamba Skuli ya Fidel Castro ndio skuli ambayo ina dakhalia mpaka sasa. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Nam. 17**

**Changamoto ya Maji katika Baadhi ya Maeneo ambayo Mabomba ya Maji Yanang'olewa katika Ujenzi wa Barabara**

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Kny. Mhe. Machano Othman Said ) –** Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya kazi kubwa na nzuri ya ujenzi wa barabara ya Bububu hadi Mkokotoni. Hata hivyo, wakati wa ujenzi huo baadhi ya mabomba ya maji yaling'olewa hivyo kuleta shida ya maji kwa wananchi wa maeneo husika.

(a) Kwa kuwa ujenzi wa barabara hiyo umekamilika, ni lini huduma hiyo ya maji itarejeshwa tena.

(b) Je, ni nani mwenye wajibu wa kurejesha huduma hiyo kati ya mjenzi wa barabara hiyo na Serikali.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 17 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, huduma ya maji itarudishwa kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar ambao ni mkopo kutoka *Exim Bank* ya India. Miongoni mwa maeneo yatakayonufaika na mradi huo ni eneo la Mfenesini ambalo litalazwa mabomba ya maji kwa ajili ya kuwahudumia wakaazi wote wa maeneo hayo na maeneo ya jirani.

(b) Mhe. Spika, naomba nijibu kwamba mwenye jukumu la kurejesha huduma hiyo ni Serikali kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda kuuliza maswali ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa Mradi huu wa Barabara ya Mahonda Mkokotoni umemaliza kipindi kirefu na wananchi wa maeneo haya wamekosa maji kwa kipindi kikubwa. Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuchelewa kurejeshwa huduma katika maeneo hayo.

b) Kwa kuwa eneo la Fuoni Polisi limekumbwa na kadhia kama hiyo wakati wa kujengwa barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni. Je, ni lini *ZAWA* watarejesha huduma ya maji safi na salama katika eneo hilo. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Yussuf Hassan Iddi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba barabara ya Mfenesini au iliyoanzia Bububu – Mfenesini kuelekea Mahonda imemalizika kwa muda na ni kweli kwamba hatua ya kurejesha huduma katika eneo hilo bado imechelewa. Kwa sababu Mhe. Spika, mradi ambao nimeueleza wa India tayari umeshaanza utekelezaji na hili ndilo ambalo limepelekea kutokurejesha ile huduma ya mwanzo ambayo ingelazimika kurejesha huduma ile baadae tukaondoa tukarejesha huduma hii kubwa. Ndio maana serikali imeona kwamba kwa sababu mradi huu mkubwa utaanza muda mfupi ujao ni vyema tukapitisha *line* katika maeneo yaliyoathiriwa na barabara kwa kupitia mradi huu mkubwa.

Kwa sababu ukataji wa maeneo hayo unaweza ukawa ni wa mara kwa mara, kwa hiyo, tukianza sasa hivi tutakata na baadae tuje tukate tena haitopendeza katika ujenzi wa barabara.

Mhe. Spika, suala la kurejesha huduma katika eneo la Fuoni wizara kupitia Mamlaka ya Maji imeshapanga mpango wa kurejesha huduma katika eneo hilo na maeneo mengine yote ambayo yamekosa huduma hii muhimu.

**Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, tatizo hili limekuwa likilalamikiwa kila leo na kwa bahati njema kila tunapojaribu kufanya miundombinu mipya hususan ya barabara huwa linajichomoza.

Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri. Je, hawaoni kama ipo haja sasa hivi kukaa wao Wizara ya Maji, Nishati na Madini lakini na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili kuandaa ile *reserve space* kwa ajili ya miundombinu kama hii. Kwa sababu tunaona kila siku matatizo haya yanakuwepo lakini mwisho wa siku tunapotaka kuingiza miundombinu tunatafuta namna ya kuziharibu barabara zetu ambazo tunazijenga kwa gharama kubwa.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Samahani Mhe. Spika, hilo la mwisho sikulipata.

**Mhe. Spika:** Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma unaweza kurudia swali la mwisho.

**Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma:** Mhe. Spika, swali langu ni moja ninachosema ni kwamba tumekuwa tuna changamoto ya ukatwaji wa barabara lakini kuna changamoto ambayo tunaipata pale tunapotengeneza njia kama huu ukosekanaji wa maji. Hili nahisi kwa maoni yangu ni kwamba linakwenda sambamba na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa maana hiyo, nauliza hamuoni kama ipo haja ya kuweza kukaa pamoja wizara hizi ili kuona hili tatizo linaondoka na wananchi wetu kupata huduma, lakini na sisi tukaweza ku-*reserve* lile eneo letu. Mhe. Spika, nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma swali lake limeanza na ushauri kwanza. Tuseme ushauri huo tumeupokea na tumeshaanza utaratibu wa kukaa pamoja kwa yale yote ambayo tunakwenda kwenye mradi kuhakikisha kwamba tunapopita tunapita kwa pamoja, ili kuondoa ule usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza kwa muda mrefu wa ukataji wa barabara pamoja na urejeshaji wa huduma hii muhimu.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar :** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na mimi naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linauliza maswali haya ya miundombinu ya barabara namna ambavyo yamekwenda kubomoa miundombinu ya maji, kadhia hii pia ipo katika Shehia ya Mgogoni ambapo vijiji kama Ditia, Tondooni, Misufini na Kichangani vijiji vyote hivyo vimekosa maji. Je, ni lini vijiji hivi vitarejeshewa huduma hiyo ya maji.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Bakar Hamad Bakar Mwakilishi wa Jimbo la Wawi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nikiri kwamba kumekuwa na changamoto hii ambayo Mhe. Mwakilishi ameieleza, lakini nimuahidi kwamba serikali kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* imepanga kurejesha huduma hizo katika maeneo yote ambayo yana changamoto na tuna mpango maalum wa kuyapitia maeneo yote kutathmini na kurejesha huduma hii muhimu. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Mwakilishi awe na subira kidogo lakini pia nimuahidi kwamba nitapita mimi mwenyewe katika Jimbo la Wawi kuangalia maeneo hayo na kuhakikisha kwamba huduma hii tunairejesha haraka iwezekanavyo.

**Nam. 13**

**Mauzo ya Karafuu katika Soko la Nje ya Nchi**

**Mhe. Mussa Foum Mussa -** Aliuliza:-

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Shirika la *ZSTC* lilifanya mauzo ya tani 5,640 za karafuu zenye thamani ya U$ 26,661,620 sawa na shilingi bilioni 61.05 kwa nchi ya India na Singapore.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa sasa bado bei iko nzuri.

(b) Je, Serikali inawaeleza nini wakulima wa zao la karafuu juu ya kuongezewa bei kwa Serikali yao hii ya Awamu ya Nane.

**Mhe. Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji) -** Alijibu:-

Ahsante sana, Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi Mussa Foum Mussa swali lake Nam. 13 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hali ya soko la karafuu duniani haikuwa nzuri na bei yake imeshuka kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo kwa kipindi cha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21 bei ya karafuu katika soko la dunia iko kwa wastani wa Dola za Kimarekani 4,700 kwa tani moja ambayo ni sawa na shilingi za Tanzania 10,857,000/= .

(b) Kwa vile Serikali kupitia Shirika la *ZSTC* imekuwa ikifidia wakulima wa zao hilo kwa kipindi cha takribani miaka mitatu sasa kutokana na bei ya karafuu kushuka katika soko la dunia, hali ambayo imelipelekea Shirika la *ZSTC* kuwa na madeni mengi kutoka Taasisi za Fedha na ambayo imekuwa ni vigumu kuyalipa. Ni vyema kwa Serikali kurejea katika utaratibu uliokubaliwa awali wa kumpatia mkulima wa zao la karafuu asilimia 80 ya bei ya soko. Hali hii itapelekea mkulima kunufaika kwa kiasi na vile vile kuwaondolea mzigo mkubwa Shirika la *ZSTC* kwa kufidia tofauti ya bei ya kununulia na kuuzia.

Aidha, hali hii itaendana na uhalisia wa biashara ambapo mkulima atapata malipo kulingana na bei ya soko ambapo endapo bei ya soko itapanda basi mkulima atapata zaidi na endapo bei itashuka basi mkulima atapata bei ambayo inaendana na uhalisia wa soko lilivyo.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

(a) Mhe. Waziri, kwa kuwa umetueleza kwamba Serikali ilikuwa ikifidia wakulima juu ya zao hili la karafuu baada ya bei kuanguka na kwa kuwa mwaka huu tunategemea karafuu imeshazaliwa kwa wingi. Je, Mhe. Waziri anawaeleza nini wakulima juu ya hii bei iliyokuwepo, itaendelea hii au itashuka.

(b) Kwa kuwa serikali ina mpango wa kujenga Kiwanda cha Mwani baada ya wakulima kuleta manung'uniko makubwa juu ya bei ya mwani hivi sasa. Je, serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda kwa ajili ya karafuu ili kutoa bidhaa zinazotokana na karafuu hapa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mussa Foum Mussa maswali yake kama ifuatavyo. Kuhusu bei ambayo ipo hivi sasa kwenye soko la dunia ni kwamba karafuu inauzwa kwa shilingi 10,000 kwa kilo, lakini bei ambayo inalipwa na serikali ni shilingi 14,000 kwa kilo. Kwa maana hiyo, serikali inalipa zaidi ya ile bei ambayo ipo katika soko la dunia, hiyo tayari ni fidia, ni *subsidy* ambayo kimsingi inaitia hasara kubwa sana serikali kwa sababu hali halisi ya soko haiendani na namna ambavyo tunainunua.

Sasa ushauri ambao tumeutoa na ndio ambao nimeutoa katika jibu langu la msingi ni kwamba twende kwenye bei elekezi ya kulipa asilimia 80 ya bei ambayo itakuwepo katika soko. Kwa hii bei ambayo tupo nayo sasa hivi haiwezi kuwa endelevu kutokana na hali ilivyo kwa sasa. Kwa hiyo, kuna umuhimu kwanza wa kurudi katika bei hiyo elekezi. Lakini bei elekezi kwa sasa hivi kama utachukua hiyo 10,000 kama utalipa asilimia 80 ina maana bei ya karafuu itashuka kutoka 14,000 ambayo tunalipa sasa mpaka shilingi 8,000 kama utaichukua bei ya sasa hivi. Kwa hiyo, hili sio suala la kukurupuka tu, ina maana kwamba kwanza ni lazima tukae na wadau kushauriana, kujua kwamba kweli tunataka kwenda katika bei hiyo elekezi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mpango wa kutengeneza Kiwanda cha Karafuu hilo lipo katika mipango ya serikali na ni kweli ni jambo ambalo linahitajika kwa sababu ni muhimu sasa tukienda katika kuongeza thamani ya zao letu la karafuu baaada ya kuuza karafuu ghafi ambayo changamoto yake tunaiona kama sasa hivi. Bei kule inapoporomoka inabidi tuuze karafuu yetu ambayo hatujaiongezea thamani na matokeo yake tunakuwa tunapoteza mapato makubwa kwa serikali. Kwa hiyo, *solution* endelevu ni hiyo ya kutengeneza viwanda ambapo mkakati huo upo na kuna baadhi ya wawekezaji ambao tumeshaanza kuongea nao kutoka Indonesia kwa ajili ya kufanya uwekezaji wa aina hiyo.

**Nam. 45**

**Matengenezo ya Barabara ya Kangani - Mtambile na Mtambile Kengeja**

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha** – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ujenzi wa barabara nyingi na za kisasa kisiwani Pemba ili kuwapunguzia umaskini wa kipato wananchi wetu hususan barabara ya Kangani – Mtambile na Mtambile Kengeja ambazo muda mfupi baada ya kuanza matumizi zinachimbika na kuharibika vibaya.

(a) Je, serikali inafahamu uharibifu huo.

(b) Je, ni lini serikali itazifanyia matengenezo barabara hizo ili kuwaondoshea adha wananchi wanaozitumia.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mohamed Mgaza Jecha swali lake Nam. 45 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ndio Serikali inafahamu uharibifu huo.

(b) Mhe. Spika, tatizo kubwa la kuharibika mara kwa mara kwa barabara zetu ni kwamba barabara zetu nyingi ni za muda mrefu na kwa sasa zinahitaji kujengwa upya. Serikali itatenga fedha kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara alizozitaja Mhe. Mjumbe na kuzipandishia lami *(overlay)* ili kuziongezea uimara na umri wa matumizi yake kama ilivyoainishwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020-2025 ibara ya 165(c) ya kuendeleza utunzaji na matengenezo ya barabara zilizokwisha kujengwa. Ahsante.

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ningependa kumuuliza swali moja la nyongeza. Hizi barabara anazozitaja Je, ameshazitembelea.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri umeshafanya ziara kwenye hizo barabara.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mohamed Mgaza Jecha swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Katika barabara hizi sijazitembelea lakini mpango wa kuzitembelea ninao kwa sababu barabara ni nyingi, kwa hivyo tumezianza nyengine na tunahakikisha barabara zote tutazitembelea. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante Waheshimiwa kwa sababu ya muda naomba nilimalize na swali la mwisho. Katibu wizara inayofuata.

**Nam. 83**

**Kutolewa kwa Elimu na Nyenzo kwa Uvuvi wa Bahari Kuu**

**Mhe. Shamata Shaame Khamis -** Aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Micheweni wamekuwa na shauku kubwa juu ya kauli na mikakati ya Serikali zinazotolewa na Mhe. Rais wa Awamu ya Nane na wanaendelea kumuombea hasa katika muelekeo wa Uchumi wa Buluu.

Je, ni lini Wizara itatoa elimu na nyenzo zenye ufanisi kwa wananchi wa Jimbo la Micheweni ambao kwa kiwango kikubwa wanapata mahitaji yao ya lazima kupitia bahari.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi -** Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shamata Shaame Khamis swali lake Nam. 83 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali imepanga kutoa elimu ya nyenzo zenye ufanisi kwa wananchi katika mpango wake wa maendeleo wa miaka mitano 2020 -2025 ambapo kila mwaka itatekeleza mpango huo  ili kuwapatia wananchi mahitaji yao ya lazima kupitia bahari katika Wilaya zote za Unguja na Pemba pamoja na vitongoji vyake ikiwemo Jimbo la Micheweni.

Hivyo, wananchi na jumuiya mbali mbali za kiserikali na zisizo za kiserikali tunaziomba kutoa mashirikiano yao katika muda wote wa utekelezaji wa mpango huu kwa ajili ya kuendeleza uvuvi, ufugaji bora wa samaki na mazao mengine ya baharini, pamoja na usarifu wa zao la mwani na dagaa kwa madhumuni ya kupata maendeleo endelevu kupitia Uchumi wa Buluu.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya serikali ambayo yana dhamira ile ile. Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali dogo la nyongeza naomba nitoe maelezo mafupi sana.

Mhe. Spika, katika Jimbo la Micheweni tuna wavuvi 3,285 ambao ni *registered*. Lakini vile vile tuna wakulima wa mwani wasiopungua 6,189, lakini vile vile wataalam aliokuwa nao Mhe. Waziri mpaka sasa hivi ni wawili tu wizara nzima, kwa wilaya nzima ana wataalam hao na idadi hii ya wakulima ambao nimewataja na wavuvi ni kwa jimbo moja tu la Micheweni.

Mhe. Spika, nilitaka kujua kuwa mpaka sasa hivi tukiwa na mpango huu wa 2020-2025 ni jambo lipi ambalo au ni kazi gani ambayo tayari imeshaanza kufanyika katika Jimbo la Micheweni ambalo lina *population* kubwa ya wavuvi ambao wametambuliwa na serikali.

Mhe. Spika, vile vile nataka kujua kwamba kumekuwa na matatizo makubwa yanayowapata wavuvi wetu, hususan wanapo kuwepo baharini kwa kupoteza maisha na wakati mwengine kupotea baharini. Tukiwa katika muelekeo wa Uchumi wa Buluu, ni hatua gani ambazo wananchi wetu hao wazifuate na wapi wafike wakati wanapofikwa na matatizo hayo hususan pale katika kutafuta kupata huduma nyengine kama za uokozi ili kuwapunguzia Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi mzigo mkubwa zaidi. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Spika, naomba arejee swali lake la mwanzo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Shamata Shaame Khamis, swali la mwanzo.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, nilitaka kujua baada ya takwimu hizo ambazo nimezitoa. Kwa sasa, kwa sababu mpango huo ni wa 2020-2025 ambao utatekelezwa. Wizara kwa upande wa Jimbo la Micheweni au kutokana na *population* hii ambayo nimeitaja ya wavuvi na wakulima wa mwani na idadi ya wafanyakazi aliokuwa nao ni kazi shughuli gani ambazo tayari kwa muda huu, kwa kasi hii ya Awamu ya Nane kipi ambacho kimeshaanza kufanyika katika eneo hilo.

Lakini vile vile, nimesema kwamba wavuvi wanapokuwepo baharini wanakabialiana na changamoto nyingi na wakati mwengine kupotea baharini, kutumia vifaa vikawaletea madhara wakati mwengine vifo. Wakati wanapotaka kwenda kuokolewa na taswira na *population* hii tuliyokuwa nayo, tunataka kujua wavuvi wapi waanzie wawafuate wataalam hawa wawili katika ofisi zipi au wapi waweze kupata hizo huduma nyengine za msaada za uokozi ili kuwapunguzia Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi kuchangia fedha kwa ajili ya uokozi na mambo mengine. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako nafikiria ningeomba kwamba tulete majibu kwa maandishi kwa vile ni wizara ambayo bado sijaielewa vizuri. *(Makofi)*

## TAARIFA ZA SERIKALI

### Hotuba ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022-2023/2024

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na kuweza kukutana leo hii katika Kikao cha Kujadili Mapendekezo ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021-2022 hadi 2023-2024.

Pili, nichukue nafasi hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa imani kubwa aliyoinesha dhidi yangu ya kuniteua kuiongoza Wizara hii muhimu kwa taifa letu.
Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kwake kuwa Makamu wa kwanza wa Rais lakini vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa zanzibar.

Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa kuchaguliwa *either* kwa kuteuliwa au kuchaguliwa kuja katika chombo hichi. Napenda pia kuchukua fursa hii adhimu kuungana na wananchi wote wa zanzibar kwa kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa imani kubwa aliyoipata kwa wazanzibari kuchaguliwa kuongoza Awamu ya Nane kwa ushindi wa kihistoria.

Mwaka huu wa Fedha  2021-2022 tunaouanza na Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya zanzibar yenye muundo wa umoja wa kitaifa. Hali kadhalika, hii ni Bajeti ya kwanza inayoanza kutekelezwa chini ya dira mpya ya maendeleo ya Mwaka 2050.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu. Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021-2022 hadi 2023-2024. Mapendekezo hayo yatatanguliwa na mapitio na mwenendo wa uchumi wa mwaka 2020. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa nusu mwaka ya Mwaka 2021 na Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya nusu mwaka ya 2020-2021. Nawasilisha pia matarajio ya Mapato na Matumizi hadi kufikia Juni 2021.

Mhe. Spika, waraka huu unatokana na matakwa ya kifungu cha 105 cha Katiba ya Zanzibar 1984, kinachomtaka Waziri anaehusika na masuala ya Fedha kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha kutayarisha na kuwasilisha katika Baraza lako la Wawakilishi Makadirio ya Bajeti ya Mwaka unaofuata.

Aidha, kifungu cha 39(1) cha Sheria ya Fedha ya Umma Nam.12 2016, kinamtaka Waziri anaesimamia Fedha kuandaa Muelekeo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka unaofuata na kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi matakwa  haya yanayoendana sambamba na Kanuni ya 93 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi inayotaka serikali kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu muelekeo wa mpango wa taifa kwa mwaka unaofuata katika kikao cha mwezi wa Februari cha Baraza la Wawakilishi.

Mapitio ya Uchumi kidunia. Mhe. Spika, kufuatia mripuko wa maradhi ya *Corona* yaani *Covid 19* Mwezi Disemba, 2019. Uchumi wa dunia uliporomoka kufikia asilimia 3.5 kwa Mwaka 2020, kutoka ukuaji wa asilimia 2.8. ukichangana na kuporomoka kwa uchumi wa umoja wa ulaya ambao uliporomoka hadi kufikia ukuaji wa hasi 7 asilimia kutoka asilimia 1.3.

Nchi ya Marekani uchumi ulikuwa unakuwa kwa hasi ya asilimia 3.4 kutoka asilimia 2.2. Nchi zinazoibukia kiuchumi nazo pia zilikumbana na changamoto, uchumi wao ulikuwa kwa hasi 3.3 asilimia kutoka ukuaji wa asilimia 2.9. Pamoja na nchi zinazoendelea ki viwanda pia uchumi ulikua kwa kasi 2.4 asilimia kutoka kukua kwa asilimia 3.6.

Mhe. Spika kwa upande wa Afrika uchumi umeripotiwa kushuka kwa asilimia 1.7 kwa mwaka 2020 ikiwa ni anguko la kutoka asilimia 5.6. Huku uchumi wa Nchi za Afrika Mashariki ulikuwa kufikia asilimia 5.2, Kenya asimilia 6, Uganda asilimia 2 na Tanzania asilimia 5.2.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani hadi kufikia Februari 10, 2021 idadi ya watu inayofika milioni 106.6 ambao Afrika ilikuwa na watu takriban milioni 2.7, Marekani milioni 47.4, Ulaya milioni 36, Kusini Mashariki mwa Asia milioni

13.1 na nchi nyenginezo zilikuwa na asilimia 7.4 zimeambukizwa ugonjwa huo duniani kote. Katika idadi hiyo milioni 2.3 wamefariki dunia.

Aidha, kwa taarifa za kitaalam za afya maambukizi ya maradhi haya ni ya haraka sana lakini hayasababishi vifo kwa haraka ambapo idadi ya wagonjwa wapatao milioni 78.4 kati ya waliopata maradhi haya wameweza kupona.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na athari ya janga la maradhi ya *COVID 19*, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuchukua hatua mbali mbali katika kuhakikisha ina imarisha uchumi wake na kukabialiana na athari za kiuchumi ambazo zimejitokeza kutokana na kuwepo kwa janga hili.

Miongoni mwa  hatua hizo, ni kupunguza masharti yaliyowekwa na kuanza kuruhusu baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii kuendelea. Kufungua vyuo vya Elimu ya juu, kufungua Shule kwa kuwapa nafasi wanafunzi kwa kipindi kile cha Kidato cha nne na cha Sita kujitayarisha na Mitihani na kwa kufanya hivyo skuli hizi ziliendelea kuendeshwa kama kawaida.

Kuanza kuruhusu kupokea Watalii kutoka nchi tofauti duniani. Tano, kuruhusu safari za ndege kuingia na kutoka nje ya nchi. 6. Kuruhusu shughuli za biashara za ndani kuwa wazi katika nyakati za kawaida na 7. Kuendelea kutoa tahadhari za ugonjwa na kusaidia kupigana na kuushinda ugonjwa huo.

Hatua nyengine zilizotumika katika kuimarisha Mapato ya Serikali na kusaidia kurahisisha shughuli za kibiashara ni pamoja na zifuatazo.

Moja, ilikuwa ni kupunguza kiwango cha tozo ya kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT* kutoka asilimia 18 hadi asilimia 15. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani *VAT* kwa vifaa vya uvuvi ikiwemo boti kubwa za kuanzia urefu wa mita 18 na zaidi, mashine za boti pamoja na vifaa vyengine vya uvuvi vinavyoingia nchini.

Pili, ilikuwa ni kupunguza kiwango cha kutoza ushuru wa hoteli kutoka asilimia 18 hadi asilimia 14. Kufuta tozo na ada zote kwa wafanyabiashara wadogo wa masokoni, mama lishe, waanika dagaa na wa jua kali ya shilingi elfu moja hadi elfu mbili kwa siku. Hivi sasa wanachotakiwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa wafanyabiashara hawa watalipa kiwango kimoja cha ada ya shilingi elfu thelathini kwa mwaka na kupewa kadi maalum ya usajili na utambulisho.

Tatu, ilikuwa kupunguza kiwango cha ada za usajili wa uwekezaji kinachotozwa na Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar yaani *ZIPA* kutoka dola za Kimarekani mia tano hadi dola za Kimarekani mia mbili.

Nne, kupunguza kiwango cha leseni ya biashara inayolipwa kwa Mawakala wa Forodha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutoka shilingi laki tatu hadi milioni moja na kuwa kiwango kimoja cha shilingi laki tatu. Kwa maelezo zaidi, naomba rejea hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Makadirio ya Mpango wa

Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka 2020/ 2021 katika ukurasa wa 53 hadi 54. Hata hivyo, hali ya uchumi wa Zanzibar katika kipindi hicho iliendelea kuwa kama ifuatavyo.

Kwa upande wa mfumko wa bei. Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2020 kasi ya mfumko wa bei ya bidhaa na huduma imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 1.9 kutoka asilimia 2.6 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019. Bei za chakula zimepanda na kufikia wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 2.7 kwa mwaka 2019. Bei zisizo za chakula zimeshuka na kufikia wastani wa asilimia 1.5 kwa mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 2.5 kutoka mwaka 2019.

Mwenendo wa biashara. Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2020 nakisi ya biashara imeongezeka na kufikia jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 440.5 kutoka shilingi za Kitanzania bilioni 383.9 kwa mwaka 2019. Kuongezeka kwa nakisi ya biashara kumesababishwa na kuongezeka kwa uwingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2020. Uagizaji wa bidhaa umefikia jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 458.7 ikilinganishwa na thamani ya shilingi za Kitanzania bilioni 411.7 kwa mwaka wa 2019. Bidhaa zilizoingizwa nchini kwa kiwango kikubwa ni bidhaa za biashara ambazo zilikuwa kwa aslimia 51.9, bidhaa za chakula ambayo ilikuwa jumla asilimia 18.8 na bidhaa za kati yaani *intermediate goods* ambazo zilikuwa asilimia 29.3.

Mhe. Spika, aidha, usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi umepungua katika kipindi cha Julai hadi Disemba na kufikia thamani ya shilingi bilioni 18.2 mwaka 2020 kutoka thamani ya shilingi bilioni 33.8 kwa mwaka 2019. Ununuzi wa zao la karafuu katika Julai – Disemba mwaka 2020 umepungua na kufikia tani 206.5 ambazo ni thamani ya shilingi bilioni 2.8 kutoka tani 1638.5 ambazo zilikuwa na thamani jumla ya shilingi bilioni 22.9 mwaka 2019. Kupungua kwa ununuzi wa zao la karafuu kumesababishwa na kupunguwa kwa uzalisha wa zao hilo kutoka wakulima nchini. Usafirishaji wa zao la karafuu nje ya nchi katika kipindi cha Julai – Disemba mwaka 2020 imefikia jumla ya tani 946.4 ambazo zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 9.9 ikilinganishwa na jumla ya tani 1,884.4 ambazo zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 20.3 kwa mwaka 2019.

Mwenendo wa uingiaji wa utalii. Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai – Disemba mwaka 2020 idadi ya wageni walioingia nchini imepungua na kufikia wageni 1,002,746 kutoka wageni 335,374 kwa mwaka 2019. Ikiwa sawa na upungufu wa asilimia 69.4. Kupungua kwa uingiaji wa idadi ya wageni nchini kumesababishwa na kuwepo maradhi ya *Corona* yaliyopelekea kuwekwa vizuizi vya kusafiri nje ya nchi kwa nchi nyingi na kuzuia safari za ndege kutoka nchi mbali mbali.

Mhe. Spika, utekelezaji wa *MKUZA III* ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2020 ambapo imefanikiwa katika maeneo kadhaa ikiwemo: Moja, kupunguza asilimia ya watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini uliokithiri kufikia aslimia 9.3 mwaka 2019 – 2020 ambapo lengo lilikuwa ni kufikia asilimia 10.

Pili, kufikia kiwango cha chini cha nchi zenye uchumi wa kati yaani *low middle income country*. Tatu, kuongeza matarajio ya umri wa kuishi kutoka miaka 48 hadi kufikia miaka 65. Nne, kuimarisha na kudumisha viwango vya elimu na kukuza maendeleo ya ujuzi kwa kuzingatia gharama. Tano, ni upatikanaji wa maji safi na salama ambao umefikia asilimia 9.8. Sita, ukuaji wa uchumi ambao umefikia asilimia 7 kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2019.

Mhe. Spika, dhamira ya MKUZA ilikuwa ni ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii kwa manufaa ya wote. Dhamira hii imeweza kufikiwa ambapo takwimu zinaonesha kuwa Zanzibar imekuwa na ukuaji wa uchumi endelevu ambapo kwa miaka mitatu imekuwa kwa asilimia 7. Mfumko wa bei umefikia kuwa chini ya asilimia 5 ambapo mwaka 2019 mfumko wa bei ulishuka na kufikia asilimia 2.7 na kiwango cha watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini kimeshuka kufikia asilimia 25.7 kwa mwaka 2019 ukilinganisha na asilimia 30.4 kwa mwaka 2014/2015. Ujumbe wa MKUZA ni kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii yenye hadhi ya uchumi wa kati. Lengo hili limefikiwa kwani takwimu za mwaka 2019 zinaonesha kuwa Zanzibar imefikia kiwango cha chini cha uchumi wa kati yaani *low middle income country* kwa kuwa kipato cha mtu mmoja cha dola za Kimarekani 1,114.

Utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa kipindi cha miezi sita yaani Julai – Disemba, 2020. Mhe. Spika, utekelezaji wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ni umaliziaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar awamu ya tatu yaani *MKUZA III* ambapo umekamilika mwaka 2020. *MKUZA III* imeendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii na kupunguza umaskini kwa:

Moja, kuwezesha ukuaji wa uchumi jumuifu na endelevu. Pili, kukuza uwezo wa watu. Tatu, kutoa huduma bora kwa wote. Nne, kuweka mazingira endelevu na uhimili wa mabadiliko ya tabia nchi. Tano, kushikamana na misingi ya utawala bora.

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ulilenga kutekeleza jumla ya programu na miradi 94 ambayo jumla ya thamani yake ilikuwa ni shilingi bilioni 609.9 zilipangwa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mpango huo ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 32.9 sawa na asilimia 5.7 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo ya mwaka 2019/2020 ambayo ilikuwa shilingi za Kitanzania 57,577,000,000. Kati ya fedha hizo serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi 197.3 sawa na asilimia 32.3 ya bajeti ya maendeleo kutoka katika fedha za ndani. Jumla ya shilingi bilioni 412.6 sawa na asilimia 67.6 zilipangwa kutolewa na washirika wa maendeleo ikiwemo shilingi bilioni 72.5 ni ruzuku na shilingi bilioni 340.5 mkopo.

Mhe. Spika, hadi kufikia Disemba, 2020 jumla ya shilingi 139,000,000,000 sawa na asilimia 22.9 ya lengo la shilingi bilioni 609.9 zilitumika katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi za Kitanzania bilioni 37.6 sawa asilimia 19.1 ya lengo la shilingi bilioni 197.3 zilitoka serikalini na shilingi bilioni 101.74 sawa na asilimia 24.7 za lengo la 412,000,000,000 zilitoka kwa washirika wa maendeleo.

Utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa kipindi cha Julai – Disemba mwaka 2020. Mhe. Spika, ili kuhakikisha utekelezaji wa *MKUZA III* unafanyika kwa ufanisi, miradi mbali mbali ilipewa kipaumbele ili kufikia malengo ya maendeleo na kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi. Programu na miradi iliyopewa kipaumbele cha juu katika utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa mwaka 2020/2021 ni kumi na tatu nayo ni kama ifuatavyo:-

Moja, kuimarisha uchumi baada ya athari ya maradhi ya *Corona* kwa kutekeleza mpango wa kuimarisha uchumi yaani *economic recovery plan*. Mbili, ilikuwa ni ukamilishaji wa jengo la tatu la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. Tatu, kuimarisha Uchumi wa Buluu kwa kuandaa mpango wa matumizi wa bahari na maeneo yake na kuanza utekelezaji. Nne, ujenzi wa Hospitali mpya ya Rufaa Binguni. Tano, ujenzi wa Hospitali ya Wete kwa kuipandisha hadhi kuwa Hospitali ya Mkoa. Sita, kukamilisha ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu. Saba, kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Chaani, Kinyasini na Kibokwa kwa Unguja na Makwararani na Mlele kwa Pemba.

Nane, ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri. Tisa, kuendelea ujenzi wa Mji wa Kisasa wa Kwahani. Kumi, kuimarisha Sekta ya Mafuta na Gesi kwa kuendelea na ujenzi wa miundombinu wa matangi ya kuhifadhia mafuta katika eneo la Bandari ya Mangapwani. Kumi na moja, kuimarisha ulinzi na usalama. Kumi na mbili, ujenzi wa barabara ya Chake Chake – Wete na kumi na tatu, ujenzi wa Kituo cha Maonesho ya Mikutano ya Kimataifa katika eneo la Nyamanzi ambao ulitarajiwa kukua katika mfumo wa mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi. Kati ya vipaumbele hivyo ni vipaumbele tisa sawa na asilimia 69.2 ambavyo vimeanza utekelezaji wake katika kipindi hichi na kuwepo katika hatua mbali mbali.

Mhe. Spika, jumla ya shilingi bilioni 256.6 zilipangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vya kwanza ambavyo kwa kipindi cha Julai – Disemba kiasi cha fedha zilizopatikana jumla ya shilingi bilioni 55.9 sawa na asilimia 21.7 ya bajeti ya mwaka. Kwa upande wa vipaumbele vya pili jumla ya shilingi bilioni 18.5 zimepangwa kutumika katika kipindi cha miezi sita na kiasi kilichopatikana ni shilingi bilioni 2.7 sawa na asilimia 15.

**Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/2021 kwa kipindi cha miezi sita cha Julai – Disemba, 2020**

**Ukusanyaji halisi wa mapato ya serikali**

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 serikali imekadiria kukusanya jumla ya shilingi trilioni 1.579 ikijumuishwa na mapato ya ndani ya trilioni 1.05, mikopo ya ndani ya jumla ya shilingi bilioni 45, Mfuko wa Pamoja wa Washirika wa Maendeleo jumla ya shilingi bilioni 3.8 na shilingi bilioni 419.4 ruzuku na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi bilioni 61 ikiwa ni sehemu ya marejesho ya ujenzi wa *Terminal III* kutoka kwa benki ya *Exim* ya China.

Mhe. Spika, kutokana na athari ya *COVID-19* kwa kipindi cha miezi sita yaani Julai hadi Disemba, 2020 serikali imekusanya jumla ya shilingi bilioni 464.6 sawa na asilimia 59.6 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 779.4 zikiwemo mapato ya ndani ya shilingi bilioni 303.3 sawa asilimia 58 ya makisio ya shilingi bilioni 522.7 katika kipindi hichi.

Mikopo ya ndani jumla ya shilingi bilioni 57.3 sawa na asilimia 126.7 ya makisio ya shilingi bilioni 50.4 katika kipindi hiki. Mapato kutoka kwa washirika wa maendeleo ya shilingi bilioni 104.3 sawa na asilimia 50.6 ya makasio ya shilingi bilioni 206.3 katika kipindi hichi.

Mapato kutoka kwa washirika wa maendeleo. Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai – Disemba, 2020 serikali imepokea jumla ya shilingi bilioni 104.2 sawa asilimia 50.6 ya makadirio ya miezi sita ya shilingi bilioni 206.2 zikiwemo ruzuku ya shilingi bilioni 8.5 na mikopo ya shilingi bilioni 95.7 kwa ajili ya miradi na programu mbali mbali za maendeleo.

**Utekelezaji halisi wa matumizi**

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai – Disemba, 2020 – 2021 jumla ya matumizi halisi yamefikia shilingi bilioni 486.7 sawa na asilimia 76.8 ya makisio ya shilingi bilioni 634 ya lengo katika kipindi hichi. Kati ya matumizi hayo, bilioni 351 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 74.2 ya makisio ya shilingi 475.8 bilioni na 133.6 bilioni zilitumika kwa shughuli za maendeleo sawa asilimia 84 ya makisio ya 158.2 bilioni. Kati ya fedha hizo, shilingi 37.7 bilioni zilitumika kutokana na fedha za serikali katika miradi ya maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 69.9 ya makisio ya shilingi bilioni 53.9 na shilingi 95.9 bilioni zinatokana na washirika wa maendeleo sawa na asilimia 91.9 ya makadirio ya shilingi 104.3 bilioni.

**Matumizi ya mfuko wa miundombinu**

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya mfuko wa miundombinu jumla ya shilingi 42.2 bilioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi 15 kwa mwaka huu. Katika kipindi cha miezi sita jumla ya shilingi bilioni 10.2 zimetumika kutoka katika mfuko wa miundombinu kwa kugharamia miradi nane sawa asilimia 23 ya makadirio ya shilingi bilioni 42.2.

**Matumizi ya serikali za mitaa**

Mhe. Spika, jumla ya shilingi bilioni 81.2 zilichangwa kwa ajili ya ruzuku kwa mwaka 2020/2021 ambapo shilingi bilioni 70.9 matumizi ya ruzuka haya yalikuwa mishahara na shilingi bilioni 10.3 ni matumizi ya kuendesha ofisi na aidha matumizi halisi kwa kipindi cha Julai – Disemba yamefikia shilingi bilioni 39.7 sawa na asilimia 97.8 ya makadirio ya shilingi bilioni 40.6 ya lengo katika kipindi hichi. Kati ya matumizi haya shilingi 38.3 bilioni zilitumika kwa mishahara sawa na asilimia 108 ya makadirio ya shilingi 35.4 bilioni na shilingi 1.41 bilioni zilitumika kwa matumizi

ya kuendesha ofisi sawa na asilimia 27.3 ya makadirio ya shilingi 5.2 bilioni katika kipindi hichi.

**Deni la Taifa**

Mhe. Spika, katika kipindi cha miezi sita hadi kufikia Disemba, 2020 deni la taifa limefikia jumla ya shilingi bilioni 896.2. Deni hilo liliongezeka kwa shilingi 74.1 bilioni sawa na asilimia 9 ikilinganishwa na deni lililoripotiwa katika mwezi Disemba, 2019 ambapo lilikuwa shilingi bilioni 822.5. Mhe.Spika, kati ya deni hilo, deni la nje ni shilingi 691.5 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 95.9 ambalo deni hili linadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na asilimia 4.1 lipo chini ya udhamini wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Deni la ndani ni TZS 204.9 bilioni ambalo ni kutoka *ZSSF* (TZS 51.7 bilioni) na hatifungani kutoka *BoT* (TZS 154.1 bilioni).

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Disemba, 2020 wastani wa uwiano wa Deni la Taifa kwa Uchumi *(Public debt to GDP ratio)* ni asilimia 22, ikiwa ni chini ya kiwango cha ukomo kinachokubalika kimataifa cha asilimia 50. Kiwango hicho cha deni kinaashiria kwamba hali ya deni letu kwa sasa ni himilivu. Hata hivyo, hadhari inapaswa kuendelea kuchukuliwa kwani tayari kuna mikopo iliyokwisha sainiwa na hivyo pindi pesa zake zitakapotolewa zitabadilisha taswira hiyo ya uwiano wa deni na pato la taifa.

**MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/2021**

**Matarajio ya Mapato Julai – Juni, 2020/2021**

Mhe. Spika, mwaka wa fedha 2020/2021 ulikabiliwa na mambo makubwa ambayo kwa njia moja au nyengine yaliathiri utekelezaji na Matarajio ya bajeti yaliyopangwa hapo awali kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati yakiwemo:

a) Mripuko wa *COVID-19*;
b) Matarajio ya kupokea Fedha za marejesho ya mkopo ya TZS 61 bilioni kutoka Exim Bank China kwa ajili ya mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria *(Terminal III)* ambazo hazikupatikana.

**Mapato ya Ndani**

Mhe. Spika, kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo, mapato ya ndani katika kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021 yanatarajiwa kufikia Jumla ya TZS 769.7 bilioni sawa na asilimia 73 ya Makadirio ya TZS 1,050 bilioni, ambapo utendaji umeathiriwa sana kutokana na athari za mripuko wa *Covid-19.* Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 655.2 bilioni, sawa na asilimia 71

ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar *(TRA)*, inatarajiwa kukusanya TZS 318.2 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya kukusanya TZS 383.5 bilioni, ikilinganishwa na ukusanyaji halisi wa TZS 279.4 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita 2019/20.

Kwa upande wa Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)* inatarajiwa kukusanya TZS 315.9 bilioni sawa na asilimia 61 ya makadirio ya TZS 516.7 bilioni. Ikilinganishwa na ukusanyaji halisi wa TZS 374.8 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita 2019/20. Kodi ya Mapato kutoka Serikali ya Muungano inatarajiwa kufikia TZS 21 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

Mhe. Spika, mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 114.6 bilioni sawa na asilimia 89 ya makadirio ya TZS 128.7 bilioni. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya Mawizara yanategemewa kufikia TZS 99.1 bilioni sawa na asilimia 95 ya makadirio ya TZS 104.7 bilioni. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 9.0 bilioni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya TZS 10.5 bilioni na Gawio la Benki Kuu ni TZS 6.5 bilioni sawa na asilimia 48 ya makadirio ya TZS 13.5 bilioni.

Mhe. Spika, matarajio hayo ya kukusanya jumla ya TZS 769.7 bilioni ifikapo Juni 2021 ni kutokana na mikakati iliyowekwa na Serikali ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali ni kama ifuatavyo; -

a) Kuanza rasmi matumizi ya mfumo wa utoaji wa risiti za kielektroniki ambazo hutoa taarifa juu ya mwenendo wa mauzo halisi ya mfanyabiashara ifikapo mwezi wa machi 2021 baada ya kukamilika kipindi cha majaribio;

b) Taasisi za kodi *(TRA & ZRB)* kuendelea na zoezi la ukaguzi ili kodi stahiki iweze kulipwa;

c) Kuwa na bei elekezi kwa ajili ya uthaminishaji wa bidhaa zinazoingia nchini.

**Mfuko wa Miundombinu**

Mhe. Spika, Matarajio ya mapato ya Mfuko wa Miundombinu ni kufikia TZS 32.7 bilioni sawa na asilimia 73 ya makadirio ya TZS 44.7 bilioni. Kati ya hizo, *TRA* inatarajiwa kukusanya TZS 11.1 bilioni na *ZRB* TZS 21.6 bilioni.

**Mapato kutoka Nje**

Mhe. Spika, hadi kufikia Juni mwaka 2021 matarajio ni kupokea Jumla ya TZS 310.6 bilioni, yakijumuisha Ruzuku ya TZS 44.6 bilioni na Mikopo ya TZS 266.0 bilioni.

**Jadweli namba:4 Matarajio ya Mapato kwa Mwaka 2020/2021**

| Matarajio yaMapato Julai ---Juni Mwaka2020/2021(TZS bilioni) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MAELEZO** | **Bajeti 2020/2021** | **Halisi Julai---Disemba2020** | **Matarajio 2020/2021** | **% ya Bajeti** |
| **Mapato yaNdani** | **1,050.0** | **303.3** | **769.7** | **73.3** |
| ZRB | 516.7 | 117.3 | 315.9 | 61.1 |
| TRA | 383.5 | 130.4 | 318.2 | 83.0 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 128.7 | 34.6 | 114.6 | 89.0 |
| PAYE Transfer SMT | 21 | 21 | 21 | 100.0 |
| **Mapato Mengineyo** | **529.2** | **161.3** | **368** | **69.5** |
| Marejesho ya Mkopo kutoka Exim Bank | 61 | 0 | 0 | 0.0 |
| Mkopo wa Ndani | 45 | 57 | 57.4 | 127.6 |
| Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 423.2 | 104.3 | 310.6 | 73.4 |
| **Jumla** | **1,579.2** | **464.6** | **1,137.7** | **72.0** |

*Chanzo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango*

**MATARAJIO YA MATUMIZI JULAI-JUNI, 2020/2021**

Mhe. Spika, hadi Juni 2021 matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1,137.7 bilioni sawa na asilimia 72 ya Bajeti kuu ya Serikali ya TZS 1,579.2 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 734.6 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na TZS 403.1 bilioni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa Matumizi hayo yanaonekana katika jadweli namba 5.

**Jadweli namba:5 Matarajio ya Matumizi kwa Mwaka 2020/2021**

| Matarajio ya Matunizi Julai ---Juni Mwaka 2020/2021(TZS bilioni) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MAELEZO** | **Bajeti** | **Halisi Julai---Disemba 2020** | **Matarajio Julai June** | **Asilimia ya Matarajio ya Bajeti** |

| | 2020/2021 | | 2020/2021 | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi yakawaida** | **969.3** | **353.1** | **734.6** | **75.8** |
| Mshahara wa Mawizara | 316.8 | 136.9 | 284.4 | 89.8 |
| MatumiziMengineyoMawizara | 182.6 | 43.0 | 102.4 | 56.1 |
| Matumizi Mengineyo Ruzuku | 108.2 | 23.1 | 71.8 | 66.4 |
| Mshahara Ruzuku | 123.8 | 65.5 | 132.3 | 106.9 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 237.9 | 84.6 | 143.7 | 60.4 |
| **Matumizi yamaendeleo** | **609.9** | **133.6** | **403.1** | **66.1** |
| Fedha za Serikali | 197.3 | 37.7 | 92.5 | 46.9 |
| Washirika wa Maendeleo | 412.6 | 95.9 | 310.6 | 75.3 |
| **JumlaKuu** | **1,579.2** | **486.7** | **1,137.7** | **72.0** |

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI, MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022-2023/2024

### YATOKANAYO NA MAJUKWAA YA UCHUMI NA BAJETI

Mhe. Spika, Jukwaa la Bajeti na Uchumi hufanyika kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Fedha namba 12 ya mwaka 2016 katika kifungu namba 38 kwa Serikali Kuu na kifungu namba 87 kwa Serikali za Mitaa. Vifungu hivyo vinamtaka Waziri anaehusika na Fedha aongoze jukwaa hilo na taarifa zake zitumike katika kuandaa Mwelekeo wa Bajeti ambao utapelekwa Baraza la Wawakilishi kwa majadiliano na uidhinishaji.

Mhe. Spika, Jukwaa la Uchumi na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 limefanyika tarehe 23/01/2021 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na tarehe 01/02/2021 kwa Upande wa Serikali Kuu katika Ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania, Kinazini –Zanzibar.

Mada kuu tatu 3 ziliwasilishwa ambazo ni:-

1. Mapitio na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo 2019/20-2021/22.
2. Mapitio na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali 2019/20-2021/22.
3. Mapitio na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali za Mitaa 2019/20-2021/22.

**Ifuatayo ni Michango na Ushauri iliyotolewa na kupendekezwa kutoka Majukwaa hayo**

Mhe. Spika, kutokana na changamoto kubwa Iliyojitokeza kwa wafanyakazi wa Sekta ya Afya na Elimu ambao wamegatuliwa kukosa fursa ya nafasi za mafunzo na udhamini *(scholarship)* kwa kutopangwa Bajeti hiyo kwa Serikali zote mbili imesisitizwa Serikali izingatie wafanyakazi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na sio kwa Sekta zilizogatuliwa tu.

Mhe. Spika, kuwepo mazingira magumu ya walimu pamoja na wanafunzi wa skuli za maandalizi na msingi, kutokuwepo uwiano mzuri wa walimu kwa wanafunzi sambamba na miundombinu duni ya maeneo yaliyogatuliwa.

Mhe. Spika, uzingatiaji wa mgao wa fedha kwa makundi maalumu, 4%,4%,2%, yaliyotajwa katika miongozo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itoe Muongozo na Uelewa wa upatikanaji wa Fedha hizo kwa wadau husika.

Mhe. Spika, Serikali kupitia OR-TMSMIM imetakiwa kutoa maelekezo na ufafanuzi juu ya matumizi ya mfuko wa jimbo kwa fedha za Uwakilishi kwani utaratibu uliopo sasa wa matumizi ya fedha hizo hazina maelekezo mahsusi. Imesisitizwa, Serikali kufuatilia na kusimamia Matumizi ya fedha za Mfuko wa wawakilishi na wabunge pamoja na kutoa muongozo na maelekezo ya vipaumbele vya matumizi ya fedha hizo ili ziweze kuingizwa katika mpango kazi wa Halmashauri husika wakati wa kupanga bajeti zao kwa Miradi ya Maendeleo ya wananchi yenye tija.

Mhe. Spika, kwa upande wa utekelezaji wa shughuli zilizogatuliwa ambazo fedha zake zinatokana na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi, Ilishauriwa Ushirikishwaji na kupatiwa vifungu stahiki kwa *LGA*, kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hiyo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo. Aidha vianzio vya mapato katika maeneo ya ugatuzi vikusanywe na kutumika kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambako shughuli husika zinatelekezwa.

Mhe. Spika, kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa vifaa tiba na madawa, ilishauriwa, Wizara ya Afya wafanye Mapitio juu ya usambazaji wa vifaa tiba na madawa ambavyo vinapelekwa *LGA* ili kwenda sambamba na mahitaji yaliyopo. Vilevile, ilipendekezwa Ujenzi wa ofisi/nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wilaya upewe kipaumbele.

Mhe. Spika, ilishauriwa kwamba posho na stahiki za Walimu zilipwe sambamba na vocha za Mshahara ili kuondoa malalamiko ya kila siku yanayojitokeza kwa walimu wa maandalizi na msingi sambamba na hilo maposho ya walimu wa TUTU yatafutiwe utaratibu maalumu na kuiingizwa kwenye hesabu zao binafsi. Aidha, ilisisitizwa kuwa, mitihani ya ndani ya majaribio kwa wanafunzi wa Maandalizi na Msingi ni muhimu, changamoto iliyopo fedha kwa ajili ya maandalizi ya mitihani hiyo hazitengwi katika Serikali za Mitaa hivyo, Serikali Kuu ipeleke fungu maalum kwa ajili ya kuendesha mitihani hiyo.

Mhe. Spika, imeshauriwa vitengo vinavyohusika na manunuzi viwe makini kuwachagua wakandarasi wa miradi ya ujenzi wenye uwezo wa fedha na taaluma kwa lengo la kutekeleza miradi yenye ubora na kiwango.

Mhe. Spika, imependekezwa bajeti ya mwaka 2021/2022 iongeze kodi za vileo kwa lengo la kupunguza idadi ya vitendo viovu katika jamii.

Vile vile, ilishauriwa bajeti ya ustawi wa jamii iongezwe ili iwawezeshe waratibu wa wanawake na watoto kusimamia kesi za udhalilishaji kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa deni la Taifa Serikali ilishauriwa iwe na tahadhari juu ya ongezeko la Deni hilo pamoja na kusisitizwa kukopa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo yenye tija kwa kuinua uchumi na kijamii.

Mhe. Spika, ilipendekezwa Serikali iainishe changamoto ambazo zimepatikana kwenye maeneo yaliyo athirika kutokana na Ugonjwa wa Korona na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na athari hizo.

Mhe. Spika, ilishauriwa kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya Utalii kwa kuutangaza na kuutafutia masoko. Vile vile suala la ajira kwa vijana lifanyiwe kazi ili kufikia lengo la Ilani ya CCM ya ajira laki tatu zilizoahidiwa.

Mhe. Spika, ilishauriwa kutokana na umuhimu wa Takwimu Serikali itenge asilimia ya bajeti kwa kila sekta kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa Takwimu sahihi.

Mhe. Spika, ilishauriwa kwamba ipo haja ya kutolewa muongozo wa majengo ya ofisi za serikali ili kuwe na kiwango pamoja na kupunguza gharama. Aidha, ilipendekezwa kwamba sheria za ajira kwa wageni ziangaliwe zaidi ili kuweka bayana stahiki zao.

## MWELEKEO WA UCHUMI WA DUNIA

Mhe. Spika, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.5 katika kipindi cha mwaka 2021. Ukuaji wa uchumi wa Afrika unatagemewa kufikia wastani wa asilimia 3.0 katika kipindi kama hicho, huku Uchumi wa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki kufikia wastani wa asilimia 4.5 kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Fedha la Dunia.

**Uchumi wa Dunia 5.5%**

| Ukuaji mzuri | | Ukuaji mbaya | |
|---|---|---|---|
| India | 11.5 | Nigeria | 1.5 |
| China | 8.1 | Poland | 2.7 |
| Malaysia | 7.0 | Saudi Arabia | 2.6 |

**Uchumi wa Afrika 3%**

| Ukuaji mzuri | | Ukuaji mbaya | |
|---|---|---|---|
| Botswana | 8.71 | South Sudan | -2.27 |
| Niger | 6.91 | Congo | -0.82 |
| Guinea | 6.64 | Ethiopia | -0.02 |

**Uchumi wa nchi za SADC 3.33%**

| Ukuaji mzuri | | Ukuaji mbaya | |
|---|---|---|---|
| Mauritius | 9.9 | Mozambique | 2.1 |
| Zimbabwe | 4.16 | Malawi | 2.5 |
| Madagascar | 3.16 | Zambia | 0.6 |

**Uchumi wa Afrika Mashariki**

| | |
|---|---|
| Rwanda | 6.32 |
| Uganda | 4.93 |
| Kenya | 4.67 |
| Tanzania | 3.6 |
| Burundi | 3.13 |

*Chanzo: Shirika la Fedha la Dunia*

**Mwelekeo wa Hali ya Uchumi Zanzibar**

Mhe. Spika, mwelekeo wa uchumi kwa mwaka 2021 unategemea kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050, Mkakati wa Maendeleo wa Muda wa Kati pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025. Kwa mwaka 2021 jambo kuu na la msingi litakuwa ni kuimarisha sekta za kiuchumi na kijamii ambazo zimeathiriwa na *COVID-19*, sambamba na kuendeleza hatua za kujenga uchumi imara na mpana zaidi *(diversified).* Vile vile kuyafanyia kazi maeneo ya msingi ya ukuwaji wa uchumi yakiwemo Uchumi wa Buluu na Viwanda vidogo

vidogo. Aidha, huduma za msingi za jamii kama vile afya na elimu zitapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, Pato halisi la taifa kwa mwaka 2021 linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 5 kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa uwekezaji, kuimarisha sekta ya Viwanda pamoja na Uchumi wa Buluu.

Matarajio ya ukuaji wa uchumi yatatokana na kuendelea kuyafanyia kazi mambo yafuatayo; -

i. Kuendelea kuhuisha sekta za kiuchumi na kijamii baada ya mtikisiko wa uchumi kutokana na *COVID-19*.
ii. Kuimarisha sekta ndogo ya usafirishaji, Serikali pamoja na watu binafsi wanatarajiwa kuongeza meli za mizigo pamoja na abiria.
iii. Kuendelea na juhudi za kuongeza uzalishaji wa vifaranga, utoaji vifaranga kwa wafugaji wadogo wadogo na kuendeleza ufugaji wa samaki.
iv. Kuendelea na uvuvi wa bahari kuu pamoja na kuongeza boti zitakazofanya shughuli zake katika bahari kuu.
v. Kuimarisha vituo vya utafiti vilivyopo nchini (Vituo vya utafiti wa uvuvi, kilimo, mifugo na afya).
vi. Kuendelea kuwawezesha watafiti na wavumbuzi kwa kuwapatia elimu na vitendea kazi.
vii. Kuongezaka kwa usafirishaji wa zao la karafuu kwa matarajio ya mwaka 2021 kuongezeka kwa uzalishaji wa zao hilo na kuongeza usarifu na usafirishaji wa zao la mwani.
viii. Kuongezeka kwa uhamasishaji wa uwekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kutekelezwa miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya *PPP*.
ix. Kuweka mazingira bora na rafiki ya kibiashara.

**SHABAHA NA MALENGO YA UCHUMI KWA 2021-2023**

Shabaha na malengo ya uchumi kwa kipindi cha miaka mitatu ni kama yatategemewa kuwepo na misingi ifuatayo:-

a. Kuwepo kwa Amani na Utulivu;

b. Uwajibikaji katika kazi;
c. Kuendeleza kuwajengea uwezo wafanyakazi;
d. Kuimarisha Utawala Bora na.
e. Kuondoa Ubadhirifu wa Mali za Umma, Wizi, Rushwa pamoja na Uzembe.

**Shabaha za Kiuchumi**

a. Kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa inategemewa kuwa baina ya asilimia 5 hadi 7.1.
b. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kuwa wastani wa chini ya asilimia 5.
c. Mapato ya ndani kwa kipindi cha miaka mitatu yanakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 25.4 ya Pato la Taifa kwa miaka 2020/21-2022/23 kutoka asilimia 24.4 kwa mwaka 2019/20.
d. Kwa kipindi cha miaka mitatu nakisi ya bajeti kwa Pato la Taifa inakadiriwa kuwa chini ya asilimia 3 ifikapo mwaka 2023 hii ni kutokana na kigezo kilichowekwa na Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki na *SADC* kuzitaka nchi wanachama nakisi zao za Bajeti kutovuka zaidi ya asilimia 3 ya Pato la Taifa.

**MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO 2021/2022-2023/2024**

Mhe. Spika, Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 utazingatia malengo na mikakati inayotokana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Dira hiyo ina lengo la kuifikisha Zanzibar katika Kiwango cha Juu cha Uchumi wa Kati kupitia mihimili mikuu minne ambayo ni:-

(i) Mageuzi ya kiuchumi;
(ii) Maendeleo ya rasilimali watu na huduma za kijamii;
(iii) Kuimarisha miundombinu; na
(iv) Utawala bora na uhimili.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha malengo ya Dira hiyo yanafikiwa, Serikali imeanza kutafsiri malengo hayo na inaendelea na uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati 2021-2025. Mbali na Dira ya 2050, nyaraka nyengine zilizozingatiwa ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020- 2025, Hotuba ya ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi, Maelekezo ya Serikali Kiujumla pamoja na ahadi mbali mbali zilizotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wakati wa kampeni ya Uchaguzi na Hotuba yake katika ziara za makundi mbali mbali. Katika utekelezaji huo, maeneo yaliyopewa

kipaumbele yatatekeleza miradi inayojikita zaidi katika kuimarisha hali za wananchi, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali.

## VIPAUMBELE VYA KITAIFA KWA MWAKA 2021/2022 -2023/2024

Mhe. Spika, **v**ipaumbele vya mwaka 2021/2022-2023/2024 ni kama ifuatavyo:-

### Kuimarisha Miundombinu

a) Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani unaojumuisha bandari ya mafuta na gesi, makontena, uvuvi, chelezo, eneo la maghala na mji wa kisasa;
b) Ujenzi wa Uwanja wa ndege Pemba; na
c) Kuanza kwa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Mpiga Duri
d) Ujenzi wa daraja la Unguja Ukuu - Uzi;
e) Kuendelea na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 135 Unguja na Pemba;
f) Kuendeleza maeneo ya uwekezaji *(Industrials Parks)* Chamanangwe, Dunga na Nungwi;
g) Kuimarisha bandari ya Malindi, Mkoani na kuanza Ujenzi mpya wa eneo la Mkumbuu;
h) Kuongeza uzalishaji wa umeme kwa njia ya jua na gesi na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji;

### Kuimarisha Sekta Kuu za Uchumi

i) Kuimarisha uchumi buluu ikiwemo viwanda vidogo vidogo na vya kati vikiwemo vya usarifu wa Mwani, Chumvi na Samaki; Kuendeleza shughuli za uvuvi wa bahari kuu na ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki; Kuendelea na shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia;
j) Kuimarisha utalii kwa wote;
k) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji;
l) Ujenzi wa machinjio ya mifugo;

e) Kuchukua hatua maalum za kusaidia zao la karafuu;
f) Kuendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana;
g) Kuimarisha mfumo wa udhibiti wa biashara kwa kuweka chombo kimoja cha kodi;
h) Kuendeleza tafiti na Ubunifu.

3. Kuimarisha Huduma za Kijamii

a) Ujenzi wa Hospitali Mpya ya rufaa ya Binguni;
b) Ujenzi wa hospitali ya Wete kwa kuipandisha hadhi ya Mkoa;
c) Kuendeleza ujenzi wa miji ya kisasa;
d) Kuimarisha mazingira ya uendelezaji wa Miji midogo midogo *(Satellite cities)* ikiwemo Nungwi, Tunguu na miji ya Pemba;
e) Kuimarisha upatikanaji wa elimu bora kwa wote kwa ujenzi wa skuli mpya za ghorofa, dakhalia, maktaba, maabara na upatikanaji wa vifaa vya kisasa;
f) Kuimarisha Vituo vya Amali kwa ajili ya kusaidia uchumi wa buluu na wahitimu kuweza kujiajiri wenyewe;
g) Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini kwa uchimbaji na uendelezaji wa visima;
h) Ujenzi wa viwanja vya michezo na sherehe;
i) Kuanzisha Mfumo wa Bima ya Afya.

**Kuendeleza Rasilimali Watu na Fedha**

a. Kuendeleza taaluma katika fani mbali mbali ikiwemo mafuta na gesi, uhandisi, huduma za ugani, udaktari na taaluma za sayansi;
b. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kidijitali ya utendaji kazi kwa ujumla, ukusanyaji mapato, usimamizi wa matumizi na manunuzi na utunzaji wa kumbukumbu za usajili wa mali za umma.

**Kuimarisha Utawala Bora**

c. Kuanza Ujenzi wa Skuli ya sheria na Utafiti;
d. Kuanza Ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar *(ZAECA)*
e. Kuendeleza miji salama kwa uwekaji wa vifaa vya ulinzi na usalama;
f. Kuendelea na Ujenzi wa Ofisi za Serikali;
g. Kuendelea na juhudi za uhifadhi wa Mji Mkongwe na Mambo ya Kale;

f. Kuendelea na ujenzi wa nyumba za viongozi wakuu wa Serikali;
g. Kuimarisha Usimamizi wa Fedha za Umma.
6. Kuimarisha Sekta Mtambuka
a. Kukabiliana na athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi;
b. Kupambana na vitendo vya Udhalilishaji.

**Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

a) Kuanza utekelezaji wa miradi ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ikiwemo: -
i. Ujenzi na uwendeshaji wa masoko sita (Mwanakwerekwe, Chuini, Mombasa, Machomane, Mkokotoni na Jumbi);
ii. Ujenzi wa vituo vya daladala Kijangwani, Chuini na Chanjaani;
iii. Ujenzi wa Kituo cha Biashara na Mikutano ya Kimataifa Nyamanzi *(Nyamanzi Convention Centre);*
iv. Ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA*
v. Ujenzi wa nyumba za makaazi ya wananchi *(Real estate);*
vi. Ujenzi wa viwanda mbali mbali.

**VIPAUMBELE VYA KITAIFA KWA MWAKA 2021/2022**

**Vipaumbele kwa mwaka 2021/2022 ni kama ifuatavyo: -**

1. Kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba;
2. Kuanza ujenzi wa barabara ya Chake Chake – Wete *(km 22.1);*
3. Kuendelea na matayarisho na ujenzi wa bandari ya Mangapwani, Mpigaduri na Mkoani;
4. Kuanza ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki;
5. Kuendelea na Ujenzi wa Hospitali Mpya ya rufaa ya Binguni;
6. Kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wete;
7. Kuendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana;
8. Kuendeleza viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa Mwani, chumvi na samaki;
9. Kuendeleza miji salama kwa uwekaji wa vifaa vya ulinzi na usalama;
10. Kuanza ujenzi wa Ofisi za Serikali zikiwemo
    i. Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango Unguja,
    ii. Ofisi za Serikali – Dodoma ;
    iii. Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali
    iv Mahanga na Ofisi za Idara Maalum za SMZ na
    v Kuandaa Mpango wa kuwepo kwa eneo maalum la mji wa Serikali;
11. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji;

12. Kuanza utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar *(Boost Inclusive Growth in Zanzibar- Big Z);*
13. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Nishati *(Zanzibar Energy Sector Transformation -ZEST);*
14. Kuanza uzalishaji wa umeme wa jua na gesi;
15. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kidijitali ya utendaji kazi kwa ujumla, ukusanyaji mapato, usimamizi wa matumizi na manunuzi na utunzaji wa kumbukumbu za usajili wa mali za umma;
16. Kuendelea kutoa huduma za maji safi na salama kwa wananchi na
17. Kuimarisha Tafiti na Ubunifu.

## MWELEKEO WA MAPATO

Mhe. Spika, kwa kuzingatia hali ya Bajeti kwa mwaka 2021/2022, Mapato ya Serikali yanatarajiwa kufikia Jumla ya TZS 1,506.2 bilioni kati ya fedha hizo jumla ya TZS 1,105.5 bilioni zimekadiriwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani, TZS 50.0 bilioni zinatokana na mkopo wa ndani, Mapato kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa vianzio vya ndani TZS 16.2 bilioni na TZS 334.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwemo mkopo wa TZS 307.9 bilioni na ruzuku ya TZS 26.6 bilioni.

### Muhtasari wa Mwelekeo wa Mapato

Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitatu ijayo, Serikali inatarajia kukusanya Jumla ya TZS 1,506.2 bilioni. kwa mwaka wa fedha 2021/22, TZS 1,791.0 bilioni, kwa mwaka 2022/23 na jumla ya TZS 1,948.2 bilioni kwa mwaka 2023/24.

Jadweli namba 6: Makisio ya Mapato kwa Mwaka 2021/22-2023/24

**Makisio ya Mapato ---2021/22---2023/24(TZS bilioni)**

| MAELEZO | Mwaka 2021/2022 | Mwaka 2022/202 | Mwaka 2023/2024 |
|---|---|---|---|
| **MAPATO** | | | |
| Mapato ya Ndani | **1,105.5** | 1,286 .2 | 1,422 .0 |
| 4.5% Msaada wa Kibajeti | **100T** | **100T** | **100T** |
| Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Vianzio vya ndani | **16.2** | **16.5** | **16.9** |
| Mkopo wa Ndani | **50.0** | 50 .0 | 40 .0 |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili | **2.0** | 2 .0 | 4 .0 |
| Mikopo na Ruzuku | **332.5** | 436 .3 | 465 .3 |
| **Jumla ya Mapato** | **1,506.2** | **1,791.0** | **1,948.2** |

*Chanzo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango*

## MWELEKEO WA MATUMIZI

Mhe. Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo, Serikali inatarajia kutumia jumla ya TZS 1,506.2 bilioni kwa mwaka wa fedha 2021/22 yakiwemo Matumizi ya kazi za Kawaida ya jumla TZS 959.3 bilioni, Matumizi ya kazi za Maendeleo ya TZS 546.9 Aidha, Serikali imekadiria kutumia jumla ya TZS 1,791.0 bilioni, kwa mwaka 2022/23 na TZS 1,948.2 bilioni kwa mwaka 2023/24.

**Jadweli namba : 7 Makisio ya Matumizi kwa Mwaka 2021/22-2023/24**

| Makisio yaMatumizi 2021/22---2023/24(TZS bilioni) | | | |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **Mwaka 2021/2022** | **2022/2023** | **Mwaka 2023/2024** |
| **Matumizi ya Kawaida** | **959.3** | **1,107 .5** | **1,431.5** |
| Mshahara Mawizara | 380.9 | 483 .8 | 667 .3 |
| Mshahara Ruzuku | 130.0 | 132 .6 | 134 .9 |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 139 .8 | 158 .6 | 250 .9 |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 111.3 | 133 .5 | 154 .7 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 181.1 | 182 .5 | 206 .8 |
| Matumizi ya Mamlaka za serikali za Mitaa kutoka vianzio vyao | 16 .2 | 16 .5 | 16 .9 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **546.9** | **683 .5** | **516 .7** |
| Fedha za Serikali | 212.5 | 245 .2 | 265 .4 |
| Mikopo na Ruzuku Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 334.4 | 438 .3 | **251 .3** |
| **Jumla Kuu** | **1,506.2** | **1,791 .0** | **1,948.2** |

*Chanzo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango*

**SURA YA BAJETI**

Mhe. Spika, kwa mwaka 2021/2022 mapato ya ndani pamoja na ruzuku na mikopo yanatarajiwa kufikia TZS 1,506.2 bilioni kwa mchanganuo ufuatao;

| | **TZS 'bilioni'** |
|---|---|
| Mapato ya Ndani | 1,105.5 |
| Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Vianzio vya ndani | 16.2 |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili yaan *(General Budget Support)* | 2.0 |
| Mkopo wa Ndani | 50.0 |
| Mikopo na Ruzuku | 332.5 |
| **Jumla ya Mapato** | **1,506.2** |

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi, jumla ya TZS 1,506.2 bilioni zinatarajiwa kutumika zikiwemo TZS 559.3 bilioni kwa matumizi ya kawaida, ikijumuisha Mishahara ya Mafungu TZS 380.9 bilioni na Mishahara ya Ruzuku TZS 130.0 bilioni na Matumizi ya Kawaida kwa Mawizara TZS 139.8 bilioni Matumizi Mengineyo ya Ruzuku TZS 111.3 bilioni na Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 197.3 bilioni. Kwa upande wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo jumla ya TZS 546.9 bilioni, ikihusisha

TZS 212.5 bilioni fedha za Serikali na TZS 334.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mchanganuo wa Matumizi hayo ni kama ifuatavyo:-

| | **TZS 'bilioni'** |
|---|---|
| Mtumizi ya Kazi za Kawaida | 959.3 |
| Mshahara Mafungu | 380.9 |
| OC Mafungu | 337.1 |
| Mshahara Ruzuku | 130 |
| OC Ruzuku | 111.3 |
| Matumizi ya Kazi za Maendeleo | 546.9 |
| SMZ | 212.5 |
| Ruzuku kutoka washirika wa Maendeleo | 26.5 |
| Mkopo kutoka washirika wa Maendeleo | 307.9 |
| **Jumla** | **1,506.2** |

**VIGEZO VYA UGAWAJI WA RASILIMALI FEDHA**

Mhe. Spika, Ugawaji wa Rasilimali Fedha kwa mwaka 2021/22-2023/24 umezingatia mambo makuu yafuatayo:

i. Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025;

ii. Maeneo ya Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo;

iii. Maagizo Maalum ya Serikali kwa mujibu wa vipaumbele vya Taifa;

iv. Programu na Miradi ya kimkakati *(Flagship Projects)* ya kitaifa, miradi yote ambayo Serikali ina dhima *(Commitments)* kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Miradi yote iliyokuwa haijakamilika utekelezaji wa shughuli zake kwa bajeti ya mwaka 2020/21.

**VIAMBATISHO**

Mhe. Spika, Pamoja na mapendekezo haya, tunaambatanisha viambatisho vifuatavyo:-

1. Kiambatisho nambari:1 Makadirio ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2021/2022-2023/2024.

2. Kiambatisho nambari:2 Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele kwa Kipindi cha Julai – Disemba 2020
3. Kiambatisho nambari:3 Utekelezaji wa Matumizi wa Miradi ya

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza naomba kuchukua nafasi hii tena kumshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kuwaunganisha Wazanzibari wote.

Pili, kwa maelekezo yake na miongozo yake ya kimapinduzi ambayo yamekuwa akiyatoa kwetu katika kufikia dira na malengo y taifa letu, vyote hivi kwa pamoja vimeanza kutoa mwanga wa matumaini katika uongozi wake.

Mhe. Spika, kuna msemo wa Kiingereza naomba niunukuu:

*“If you are not willing to risk the unsually you have to settle for ordinary”*

Mhe. Rais amekuwa dira nzuri kwetu pia naomba kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano makubwa na miongozo mliyotupa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango lakini vile vile nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati nzima ya Bajeti. *(Makofi)*

Pili, nitumie nafasi hii kipekee kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na kamati nzima ya bajeti kwa mashirikiano makubwa waliyotupa katika kufanikisha uwaandaji wa taarifa hii.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima kubwa sasa niliombe baraza lako liidhinishe na hatimaye ikubaliane na mapendekezo ya mwelekeo wa Makadirio ya Bajeti TZS 1,506.2 bilioni na Kuiruhusu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutayarisha na kuwasilisha Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022-2023/2024.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Kiambatisho Nambari :2**

**UPATIKANAJI WA FEDHA KWA PROGRAMU NA MIRADI 2020/2021, (TZS MILIONI)**

| Wizara/Taasisi | Fedha Zilizopangwa | | | Jumla | | | Asilimia | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU/MRADI** | **SMZ** | **WM** | **JUMLA** | **SMZ** | **WM** | **JUMLA** | **SMZ** | **WM** | **JUMLA** |
| **OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI** | | | | | | | | | |
| Uimarishaji Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali | 1,500 | | 1,500 | 1,250 | | 1,250 | 83 | | 83 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,500** | | **1,500** | **1,250** | | **1,250** | **83** | | **83** |
| **OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS** | | | | | | | | | |
| Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) | 50 | 21,548 | 21,598 | | 469 | 469 | 0 | 2 | 2 |
| Kujenga Uwezo wa Kukabiliana na Maafa | | 186 | 186 | | 39 | 39 | | 21 | 21 |
| Kuimarisha Usimamizi wa Mazingira, Maliasili na Mabadiliko ya Tabianchi-Zanzibar | 300 | 290 | 590 | | | | 0 | 0 | 0 |
| Kukuza Uwezo wa Kitaifa wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (ADB-ACCF) | | 676 | 676 | | 62 | 62 | | 9 | 9 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **350** | **22,700** | **23,050** | | **570** | **570** | **0** | **3** | **2** |
| **TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia | 1,900 | | 1,900 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,900** | | **1,900** | | | | **0** | | **0** |
| **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar | 19,500 | | 19,500 | 2,287 | | 2,287 | 12 | | 12 |
| Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG - Z) | | 19,964 | 19,964 | | 34,973 | 34,973 | | 175 | 175 |
| Programu ya Ujenzi wa Miji Mipya | 20,000 | | 20,000 | | | | 0 | | 0 |
| Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP) | | 1,639 | 1,639 | | 511 | 511 | | 31 | 31 |
| Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili | 100 | 4,541 | 4,641 | | 314 | 314 | 0 | 7 | 7 |
| Mradi wa Kujenga Uwezo Taasisi za Serikali | 20 | 107 | 127 | | 240 | 240 | 0 | 225 | 189 |
| Uimarishaji wa Maeneo Huru Micheweni Pemba | 1,800 | | 1,800 | | | | 0 | | 0 |
| Mtandao wa Uingizaji wa Taarifa za Bajeti | 500 | | 500 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **41,920** | **26,251** | **68,171** | **2,287** | **36,038** | **38,324** | **5** | **137** | **56** |
| **TUME YA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) | 550 | 100 | 650 | | | | 0 | 0 | 0 |
| Mpango wa Kuhuisha Uchumi (ERP) | 7,000 | | 7,000 | | | | 0 | | 0 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kupunguza Umasikini na Ufuatiliaji wa SDGs | 150 | | 150 | 219 | | 219 | 146 | | 146 |
| Uratibu na Usimamizi wa Malengo na Maendeleo Endelevu (SDGs) na MKUZA III | 100 | 801 | 901 | | 359 | 359 | 0 | 45 | 40 |
| Kuoanisha Masuala ya Idadi ya Watu katika Afya ya Uzazi, Jinsia na Kupunguza Umasikini | | 286 | 286 | | 180 | 180 | | 63 | 63 |
| Uendelezaji wa Takwimu Zanzibar (ZSDP) | | 3,322 | 3,322 | | 697 | 697 | | 21 | 21 |
| Kuendeleza Tafiti na Ubunifu | 500 | | 500 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **8,300** | **4,509** | **12,809** | **219** | **1,236** | **1,455** | **3** | **27** | **11** |
| **WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI** | | | | | | | | | |
| Programu ya Umwagiliaji | 19,900 | 47,193 | 67,093 | | 11,782 | 11,782 | 0 | 25 | 18 |
| Programu ya Kusaidia Kilimo na Uhakika wa Chakula (ERPP) | | 2,211 | 2,211 | | 1,081 | 1,081 | | 49 | 49 |
| Uimarishaji Uvuvi wa Bahari Kuu | 2,000 | 12,152 | 14,152 | | | | 0 | 0 | 0 |
| Kuimarisha Ufugaji wa Mazao ya Baharini | | 736 | 736 | | | | | 0 | 0 |
| Mradi wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Mashariki mwa Bahari ya Hindi (SWIOFISH) | | 8,651 | 8,651 | | 2,888 | 2,888 | | 33 | 33 |
| Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi | | 2,141 | 2,141 | | | | | 0 | 0 |
| Kuendeleza Utafiti wa Mifugo | 1,000 | | 1,000 | | | | 0 | | 0 |
| Mradi wa Kudhibiti Nzi wa Matunda | 100 | 120 | 220 | | | | 0 | 0 | 0 |
| Kudhibiti Sumu Kuvu inayotokana na | | | | | | | | 0 | 0 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ulaji wa<br>Mahindi na Njugu | | 932 | 932 | | | | | | |
| Uhifadhi wa Misitu kwa Faida za Kiuchumi | | 3,801 | 3,801 | | | | | 0 | 0 |
| Kilimo cha Kushajihisha Ukulima wa Mboga Mboga<br>na Matunda | | 5,603 | 5,603 | | | | | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **23,000** | **83,541** | **106,541** | | **15,752** | **15,752** | **0** | **19** | **15** |
| **WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA** | | | | | | | | | |
| Programu ya Mazingira Bora ya Biashara | 300 | | 300 | | | | 0 | | 0 |
| Uimarishaji wa Maeneo ya Viwanda (Indurstrial Park | 1,000 | | 1,000 | 396 | | 396 | 40 | | 40 |
| Kuimarisha viwanda vidogo vidogo na vya kati (SMIDA) | 1,000 | | 1,000 | 25 | | 25 | 3 | | 3 |
| Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo,Wakati na Wakubwa | 4,500 | 4,600 | 9,100 | | | | 0 | 0 | 0 |
| Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar | 3,000 | | 3,000 | | | | 0 | | 0 |
| Mfumo mpya wa Utoaji Leseni kwa Maendeleo ya<br><br>Sekta Binafsi | 400 | | 400 | 200 | | 200 | 50 | | 50 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **10,200** | **4,600** | **14,800** | **621** | | **621** | **6** | **0** | **4** |
| **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | | | | |
| Programu ya Kuimarisha Miundombnu ya Elimu | 1,000 | | 1,000 | | | | 0 | | 0 |
| Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi | | 3,253 | 3,253 | | 1,723 | 1,723 | | 53 | 53 |
| Uimarishaji wa Elimu ya Msingi | | 402 | 402 | | 18 | 18 | | 4 | 4 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uimarishaji wa Elimu ya Lazima | 3,500 | 11,307 | 14,807 | 350 | 8,369 | 8,719 | 10 | 74 | 59 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,500** | **14,962** | **19,462** | **350** | **10,111** | **10,461** | **8** | **68** | **54** |
| **WIZARA YA AFYA** | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | |
| Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar | 248 | 5,586 | 5,834 | 40 | 1,431 | 1,471 | 16 | 26 | 25 |
| Kuipandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja | 1,500 | | 1,500 | 5 | | 5 | 0 | | 0 |
| Kuzipandisha hadhi Hospitali za Wilaya na hospitali za Vijiji | 5,000 | | 5,000 | 615 | | 615 | 12 | | 12 |
| Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Hospital ya Rufaa Binguni | 6,000 | | 6,000 | 1,402 | | 1,402 | 23 | | 23 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa-Pemba | 2,000 | | 2,000 | 107 | | 107 | 5 | | 5 |
| Ujenzi wa Maabara ya Mamlaka ya Dawa na Vipodozi | 2,100 | | 2,100 | | | | 0 | | 0 |
| Ujenzi wa Hospital ya Wagonjwa wa Akili | 1,400 | 1,400 | 2,800 | 14 | | 14 | 1 | 0 | 1 |
| Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Afya | 2,000 | | 2,000 | 160 | | 160 | 8 | | 8 |
| Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto | 500 | 9,574 | 10,074 | | 523 | 523 | 0 | 5 | 5 |
| Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma | 248 | 5,090 | 5,338 | | 1,416 | 1,416 | 0 | 28 | 27 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **20,996** | **21,651** | **42,647** | **2,343** | **3,370** | **5,713** | **11** | **16** | **13** |
| **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | 466 | 67,129 | 67,596 | | 12,792 | 12,792 | 0 | 19 | 19 |
| Kuendeleza Visima vya Ras el Khaimah | 4,000 | | 4,000 | 438 | | 438 | 11 | | 11 |
| Usambazaji Umeme Vijijini | 500 | | 500 | | | | 0 | | 0 |
| Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZEST) | | 17,850 | 17,850 | | | | | 0 | 0 |
| Kujenga Uwezo na Matengenezo ya Miundombinu ya Umeme Zanzibar | | 3,500 | 3,500 | | | | | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,966** | **88,479** | **93,446** | **438** | **12,792** | **13,231** | **9** | **14** | **14** |
| **WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI** | | | | | | | | | |
| Ujenzi wa barabara za Kizimbani-Kiboje (km7.2) na | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumbi-Koani (km 6.3) | 2,000 | | 2,000 | | | | 0 | | 0 |
| Ujenzi wa barabara ya Chake-Wete | 8,000 | 8,990 | 16,990 | | | | 0 | 0 | 0 |
| Ujenzi wa Barabara za Bububu-Mahonda - Mkokotoni (31 km), Mkwajuni-Kijini (9.4 km), Pale Kiongele - Mkwajuni (4.6 km), Matemwe - Muyuni (7.6 km), Fuoni - Kombeni (km 8.6) na Bububu Polisi - Chuini (km3) | 1,500 | 8,334 | 9,834 | | 19,182 | 19,182 | 0 | 230 | 195 |
| Ujenzi wa Barabara ya Jozani-Charawe-Ukongoroni (km 23) | 2,000 | | 2,000 | 353 | | 353 | 18 | | 18 |
| Ujenzi wa Barabara ya Kitogani - Paje, Mahonda - Donge - Mkokotoni, Kinyasini - Kiwengwa na Dunga - Chwaka | 2,000 | | 2,000 | | | | 0 | | 0 |
| Ujenzi wa Barabara ya Unguja Ukuu - Uzi Ng'ambwa | 5,000 | | 5,000 | | | | 0 | | 0 |
| Ujenzi wa Barabara ya Fumba - Kisauni (12 km) | 1,000 | | 1,000 | | | | 0 | | 0 |
| Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria Zanzibar | 5,500 | 124,586 | 130,086 | 16,931 | 2,449 | 19,380 | 308 | 2 | 15 |
| Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 1,000 | | 1,000 | | | | 0 | | 0 |
| Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri | 5,000 | | 5,000 | 1,080 | | 1,080 | 22 | | 22 |
| Ununuzi wa Land Craft | 2,500 | | 2,500 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **35,500** | **141,910** | **177,410** | **18,364** | **21,631** | **39,995** | **52** | **15** | **23** |
| **WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE, WANAWAKE NA WATOTO** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usawa wa Kijinsia na Kuwawezesha Wanawake | | 180 | 180 | | | | | 0 | 0 |
| Mradi wa Jinsia | | 471 | 471 | | 155 | 155 | | 33 | 33 |
| Mradi wa Hifadhi ya wazee | 1,100 | | 1,100 | | | | 0 | | 0 |
| Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kulea na Kutotolea Wajasiriamali (Incubator) | 1,000 | | 1,000 | 140 | | 140 | 14 | | 14 |
| Mradi wa Hifadhi ya Jamii | | 121 | 121 | | 11 | 11 | | 9 | 9 |
| Mradi wa Hifadhi ya Watoto | | 388 | 388 | | 58 | 58 | | 15 | 15 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,100** | **1,159** | **3,259** | **140** | **224** | **364** | **7** | **19** | **11** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 1,500 | | 1,500 | 22 | | 22 | 1 | | 1 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,500** | | **1,500** | **22** | | **22** | **1** | | **1** |
| **MKURUGENZI WA MASHTAKA** | | | | | | | | | |
| Ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti | 600 | | 600 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **600** | | **600** | | | | **0** | | **0** |
| **OFISI YA RAIS - UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** | | | | | | | | | |
| Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma - II | 400 | | 400 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **400** | | **400** | | | | **0** | | **0** |
| **MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI** | | | | | | | | | |
| Ujenzi wa Ofisi ya ZAECA | 1,000 | | 1,000 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,000** | | **1,000** | | | | **0** | | **0** |
| **WIZARA YA HABARI, UTALII NA MAMBO YA KALE** | | | | | | | | | |
| Programu Mjumuisho ya Kuendeleza Utalii | 2,700 | | 2,700 | 443 | | 443 | 16 | | 16 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Jengo la Ofisi na Studio za Redio Mkanjuni-Pemba | 1,400 | | 1,400 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,100** | | **4,100** | **443** | | **443** | **11** | | **11** |
| **KAMISHENI YA UTALII** | | | | | | | | | |
| Kuimarisha Utalii kwa Wote | 2,000 | | 2,000 | 362 | | 362 | 18 | | 18 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,000** | | **2,000** | **362** | | **362** | **18** | | **18** |
| **WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** | | | | | | | | | |
| Programu ya Ajira kwa Vijana | 2,000 | | 2,000 | 1,000 | | 1,000 | 50 | | 50 |
| Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya | 2,500 | | 2,500 | 643 | | 643 | 26 | | 26 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,500** | | **4,500** | **1,643** | | **1,643** | **37** | | **37** |
| **OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | | | | |
| Programu ya Ugatuzi wa Masuala ya Elimu | 1,000 | 2,896 | 3,896 | 350 | | 350 | 35 | 0 | 9 |
| Uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi | 8,000 | | 8,000 | 5,525 | | 5,525 | 69 | | 69 |
| Ujenzi wa Kiwanda cha Ushoni (ZQTL) | 2,500 | | 2,500 | 610 | | 610 | 24 | | 24 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **11,500** | **2,896** | **14,396** | **6,484** | | **6,484** | **56** | **0** | **45** |
| **WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Vizazi na Vifo | 1,000 | | 1,000 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,000** | | **1,000** | | | | **0** | | **0** |
| **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)** | | | | | | | | | |
| Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi | 4,800 | | 4,800 | 584 | | 584 | 12 | | 12 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM | 700 | | 700 | 350 | | 350 | 50 | | 50 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **5,500** | | **5,500** | **934** | | **934** | **17** | | **17** |
| **KIKOSI CHA VALANTIA** | | | | | | | | | |
| Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari | 1,500 | | 1,500 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,500** | | **1,500** | | | | **0** | | **0** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **CHUO CHA MAFUNZO** | | | | | | | | | |
| Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga | 1,500 | | 1,500 | 250 | | 250 | 17 | | 17 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,500** | | **1,500** | **250** | | **250** | **17** | | **17** |
| **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | | | | | | | |
| Ujenzi wa Skuli ya Sekondari na Ufundi - Mtoni | 2,500 | | 2,500 | 619 | | 619 | 25 | | 25 |
| Ujenzi wa Majengo ya Kambi za JKU Pemba | 2,000 | | 2,000 | 545 | | 545 | 27 | | 27 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,500** | | **4,500** | **1,164** | | **1,164** | **26** | | **26** |
| **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | | | | | | | |
| Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari | 2,500 | | 2,500 | | | | 0 | | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,500** | | **2,500** | | | | **0** | | **0** |
| **JUMLA KUBWA** | **197,332** | **412,659** | **609,991** | **37,315** | **101,747** | **139,061** | **19** | **25** | **23** |

**Kiambatisho Nambari :3**

**UPATIKANAJI WA FEDHA MFUKO WA MIUNDOMBINU, 2020/2021 (TZS MILIONI)**

| JINA LA PROGRAMU/MRADI | Kilichopangwa | Kilichopatikana | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI** | | | |
| Uimarishaji Uvuvi wa Bahari Kuu | 2,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,000** | **0** | **0** |
| **WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA** | | | |
| Kuimarisha Taasisi ya Viwango Zanzibar | 3,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **3,000** | **0** | **0** |
| **WIZARA YA AFYA** | | | |
| Ujenzi wa Hospital ya Rufaa Binguni (Awamu ya Kwanza) | 6,000 | 1,402 | 23 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **6,000** | **1,402** | **23** |
| **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA, MAJI NA NISHATI** | | | |
| Kuendeleza Visima vya Ras el Khaimah | 2,000 | 438 | 22 |
| Usambazaji Umeme Vijijini | 500 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,500** | **438** | **18** |
| **WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI** | | | |
| Ujenzi wa Daraja la Uzi-Ng'ambwa | 5,000 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Land Craft | 2,400 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **7,400** | **0** | **0** |
| **MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI** | | | |
| Ujenzi wa Ofisi ya ZAECA | 1,000 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,000** | **0** | **0** |
| **KAMISHENI YA UTALII** | | | |
| Kuimarisha Utalii kwa Wote | 2,000 | 362 | 18 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,000** | **362** | **18** |
| **WIZARA YA VIJANA, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** | | | |
| Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya | 2,500 | 643 | 26 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,500** | **643** | **26** |
| **OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | |
| Uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi | 8,000 | 5,525 | 69 |
| Ujenzi wa Kiwanda cha Ushoni (ZQTL) | 1,400 | 610 | 44 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA YA FUNGU** | **9,400** | **6,134** | **65** |
| **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | |
| Ujenzi wa Skuli ya Sekondari na Ufundi - Mtoni | 2,000 | 619 | 31 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,000** | **619** | **31** |
| **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)** | | | |
| Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi | 4,800 | 584 | 12 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,800** | **584** | **12** |
| **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | |
| Ununuzi wa Vifaa vya Zimamoto | 1,600 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,600** | **0** | **0** |
| **JUMLA KUBWA** | **44,200** | **10,183** | **23** |

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa sasa kwa heshima na taadhima naomba nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili na yeye aje awasilishe taarifa ya kamati. Karibu sana mheshimiwa.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum (Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti):** Mhe. Spika, nakushukuru sana. Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai na uzima na kutuwezesha kukutana tena ili kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Aidha, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuniamini na kuniteuwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Baraza hili la kumi. Nachukua fursa hii kumuahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa juhudi na kwa uweledi mkubwa kabisa katika kuitumikia Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kusimama mbele ya Baraza lako kwa niaba ya Kamati ya Bajeti kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2022/2023.

Mhe. Spika, msingi wa hotuba hii ni Matakwa ya Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) ambayo yameelekeza kuwa, Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa yatawasilishwa katika Kamati ya Bajeti kabla ya kuwasilishwa Barazani.

Mhe. Spika, naomba nikuarifu kuwa Kamati yangu imeitekeleza vyema kanuni hiyo kwa kupokea waraka huo na kufanya majadiliano na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Aidha, katika utekelezaji wa kazi hiyo kamati yangu pia imezingatia matakwa ya kanuni ya 93(4) inayoelekeza kuwa Kamati ya Bajeti kuwaalika Wenyeviti wa Kamati za Kudumu pamoja na wadau kwa ajili ya kutoa maoni yao kuhusu taarifa hiyo.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa naomba niwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza kwa ushirikiano wao walionipatia kwa kufika mbele ya Kamati ya Bajeti na kutoa maoni yao. Aidha, kwa namna ya kipekee kabisa naomba niwashukuru wadau mbali mbali walioalikwa na kamati yangu kwa kutenga muda wao na kufika mbele ya kamati kutoa maoni yao, sisi Wajumbe wa Kamati tunathamini sana michango yao. Napenda kuwahakikishia kuwa maoni na michango yao waliyoiwasilisha ni ya umuhimu mkubwa na imezingatiwa na kamati yangu wakati wa kufanya majadiliano na serikali na wakati wa kuandaa hotuba hii.

**Mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar kwa Kipindi cha Julai – Disemba, 2020**

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai - Disemba, 2020 serikali iliendelea kuchukua juhudi na hatua mbali mbali katika kukabiliana na athari za janga la maradhi ya *Corona (Covid 19).* Kamati yangu inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuchukua hatua hizo ikiwa ni pamoja na kupunguza masharti na kuruhusu baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii kuendelea kufanyika. Kwa upande mwengine, kamati inawasisitiza wananchi nao kuwajibika na kuunga mkono jitahada hizo kwa kufuata maelekezo ya serikali yanayotolewa katika vipindi tofauti.

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar unategemea sana uchumi wa huduma kama vile shughuli za kitalii, biashara, ambazo kwa kiasi kikubwa zimeathiriwa na mripuko wa maradhi ya *Corona* na kusababisha uchumi wa nchi kushuka kutokana na ukusanyaji mdogo wa mapato katika kipindi cha Julai - Disemba 2020.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali pamoja na hatua mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa katika kukabiliana na athari za maradhi ya *Corona*, kutilia mkazo sekta nyengine za kiuchumi kama vile kilimo, uvuvi, kuimarisha viwanda vidogo vidogo, kuimarisha utalii wa ndani ili kuhakikisha uchumi wetu unakua salama pindi itakapotekeza majanga kama haya ya maradhi ya mripuko na majanga mengine mbali mbali yasiyotegemewa.

**Mfumko wa Bei**

Mhe. Spika, takwimu zinaonesha kuwa mfumko wa bei za bidhaa na huduma imeshuka na kufikia wastani wa asilimia 1.9 kipindi cha Julai – Disemba, 2020 kutoka wastani wa asilimia 2.6 kwa kipindi kama hicho mwaka 2019, hali hii inatokana na kushuka kwa bei za mafuta na kupungua kwa idadi ya watalii nchini. Kamati inaishauri serikali kuweka mikakati madhubuti ya kiuchumi kama vile kuongeza uzalishaji kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo ili kupunguza mfumko wa bei.

**Mwenendo wa Biashara**

Mhe. Spika, nakisi ya biashara imeongezeka na kufikia TZS 440.5 bilioni kutoka TZS 383.9 bilioni kwa mwaka 2019. Kuongezeka kwa nakisi ya biashara kumesababishwa na kuongezeka kwa uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi zenye thamani ya TZS 458.7 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 417.7 bilioni kwa mwaka 2019.

Mhe. Spika, ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote unategemea sana uzalishaji wa bidhaa za ndani na kuziuza nje ya nchi. Kuongezeka kwa nakisi ya biashara hutokana uingizaji mkubwa wa bidhaa za nje nchini ambao unaathiri soko la bidhaa za ndani na kusababisha uchumi wa nchi kushuka. Hivyo, kamati inaishauri serikali kuviwezesha viwanda vidogo vidogo ili kuzalisha bidhaa mbali mbali ambazo zitatumika nchini na kusafirishwa nje ya nchi na kupunguza tatizo la ajira kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, kamati inaishauri serikali kutatua changamoto za wafanyabiashara wanaosafirisha bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuondosha vikwazo visivyo vya kikodi *(Non Tax Barriers).*

Mhe. Spika, sambamba na hili, kamati inaishauri serikali kuiangalia upya Taasisi ya Viwango Zanzibar yaani *Zanzibar Bureau of Standard*, ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa hapa Zanzibar, zinazotumika Zanzibar na zile zinazosafirishwa nje ya nchi zinakuwa na viwango na ubora unaokubalika katika soko letu na masoko ya nje ya Zanzibar, ili kuongeza uzalishaji na uuzaji wa mazao yetu nje ya nchi na kupunguza nakisi au urari wa biashara.

Mhe. Spika, ununuzi wa zao la karafuu katika kipindi cha Julai- Disemba, 2020 umepungua na kufikia tani 206.5 zenye thamani ya TZS 2.8 bilioni kutoka tani 1,638.5 zenye thamani ya TZS 22.9 bilioni mwaka 2019. Pamoja na mchango wake mkubwa

katika uchumi, biashara ya zao la karafuu inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kushuka kwa bei katika soko la dunia, kupungua kwa usafirishaji wa zao hili nje ya nchi hali inayopelekea mauzo ya karafuu hushuka sana kiasi cha kuongezeka kwa nakisi ya biashara za nje, kwa lengo la kuufanya mchango wa zao la karafuu kuwa endelevu katika ukuaji wa uchumi.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali kutanua wigo wa biashara kwa kuanza utaratibu wa kulisarifu zao la karafuu na kuuza bidhaa zinazotokana na zao hilo badala ya kuuza karafuu ghafi. Aidha, kamati imebaini sehemu kubwa ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi unabebwa na zao la karafuu hali ambayo inapelekea kuwa na nakisi kubwa ya urari wa biashara inapotokea kushuka kwa uzalishaji na uuzaji wa zao hilo. Hivyo, kamati inaishauri serikali kutilia mkazo uzalishaji wa bidhaa nyengine ili kupunguza nakisi ya biashara.

**UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASKINI ZANZIBAR (MKUZA III)**

Mhe. Spika, tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar Awamu ya Tatu (MKUZA III) inaonesha kufanikiwa kwa baadhi ya malengo ya mpango huo ikiwemo kufikia kiwango cha chini cha uchumi wa kati yaani *(Low Middle Income Country)* kwa kuwa na kipato cha mtu mmoja cha US$ 1,114, kuimarika kwa upatikanaji wa maji safi na salama, ukuaji wa uchumi kufikia asilimia saba (7%) pamoja na kushuka kwa kiwango cha watu wanaoishi chini wa mstari wa umasikini kufikia asilimia 25.7 mwaka 2019/20 kutoka asilimia 30.4 mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyooneshwa katika tathmini ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III) ikiwemo suala la upatikanaji wa huduma za maji iliyoripotiwa kufikia asilimia 98.8, takwimu hizo zinakizana na hali halisi ya maisha katika jamii. Bado kuna baadhi ya maeneo yakiwemo ya mjini na vijijini yanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama. Kamati inaishauri serikali wakatiwa uwekaji wa shabaha ya viashiria na mipango ya maendeleo izingatie kuweka viashiria vinavyoendana na mazingira na vinavyoakisi hali halisi ya wananchi wetu.

**UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA PROGRAMU NA MIRADI KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA, 2020/2021**

Mhe. Spika, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ulijumuisha Programu na Miradi 94 ambayo ilipangiwa Jumla ya TZS 609.9 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka huo wa fedha ikiwa ni ongezeko la TZS 32.9 bilioni sawa na asilimia 5.7 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2019/20 ya TZS 577.0 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 197.3 bilioni sawa na asilimia 32.3 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za ndani.Jumla ya TZS 412.6 bilioni sawa na asilia 67.6 zilipangwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo ikiwemo TZS 72.5 bilioni ni ruzuku na TZS 340.5 bilioni ikiwa ni mkopo.

Mhe. Spika, utekelezaji wa mpango wa maendeleo unaonesha hadi kufikia Disemba, 2020 jumla ya TZS 139 bilioni sawa na asilimia 22.9 ya lengo la TZS 609.9 bilioni

zilitumika. Asilimia ya utekelezaji wa programu za maendeleo kwa nusu mwaka ni ndogo sana, hii maana yake miradi mingi haijaanza kutekelezwa au ipo katika hatua za maandalizi.

Mhe. Spika, kwa kuwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 umebakia muda mfupi kabla ya kumalizika, kamati inaishauri serikali kupanga bajeti ambazo zina uhalisia kwani miradi mingi inapangwa kwa miaka kadhaa lakini hakuna utekelezaji unaofanywa hata wa kazi za awali. Mathalan, katika Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar *(Zanzibar Energy Sector Transformation – ZEST)* kulitengwa TZS 19.207 bilioni katika mwaka wa fedha 2019/2020 na TZS 17.85 bilioni katika mwaka wa fedha 2020/2021 lakini kiuhalisia mradi huu haujaanza kutekelezwa na wala haiwezekani kutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha kwa sababu mradi ndio kwanza upo katika maandalizi ya awali.

Mhe. Spika, Kikao cha Bodi ya Benki ya Dunia cha kuidhinisha ombi la mradi huo kimepangwa kufanyika Septemba, 2021 ambapo itakuwa ni mwaka wa fedha mwengine (2021/2022). Kamati inaishauri serikali, kuijengea uwezo Tume ya Mipango, ili iweze kupanga mipango ya serikali kwa uweledi na uhalisia, kuepuka kuingiza miradi ambayo haitatekelezeka katika muda husika. Hii itaondosha kupandisha Bajeti ya Serikali ambayo mara nyengine inakosa uhalisia.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI KWA MAENEO YA VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA JULAI – DISEMBA, 2020

Mhe. Spika, waraka wa Mwelekeo wa Hali Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022 - 2022/2023 unaeleza utekelezaji wa miradi kwa maeneo ya vipaumbele kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2020. Kati ya vipaumbele vya juu 13 vilivyoainishwa kutekelezwa, vipaumbele tisa tu ndivyo vilivyoanza kutekelezwa au kuendelea kutekelezwa.

Mhe. Spika, sehemu kubwa za vipaumbele hivyo tisa vilivyoanza kutekelezwa vipo katika hatua ya chini kabisa mfano Mradi wa Ujenzi wa Hospitali Mpya ya Rufaa ya Binguni, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake - Wete na Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, kamati inaisisitiza serikali kuhakikisha kuwa vipaumbele vinavyoainishwa kupitia bajeti vinatekelezwa ipasavyo na pia serikali kuendelea kusimamia wizara na taasisi zake kwa kuhakikisha kuwa, maeneo yanayoainishwa katika bajeti yanafanyiwa kazi kwa wakati na kuondosha kasoro mbali mbali ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika miradi. Kamati inaiomba serikali kuendelea kusimamia taasisi zake ili ziweze kusimamia vyema mikataba na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo.

## UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021 KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (JULAI – DISEMBA, 2020)

Mhe. Spika, Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaokuja huzingatia pia utekelezaji wa bajeti kwa miaka iliyopita na bajeti inayoendelea katika maeneo  mbali mbali ikiwemo yale yanayogusa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo

vya ndani na vya nje. Katika bajeti ya mwaka 2020/2021, serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 1,579.2 bilioni. Hali halisi ya ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa kipindi cha miezi sita ni jumla ya TZS 464.6 bilioni sawa na asilimia 59.6 ya lengo la TZS 779.4 bilioni.

Mhe. Spika, kwa kuwa upatikanaji wa mapato kwa kipindi cha miezi sita umefikia asilimia 59.6 tu ya lengo lililopangwa na kwa kuzingatia kuwa, utekelezaji wa bajeti unaoleta tija kwa wananchi unategemea na upatikanaji mzuri wa mapato ya ndani na ya nje, kamati inaishauri serikali, kuendelea na usimamizi madhubuti wa taasisi zote zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato kwa kipindi kilichobakia cha utekelezaji wa bajeti ya 2020/2021 ili mapato yaweze kupatikana kwa kiwango cha juu zaidi ukilinganisha na miezi sita iliyopita na yaweze kutumika katika kuwapatia huduma mbali mbali wananchi.

Mhe. Spika, kamati imearifiwa kuwa, miongoni mwa sababu zilizopelekea kushuka kwa mapato kwa kipindi cha miezi sita iliyopita ni pamoja na mripuko wa maradhi ya *COVID 19*. Kwa kuwa utekelezaji wa shughuli za kawaida na za maendeleo unategemea sana upatikanaji wa mapato ya ndani na ya nje, kamati inaishauri serikali kuandaa mipango ya muda mfupi na muda mrefu ikiwemo kutanua wigo wa sekta mbali mbali za kiuchumi ili kukabiliana na hali tofauti za mitikisiko ya kiuchumi zinazoweza kujitokeza.

**Mfuko wa Miundombinu**

Mhe. Spika, kamati ilipopitia matumizi ya Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha miezi sita (Julai – Disemba, 2020), ilibaini jumla ya TZS 44.2 bilioni zilipangwa kutumika kwa mwaka na ambapo kiasi cha TZS 10.2 bilioni zimetumika katika kugharamia miradi minane (8) kati ya miradi kumi na tano (15) iliyopangwa kwa mwaka sawa na asilimia 23 ya utekelezaji. Miongoni mwa miradi inayopata mgao wa fedha za mfuko ni pamoja na mradi wa Uimarishaji Uvuvi wa Bahari Kuu, Mradi wa kuimarisha Taasisi za Viwango na Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini ambapo kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2020 miradi yote hii haikupata mgao wa fedha za Mfuko waMiundombinu.

Mhe. Spika, kamati inapata wasi wasi juu ya utekelezaji wa miradi inayotumia fedha zinazotokana na Mfuko wa Miundombinu iwapo miradi hiyo ndio iliyolengwa kwa mujibu wa uanzishwaji wa mfuko huo. Aidha, kamati inaishauri serikali kuweka utaratibu madhubuti wa utumiaji wa fedha zinazotokana na Mfuko wa Miundombinu ili kuepusha matumizi tofauti na malengo ya uanzishwaji wa mfuko huo. Aidha, kwa mwaka wa fedha huu wa 2020/2021, fedha zinazotokana na Mfuko wa Miundombinu hazitarajiwi kufikiwa kukusanywa kama zilivyopangwa, kamati inaishauri serikali, kutoa taarifa ni jinsi gani fedha hizo zitaweza kukusanywa na kutumika kwa ukamilifu katika miradi iliyopangwa.

**Matumizi ya Serikali za Mitaa**

Mhe. Spika, jumla ya TZS 81.2 bilioni zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa mwaka 2020/2021 ambapo TZS 70.9 bilioni ni matumizi ya Ruzuku ya Mshahara na TZS 10.3 bilioni ni matumizi ya Kuendesha Ofisi. Matumizi halisi kwa

kipindi cha Julai – Disemba 2020/21 yamefikia TZS 39.7 bilioni sawa na asilimia 97.8 ya makadirio ya TZS 40.6 bilioni.

Mhe. Spika, kama ilivyo kwa Serikali Kuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa hupata fedha kutoka kwenye vyanzo mbali mbali na kwa kuwa, mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022 –2023/2024 hayajaonesha mapato na vyanzo vyake ya Serikali za Mitaa, Kamati inashauri kuongezwa kwa kipengele hicho ili yaweze kufahamika na kuonesha taswira halisi katika Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali.

**Deni la Taifa**

Mhe. Spika, kamati imepokea taarifa ya Deni la Taifa kwa kipindi cha Julai – Disemba 2020/21 lililofikia TZS 896.2 bilioni ukilinganisha na kiasi cha TZS 822.5 bilioni kwa kipindi kama hicho Disemba, 2019. Kati ya deni hilo, deni la nje ni TZS 691.5 bilioni na deni la ndani ni TZS 204.9 bilioni. Kiwango hicho cha deni la ndani kwa wastani wa uwiano wa deni kwa uchumi (*Domestic Debt to GDP ratio*) ni asilimia 22, kiwango hicho kinaonesha kuwa, deni ni himilivu.

Mhe. Spika, kamati inashauri wakati wa kupima uhimilivu wa Deni la Taifa, tusijitosheleze kwa kigezo kimoja cha kupima uwiano wa deni na pato la taifa pekee badala yake iangalie vigezo vyengine ambavyo vinaweza kutupa picha halisi ya uwezo wa kukopa ikiwemo kigezo cha uwiano wa deni na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi (*Debt to Export*) na uwiano deni na ukusanyaji wa mapato (*Debt to Revenue*). Vigezo hivi vitatupa vile vile njia bora ya kuweka mikakati ya kusimamia deni letu la ndani kwa umakini kwa kuwa deni la nje, kwa kiasi kikubwa linadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kamati inaishauri serikali iendelee kukopa kwa umakini na kwamba, fedha zinazokopwa, zielekezwe katika miradi yenye kuleta tija na uzalishaji.

**MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2020/2021**

Mhe. Spika, mwenendo wa makusanyo wa mapato ya ndani katika kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021 yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1,137.7 bilioni sawa na asilimia 72 ya makadirio ya TZS 1,579.2. Kamati inaishauri serikali kusimamia vyema makusanyo katika kipindi kilichobakia cha utekelezaji wa bajeti ya 2020/2021 na kuhakikisha kuwa, changamoto za upungufu wa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha Julai – Disemba 2020/2021 zilizojitokeza kutokana na mripuko wa maradhi ya *COVID 19* pamoja na nyenginezo zinafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi,hadi kufikia Juni 2021 matumizi ya serikali yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 1,137.7 bilioni sawa na asilimia 72 ya Bajeti Kuu ya Serikali ya TZS 1,579.2 bilioni. Kamati inaishauri serikali kuendelea kusimamia taasisi zake katika kufanya matumizi yanayozingatia taratibu za mipango ya kazi zao sambamba na kusimamia taasisi hizo kwa karibu katika shughuli zote za manunuzi zinazofanyika ili kuhakikisha kuwa taratibu zinafuatwa na kupatikana kwa thamani ya fedha halisi zinazotumika kwa kila kazi iliyopangawa. Aidha, kamati inaishauri serikali kusimamia mashirika yake na taasisi zinazojitegemea, ili zisifanye matumizi ambayo hayakupangiwa bajeti katika kipindi hichi kilichobakia. Kamati pia inaishauri serikali kuwa makini inapotoa fedha za matumizi mengineyo (*Other Charges – OC*) katika

kipindi hichi ambacho tunaelekea mwishoni mwa mwaka wa fedha, kwani kuna baadhi ya taasisi zinapanga matumizi ambayo hayana tija ilimradi tu fedha hizo zitumike na zisirudishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021/2022 – 2023/2024**

Mhe. Spika, mwelekeo wa uchumi kwa mwaka wa 2020/2021 unalenga kuyafanyia kazi maeneo ya msingi ya ukuwaji wa uchumi yakiwemo Uchumi wa Buluu na viwanda vidogo vidogo. Kamati inaishauri serikali kutolewa ufafanuzi namna maeneo haya yatakavyofungua fursa za kiuchumi kama ambavyo yametajwa katika Dira ya Maendeleo ya 2050 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi mwaka 2020-2025 na ahadi za Mhe. Rais. Kamati pia inaishauri serikali kuonesha namna ya fursa za ajira hususan kwa vijana zitakavyopatikana kupitia maeneo hayo na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuendeleza uchumi. Tukumbuke kuwa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020–2025, inaazimia kuzalisha ajira laki tatu katika kipindi cha miaka mitano.

**MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO 2021/2022 – 2023/2024**

Mhe. Spika, Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 utazingatia malengo na mikakati inayotokana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Kamati imebaini kasoro zilizojitokeza katika tathmini iliyofanywa ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020 zikiwemo kukosekana kwa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini *(M&E framework)*. Hali hii imepelekea kuwa na ugumu wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa Dira hiyo katika baadhi ya maeneo na kutokuwepo kwa takwimu za kutosha kutoka katika sekta mbali mbali.

Mhe. Spika, katika Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, serikali inapaswa kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini (*M&E framework*) sambamba na Mpango wa Maendeleo ili tathmini zinazofanywa ziendane na hali halisi. Kamati imebaini baadhi ya miradi kuripotiwa utekelezaji wake kinyume na uhalisia wa hatua zilizofikia katika uendelezaji wake kwa mfano Ujenzi wa Hospitali ya Wete. Katika hatua hii, serikali iendelee kuimarisha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini katika taasisi zake ili utekelezaji wa miradi na shughuli nyengine za serikali ziendane na uhalisia uliopo.

**VIPAUMBELE VYA KITAIFA 2021/2022 – 2023/2024**

Mhe. Spika, miongoni mwa nyaraka zilizotumika kutengeneza Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo 2021/2022 – 2023/2024 ni Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2020-2025 na Hotuba ya Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi.

Mhe. Spika, licha ya nyaraka hizi kuweka msisitizo katika udhibiti na uimarishaji wa mapambano dhidi ya rushwa, uhujumu uchumi na ufisadi pamoja na udhalilishaji wa wanawake na watoto lakini katika taarifa hii maeneo haya hayakupewa kipaumbele. Kamati inaishauri serikali kuyapa kipaumbele maeneo haya kwani ni muhimu sana

katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa Zanzibar na ni maeneo mtambuka. Aidha, kamati inampongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchukua hatua madhubuti dhidi ya udhalilishaji, ufisadi na rushwa, kutoa maagizo ya kuanzishwa Mahakama ya Kupambana na Udhalilishaji na Mahakama ya Kupambana na Ufisadi na Uhujumu Uchumi.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mpango wa Maendeleo 2021/2022 – 2023/2024 unakwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025, kamati inaiomba serikali kuzingatia maeneo mengine kwa ajili ya kuleta maendeleo na kuyafikia malengo ya Ilani. Hatua hizi ni pamoja na ushirikishwaji wa Watanzania waliopo nje yaani *Diaspora* katika maendeleo ya Zanzibar na kutiliwa mkazo uanzishwaji wa vituo vya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambavyo vitasaidia sana vijana kuweza kupata ujuzi wa kiteknolojia.

Mhe. Spika, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imehakikisha vile vile kwamba katika kipindi hichi, kutakuwa na hatua za matayarisho na uanzishwaji wa Soko la Mitaji la Zanzibar yaani **Zanzibar** *Stock Market*. Kwa kuwa hali ya uchumi ya wananchi Zanzibar pekee, inaonesha utayari wao wa kuweza kununua na kuuza hisa katika makampuni mbali mbali ya kitaifa na kimataifa ambayo yatakuwa yamejiorodhesha katika Soko la Hisa la Zanzibar, kamati inaishauri serikali kuanza matayarisho ya uanzishwaji wa Soko la Mitaji la Zanzibar yaani *Zanzibar Stock Market*.

**MWELEKEO WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

Mhe. Spika, jumla ya TZS 1,506.2 bilioni zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika mwaka wa fedha 2021/2022 hii ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 4.6 ya bajeti ya mwaka 2020/2021. Aidha, jumla ya TZS 1,105.5 bilioni zimekadiriwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani.

Mhe. Spika, ukilinganisha kiasi cha fedha kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutoka katika vyanzo vya ndani ni kikubwa zaidi kuliko kiasi kilichopangwa kukusanywa katika vyanzo vya ndani mwaka 2020/2021.

Mhe. Spika, kwa kuwa sekta nyingi za kiuchumi zimeathirika kutokana na mripuko wa Ugonjwa wa *CORONA*. Kamati inapendekeza kubainishwa kwa mikakati madhubuti ya kisera, kikodi na ya kibajeti itakayofanikisha ukusanyaji wa mapato hayo unaongezeka licha ya kuwepo mdororo wa kiuchumi uliosababishwa na ugonjwa huo.

Mhe. Spika, kabla ya kumalizia hotuba hii napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kupanga vyema safu ya watendaji serikalini na kwa kufanya teuzi mbali mbali. Maendeleo ya nchi yanategemea mchango wa watumishi wa umma. Uwajibikaji wa watumishi wa umma utaiwezesha Zanzibar kufanikiwa katika nyanja tofauti kama vile ujenzi wa miundombinu, kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato ya serikali na pia kutoa huduma bora kwa wananchi.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kukushukuru wewe pamoja na Katibu wa Baraza kwa mashirikiano ya karibu pamoja na miongozo mbali mbali mliyokuwa mkiipatia kamati katika kipindi chote cha kazi za kamati. Naomba vile vile nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Uchumi pamoja na watendaji wake kwa kutoa mashirikiano ya dhati kwa kamati pale ambapo tulipokuwa tukitoa hoja zetu kwa umahiri. Nawashukuru vile vile wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa utulivu. Aidha, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao na ustahamilivu wao wakati tukitekeleza majukumu ya kamati.

Mhe. Spika**,** ili kuzipa uzito shukurani zangu kwa Wajumbe wa Kamati na kwa faida ya kuweka kumbukumbu nzuri kwenye Taarifa Rasmi za Baraza (*Hansard*), naomba uniruhusu niwataje kwa majina yao Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Said Saleh Salim | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Anna Athanas Paul | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| 6. | Mhe Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Harusi Said Suleiman | Mjumbe |

Mhe. Spika, aidha napenda kuishukuru Sekretariati ya Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano mzuri, ushauri na miongozo wanayoipatia kamati yangu**.** Naomba nao niwashukuru kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Abdalla Ali Shauri | 2. Ndg. Asha Said Mohamed |
| 3. Ndg. Shaib Fadhil Shaib | 4. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi |

Mhe. Spika, kwa kuwa msingi wa taarifa hii ni kutoa picha halisi ya mwelekeo wa bajeti ijayo na kuipa fursa serikali kuchukua maoni mbali mbali yenye lengo la kuiboresha bajeti, ni matumaini ya kamati yangu kuwa maoni na ushauri uliotolewa na kamati yangu pamoja na ushauri utakaotolewa na Wajumbe wa Baraza lako utazingatiwa na serikali katika matayarisho ya bajeti ya mwaka 2021/2022. Aidha, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako waichangie taarifa hii ili kuipa fursa serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuyachukua maoni na mapendekezo yao kwa lengo la kutayarisha bajeti ijayo iliyo bora na inayoakisi uhalisia na matakwa wa wananchi na ambayo inakwenda sambamba na kasi na malengo ya Serikali ya Awamu ya Nane.

Mhe. Spika, nashukuru sana na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Waheshimiwa Wajumbe, baada ya uwasilishaji huo wa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati sasa ni wakati wa kuchangiwa kwa hoja hii na mpaka sasa hivi nina wajumbe wanne tu kwa sasa hivi ambao wameleta maombi yao, na naomba niwataje watatu wa mwanzo ili wengine wanaweza kuendelea kuleta maombi yao. Naomba nianze na Mhe. Habibu Ali Mohamed kama mchangiaji wetu wa mwanzo ambaye atafuatiwa na Mhe. Bakar Hamad Bakar na Mhe. Shamata Shaame Khamis ajiandae.

**Mhe. Habibu Ali Mohamed:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka 2021/22-2023/2024.

Mhe. Spika, naomba nijielekeze mchango wangu katika kuhuisha uzalishaji wa zao la karafuu. Mhe. Spika, kama inavyoeleweka zao la karafuu ni zao ambalo linaingizia fedha za kigeni Serikali yetu ya Zanzibar. Mhe. Spika, katika mwaka 2011 bei ya soko la dunia iliongezeka na ilikuwa ni faraja kwa wakulima wetu wa karafuu kuongezwa bei hili, na hii ilipelekea mashamba mengi katika kisiwa cha Unguja na Pemba yakawekwa katika hali nzuri, ya usafi, wananchi na wakulima wakashajihishwa wakapanda mikarafuu mingi na leo hii tunafikia katika mwaka 2020 mikarafuu ile ambayo imelelewa tokea mwaka 2011 mpaka 2020 imeshakuwa inazalisha.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba bei ya karafuu imeongezeka lakini Shirika la *ZSTC* linaendelea kupata hasara na serikali ya awamu iliyopita ilisema bei ya karafuu haitoteremshwa itabakia kama ilivyo, yaani wakulima wanunuliwe karafuu zile kwa asilimia 80.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba bado bei ya karafuu inaendelea kushuka, sijui serikali imejipanga na mikakati gani kuhakikisha kwamba Shirika la *ZSTC* halipati hasara, lazima tuangalie. Kwa sababu kuna *difference* kubwa inaonekana sasa hivi na serikali haijaziba lile pengo ambalo *ZSTC* imepata hasara. Mpaka sasa ukiangalia *ZSTC* kuna wafanyakazi wamestaafu miezi minane iliyopita nyuma hawajawalipa mafao yao, wakati kipindi cha nyuma kwa kumbukumbu zangu ni kwamba haiwezi kufika miezi miwili au mitatu wafanyakazi wasipate mafao yao. Kwa hivyo, lazima serikali ije na mikakati kwamba itaweza kulipa lile pengo ambalo serikali imesema kuwa bei ya karafuu ibakie ile ile na bei ya soko la nje ilikuwa imeshuka. Hilo naomba serikali iliangalie kwa vizuri kwenye masuala ya bei.

Hata sasa hivi kuna wasi wasi mkubwa kwa wakulima wa karafuu ambao tayari wameshafuatwa kwa ajili ya kukodi mikarafuu, lakini wana wasi wasi kwamba bei ya karafuu huenda ikashuka. Kwa hivyo, tuitake serikali ije na kauli ambayo itasema bei ya karafuu itaendelea kubaki hii hii au kutakuwa na mabadiliko yoyote ya bei hiyo ili wakulima sasa hivi wajitayarishe kwa ajili ya kwenda kukodi mikarafuu. Ukitizama ni kwamba msimu huu kuna karafuu nyingi zimezaliwa zinaweza zikafika tani 6,000 mpaka 8,000 kwa sababu mikarafuu imezaa sana. Mimi mwenyewe nina shamba la mikarafuu miaka miwili haijazaa lakini sasa hivi inaonesha dalili nzuri za kupata karafuu za kutosha. Kwa hivyo, inatakiwa serikali ijipange vizuri pia na masuala ya mikopo yanakuwa na riba kubwa, sijui Shirika la *ZSTC* litafanya njia gani kuweza kupata fedha kwa ajili ya karafuu msimu unaokuja.

Jengine ambalo nataka nichangie ni ukurasa wa nne katika kitabu hiki cha Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti. Imeonesha kwamba uzalishaji wa unga wa ngano umeongezeka kutoka tani 18,849 mpaka tani 23,580 na mahitaji ya makisio unga wa ngano kwa Zanzibar ni karibu tani 43,000, hii inaonesha ni faraja kubwa. Uagiziaji wa unga wa ngano kutoka nje ya nchi umepungua kutoka tani 5,708 mpaka 2,607. Kwa hivyo, naona serikali hapa itoe vivutio maalum kwa wawekezaji ili kuanzisha viwanda vya bidhaa hizi, tupunguze kutumia fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya kuagiza unga wa ngano kutoka nje ya nchi.

Mhe. Spika, jengine ambalo nimeliona hapa sijaona takwimu za uzalishaji wa mpunga kwa Zanzibar wakati tunasema kwamba tuna mabonde, tunatumia *irrigation system* kwa ajili ya umwagiliaji. Kwa hivyo na hili nataka liangaliwe, sijaona kabisa hapa kwenye ukurasa nambari nne.

Jengine ni suala la sukari. Tuna kiwanda cha Mahonda na tatizo la sukari bado lipo tunaagiza sukari kutoka nje. Kwa hivyo, serikali iandae mkakati maalum wa kuhakikisha kwamba kiwanda cha Mahonda kinazalisha sukari ya kutosha ili kupunguza uagiziaji wa sukari kutoka nje. Hata ukiangalia katika kisiwa cha Pemba tuna wakulima wengi wa miwa, kwa hivyo tuangalie uwezekano wa kujenga kiwanda cha miwa Pemba kupunguza uagiziaji wa sukari kutoka nje.

Mhe. Spika, kwenye Mwelekeo wa Mapato. Hapa matarajio ya ukusanyaji wa mapato tumeambiwa ni 1.5 trilioni kwa mwaka 2021/2022 ambapo kati ya fedha hizo 1.1 trilioni sawa na asilimia 73 yanayotokana na mapato ya ndani na mwenendo mzuri wa serikali. Mimi naishauri serikali iongeze msukumo kwa taasisi zile ambazo zinakusanya mapato kama *TRA*, *ZRB*, tuhakikisha kwamba kule hakuna ufisadi, hakuna rushwa, hakuna wizi. Hapa serikali itakuwa imefanya kazi ya ziada kwa mujibu wa mwelekeo wa bajeti ambao umeoneshwa katika kitabu hiki.

Mhe. Spika, vimetajwa vipaumbele karibu 13 hapa ambapo serikali ilipanga kutumia shilingi 2,56.6 bilioni kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele hivyo katika ukurasa wa 17. Hiyo ni ya mwezi wa Julai – Disemba 2020. Jumla ya shilingi 55.9 bilioni sawa na asilimia 21.7 zilipatikana kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele hivyo. Sasa mheshimiwa mimi hapa nashauri, tumetenga fedha hizo lakini zilizopatikana ni kidogo, kwa hivyo naishauri serikali vile vipaumbele viko vingi hivyo tuangalie vipaumbele vichache ambavyo vitatekelezeka kwa mujibu wa fedha tulizonazo.

Mhe. Spika, mchango wangu ni huo katika Kitabu hiki cha Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti, naomba niishie hapo nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Habibu Ali Mohamed naomba sasa nimwite Mhe. Bakar Hamad Bakar atafuatiwa na Mhe. Shamata Shaame Khamis na Mhe. Suleiman Makame Ali ajiandae.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nami kuweza kuchangia Hotuba hii ya Mwelekeo wa Hali ya Kiuchumi, Mpango wa Maendeleo pamoja na Bajeti ya Mwaka 2021/2024.

Mhe. Spika, kabla sijaenda kwenye uchangiaji wa hotuba hii naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyeweza kunisimamisha hapa, lakini pia kutujaalia afya njema sisi wajumbe na kuweza kutekeleza majukumu yetu kama ambavyo sheria inatutaka.

Pia naomba kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwanza kwa ushindi mkubwa wa kishindo asilimia zaidi ya 76, lakini pili kwa namna ambavyo anajipambanua na utendaji wake wa kazi wa uwazi na ukweli

ambapo tunaushuhudia sasa. Mhe. Spika, namtakia umri mrefu na afya bora Rais wetu huyu ili tuendelee kushuhudia mambo mema ambayo amejipangia ama tumepanga kuyafanya kwa Zanzibar yetu.

Mhe. Spika, kipekee niwashukuru wananchi wa Jimbo la Wawi kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao, lakini pia nikishukuru chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kuniteuwa na kunisimamia mpaka nikapata ushindi huu au ushindi wa kishindo.

Mhe. Spika, sitotenda haki kama sitompongeza na kumshukuru sana Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango kwa namna ya uwasilishaji wake na uandaaji wa kitabu hiki kwa hotuba hii, amefanya *presentation* nzuri, hotuba hii ni nzuri na mimi sina budi nimpongeze kwa hotuba yake hii ya mwanzo, inaonekana kama vile ni mzoefu wa miaka mingi kwenye mambo haya.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye kuchangia hotuba hii moja kwa moja na mimi kwenye mchango wangu nitajikita kwenye ukurasa wa 23, 24 hadi 25. Kwenye ukurasa wa 23 kuna vipaumbele vya taifa kwa mwaka huu wa 2021/2022 kwa maana ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022. Vipaummbele hivi kwenye *list* hii ni vipaumbele 17.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu naona vipaumbele hivi ni vingi sana hasa ukizingatia kwamba vipaumbele vya miaka mitatu ni vipaumbele saba tu, lakini ukija vipaumbele vya mwaka huu mmoja tunavikuta viko 17. Nashauri kwa Mhe. Waziri aende akavi-*group* kama ambavyo ame-*group* kwenye vipaumbele vya miaka mitatu na hivi viwe vipaumbele vichache visionekane kwamba tuna vipaumbele vingi na kutokana na rasilimali tulizonazo naamini kwa vipaumbele hivi hatuwezi kuvitekeleza kwa pamoja. Kwa hivyo, aende akavi-*group* ili tuangalie namna gani ya kuweza kuvitekeleza.

Sambamba na hilo, kuna vitu vya msingi ambavyo kila siku Mhe. Rais amekuwa akivisemea hatuvioni kama ni vipaumbele vya mwaka wetu huu wa 2021/22. Suala kama la Utawala Bora, suala hili kila siku Mhe. Rais amekuwa analizungumza lakini kwenye *list* hii ya vipaumbele 17 sikioni kipaumbele hiki cha utawala bora, *issue* ya ubadhirifu wa mali za umma, wizi, uzembe, rushwa, sijakiona hicho kwenye vipaumbele ambavyo tunavyo. Kwa hivyo, namshauri sana Mhe. Waziri jambo hili pia aliingize kwenye vipaumbele vyetu atafute namna ya kuweza kuliingiza jambo hili kwa sababu ndilo jambo ambalo tunakwenda nalo kwa sasa hivi. Mheshimiwa ni lazima tuwadhibiti wala rushwa, tuwadhibiti wazembe, wabadhirifu wa mali za umma na ili kuwadhibiti huko ni lazima tuwe na kipaumbele kwenye *list* ya vipaumbele hivi, lazima tuliingize jambo hili.

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii inachangia zaidi ya asilimia 28 ya pato la nchi yetu, lakini kwa masikitiko makubwa sijaona kwenye *list* ya vipaumbele hivyo 17 Sekta ya Utalii imepewa fungu lipi. Kwa hivyo, nashauri Mheshimiwa, namshauri Mhe. Waziri aangalie namna ya kuiweka sekta hii ya utalii kipekee kama pia ni kipaumbele cha nchi yetu. Nchi yetu hii ni nchi ya visiwa tunategemea sana suala la utalii ili kuongeza mapato yetu, mimi ninavyoona hata hio asilimia 28 ni ndogo sana kwa utalii. Kwa hivyo, kwanza tuziingize kwenye kipaumbele chetu lakini pia tutafute namna ya kuboresha upatikanaji wa mapato ambayo yanatokana na sekta ya utalii. Tuitangaze nchi yetu,

tuvitangaze vivutio vya nchi yetu ili kuongeza idadi ya utalii lakini pia kuboresha uwanja huu mpana wa sekta hii nzima ya utalii.

Mhe. Spika, kwenye kipaumbele nambari 15 nimeona kwamba kuna kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kidijitali ya utendaji wa kazi kwa ujumla kwa maana ukusanyaji wa mapato, usimamizi na matumizi pamoja na manunuzi.

Mhe. Spika, tuna sheria nambari 12 na 11 kama sikosei ya mwaka 2016, sheria hizi ni Sheria ya Fedha na Sheria ya Manunuzi. Pamoja na mapungufu makubwa yaliomo ndani ya sheria hizi, lakini hadi leo sheria hizi hazina kanuni. Mhe. Waziri tumuombe sana sasa imefika wakati wa kuzitungia kanuni sheria hizi lakini pia ziangaliwe namna ya kuweza kuziboresha yale mapungufu ambayo yamo kwenye sheria hizi aweze kutuletea tuweze kwenda kuzibadilisha na kuzitengenezea mazingira mazuri kwa ajili ya uchumi mpana wa nchi yetu. Mapungufu yaliomo kwenye sheria hizi ndio hayo ambayo wanayatumia baadhi ya watendaji ambao sio waaminifu kuweza kufanya ubadhirifu mkubwa kwenye sekta hizi za umma. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nimuombe sana kwenye suala hili alipe kipaumbele kikubwa tangu mwaka 2016 hatuna kanuni zinazoweza kuziongoza sheria zetu hizi mbili, Sheria nambari 11 na 12.

Mhe. Spika, nije kwenye kipaumbele nambari moja ambacho ni Kuendelea na Matayarisho ya Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba. Mheshimiwa tumekuwa tunafanya miradi mingi kwenye nchi yetu, changamoto ambayo tunakuwa tunakutana nayo ni namna ambavyo tunawatenga wazawa kwenye masuala ya miradi mikubwa kama hii. Nimuombe sana Mhe. Waziri ambapo tutakuja kutekeleza jambo hili tuwape kipaumbele wazawa kwenye miradi ya maendeleo mikubwa kama hii pamoja na mradi huu, lakini pia kuna miradi ya ujenzi wa barabara mbali mbali. Wananchi wetu tulionao hasa wazalendo wa nchi hii ndio ambao pia tunawatumia kama ni walinzi wa miradi hii na walinzi wa mali za umma. Kwa hivyo, tunapoanza kuwabagua, kuwatenga kwamba hatuwashirikishi kwenye miradi hii mikubwa tunatengeneza *gape* kubwa ambao linaweza kuepukika. Kwa hivyo, nimshauri sana Mhe. Waziri kwenye mradi huu wa Uwanja wa Ndege pamoja na miradi mengine ambayo itatekelezwa tuwatumie sana wazawa hasa kwa yale maeneo ambayo wana uwezo nayo kuyafanya.

Mhe. Spika, pia nakuja kwenye kipaumbele nambari saba ambacho ni Kuendelea na Utekelezaji wa Programu ya Ajira kwa Vijana. Mhe. Spika, programu hii haikuanza leo ipo ndio maana Mhe. Waziri akasema ni kuendelea kwa programu hii. Programu hii ambayo ipo imejaa malalamiko na ukakasi mkubwa, kiukweli kwa programu hii ambavyo imetekelezwa haijawatendea haki vijana. Mimi nazungumza niki-*declare interest* nilikuwa Mwenyekiti wa Baraza la Vijana lakini pia nilikuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana Taifa, programu hii haijawatendea haki vijana. Tunaambiwa kuna shilingi bilioni tatu ambazo zimetumika lakini ukiziangalia uhalisia wa fedha hizi kiukweli usiofichika huzioni.

Mhe. Spika, vimenunuliwa vyarahani kwenda kupelekwa kwenye vikundi vya vijana ukienda kufanya utafiti wa vyarahani hivyo vyote vimelala sasa hivi au kama sio vyote basi ni zaidi ya asilimia 95, ukifanya utafiti vyarahani vyote ni vibovu. Tunaambiwa kuna mradi wa kilimo cha pilipili uko wapi. Kwa hviyo, tunawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri kwenye programu hizi naamini Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo namuamini sana, Makamu wangu Mwenyekiti wa Umoja wa

Vijana Taifa naamini wizara hii ataitendea haki. Namuomba sana aende akafanye utafiti kwenye jambo hili programu hii imeanza lakini haijafanya vizuri.

Mhe. Spika, pia naomba nielekee kwenye eneo la Mapato ya Ndani. Kwenye eneo hili la mapato ya ndani kuna *dividend* za mashirika mbali mbali ya umma. Hapa imewekwa shilingi bilioni 11 kama ni makisio ya *dividend* kwenye mashirika haya ya umma kwa serikali. Kwa *list* ya mashirika tuliyonayo Zanzibar na *amount* hii ya *dividend* ni ndogo mno. Tunakuomba sana Mhe.Waziri uyaangalie tena upya mashirika haya na *dividend* ambazo wanapata wanaigawia serikali. Mashirika mengi tuliyonayo yanaendeshwa kwa hasara kubwa, watendaji wanayatumia wanavyotaka wenyewe, tunakuomba sana Mhe. Waziri uyaangalie upya mashirika yetu. Lakini pia na mawiziri ambao wanayaendesha mashirika haya kwa sababu mashirika haya yamo ndani ya wizara tofauti, lakini ukiangalia wingi wake na *dividend* hii ambayo imewekwa hapa, gawio hili la serikali ambalo limewekwa hapa bilioni 11 ni ndogo mno.

Mhe. Spika, pia nije kwenye suala la matumizi, bila ya udhibiti wa matumizi ya fedha za serikali kila siku itakuwa ni hadithi tu. Nakuombeni sana Waheshimiwa Mawaziri matumizi yanayofanyika hasa kwenye mashirika…

**Mhe. Spika:** Naomba umalizie mheshimiwa.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar**: Nakushukuru Mhe. Spika. Kwenye mashirika yetu ni matumizi mimi nayaita matumizi mengine ni ya ovyo, nakuombeni sana kuna mambo ambayo ukiambiwa pesa zimetumika kwa kweli hayaingii akilini. Sisi tumekwenda tumeona, mtu mmoja analipwa kwenye vipengele tofauti vitatu lakini kwa jambo moja, mtu huyo huyo mmoja analipwa pengine mara tatu, mara nne jambo moja lakini limetengenezewa majina tu, jina hili, posho hili lakini mwelekeo wa jambo lile ni moja. Kwa hiyo, nikuombeni sana Waheshimiwa Mawaziri kuliangalia upya jambo hili.

Lakini pia nimalizie kwa kutoa mapendekezo yangu kwenye suala la mgawanyo wa matumizi, matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Mhe. Spika, wananchi wanatupima zaidi kwenye matumizi ya maendeleo.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa nakushukuru sana muda wako umekwisha.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar**: Nakushukuru sana Mhe. Spika, lakini napendekeza kwamba matumizi ya maendeleo yawe asilimia angalau 40. Ahsante.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Bakar Hamad Bakar. Mheshimiwa anayefuata sasa hivi ni Mhe. Shamata Shaame Khamis na ajiandae Mhe. Suleiman Makame Ali.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena na mimi natumia fursa hii, kwanza kabisa kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uzima na afya hata tukawepo hapa tukiwa tunatekeleza majukumu ya uwakilishi kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu.

Mhe. Spika, vile vile naomba nitumie fursa hii kuendelea kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanayoendelea kuifanya katika nchi yetu kwa lengo la kuendeleza, kuijenga nchi yetu kutoka pale

ambapo imefikia katika Awamu ya Saba na kuendeleza katika kasi nyengine mpya kwa Awamu hii ya Nane. Mwenyezi Mungu awajaalie kheri zaidi na ufanikishaji mzuri na mwema uliotukuka zaidi.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea ningeomba nitumie fursa hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa mara nyengine tena kwa kuendelea kunivumilia na kuniamini kuendelea kutekeleza majukumu yao kama vile ambavyo wamenituma. Lakini baada ya utangulizi huo, naomba kabla sijachangia niombe kidogo kwa Mhe. Waziri tuangalie kufanya marekebisho madogo kama itaruhusu ikiwa utaalam ndio unaonesha hivyo, basi naomba nisikilizwe kidogo katika mchango wangu mimi nitaanza kwenye ukurasa wa 20 mpaka 23 sitotumia kwenda nje ya hapo.

Lakini vile vile kwenye vipaumbele vya kitaifa kwa mwaka 2021-2022-2023-2024 kuna vile vipaumbele vimeainishwa viko saba, lakini kipengele namba 1 amesema kuimarisha miundombinu, lakini vile vile kipengele namba 2 kimesema kuimarisha Sekta ya Kukuza Uchumi, na kipengele namba 3 kimejificha kidogo nilitaka hapo kiainishwe ili kiweze kusomeka vizuri kwa mtiririko huo mheshimiwa ambao ameukusudia kama amenielewa. Lakini sambamba na hilo, ukitoka namba 4 na 5 vinaonekana vizuri lakini namba 6 kimejificha kama kwamba hakipo kimekwenda na mtitiriko vile kuimarisha Sekta ya Mtambuka. Naomba na hiyo waiweke sawa ili iweze kusomeka vizuri waheshimiwa isitupe tabu sana.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, naomba na mimi niendelee kwanza kabisa kumpongeza sana Mhe. Waziri lakini vile vile Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji wa hotuba hii ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kwa kweli, wote kwa pamoja wamejitahidi sana katika kuyaona yale ambayo yanahitajika katika nchi yetu. Lakini vile vile mimi niseme tu kwamba, hotuba hii ya Mwelekeo na Mpango huu wa Bajeti kwa Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, naiunga mkono sana kwa kiwango kikubwa na niseme niipongeze katika jitihada hizo.

Lakini Mhe. Spika, naomba nianze moja kwa moja, mimi nitatumia kwamba Mhe. Rais juzi alivyokuwa na hotuba yake hapa ndani tulivyokuwa tukijadili kila mmoja wetu aliipongeza sana. Lakini vile vile wakati Mheshimiwa alipokuwa akiwasilisha amesema katika *tools* yake ambayo imempelekea katika kuelekea na mpango huu ametumia Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Dira ya Mpango wa Kiuchumi. Vigezo vyengine alivyovitumia ni ahadi mbali mbali ambazo zimeahidiwa na Mhe. Rais. Kwa hivyo, kutokana na hali hiyo mimi nataka niende kwenye vipengele hivyo vya vipaumbele.

Kwanza, nataka niende katika kipengele cha 5 ambacho ni kuendelea na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 135 Unguja na Pemba. Mhe. Spika, ukweli ni kwamba mimi niseme katika mwelekeo huu katika Jimbo la Micheweni fursa tulizokuwanazo nina uhakika kabisa kwamba tunaweza tukapata tukaongeza upatikanaji wa fedha nyingi kwa kuweza kuzitumia fursa hizi. Mpango huu kwa mchango wa asilimia kubwa pia inaweza ikapatikana kwa kupitia Jimbo la Micheweni, pindi kama yale ambayo tumeyasema tunakwenda kuyafanya kama uhalisia ulivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti wa Bajeti alisema kwamba sasa anashauri kwa kamati yake serikali iangalie utaratibu wa kuwawezesha wataalam wa mipango katika kuwajengea uwezo ili kuweza kubuni miradi mizuri au kupanga vizuri ili nchi isiweze kutekeleza

miradi ambayo haina tija sana kwa wananchi wetu. Kwa mfano, leo Micheweni kumekuwa na eneo la uwekezaji kwa muda mrefu sana tokea enzi za Mhe. Rais Dkt. Salmin Amour alikeenda kutamka kule Micheweni kwamba ni eneo huru pamoja na Fumba. Fumba tumeanza utekelezaji lakini kwa ujumla Mhe. Spika, tukiliangalia eneo la Micheweni, ukilinganisha fursa zilizokuwepo Micheweni na Fumba unakuta kwamba Micheweni bado kuna fursa ambazo ziko vizuri zaidi. Kwa maana kwamba, eneo liko kubwa zaidi ambalo halijavamiwa na bado hatujaanza uwekezaji, lakini jitihada za serikali tumeanza kuona kwa sasa hivi tayari wawekezaji kila waliokuwa wanakuja walikuwa wanalalamikia kuhusu miundombinu ya barabara, maji na mambo mengine. Serikali imeelekeza hivyo.

Mhe. Spika, taarifa tuliyokuwa nayo sasa hivi ujenzi wa barabara ulikuwa umeshaanza lakini hivi sasa ninavyokwambia vifaa vile ambavyo vimetumika katika kujenga barabara hiyo vimeshaondolewa na Mhe. Rais alielekeza kwamba barabara au miuondombinu ile ijengwe kwa kipindi cha miezi minne ambao wataalam walitaka kwamba wao wajenge kwa miezi nane. Sasa yeye Mhe. Rais aliagiza ijengwe kwa miezi minne lakini hivi ninavyokwambia vifaa vimeshaondoshwa na ujenzi bado haujakamilika na hatujui kwamba hayo maelekezo au hizi dira tunazozitumia tunakwenda kuzitekeleza kwa wakati gani.

Kwa hiyo, mheshimiwa atakapokuja katika hili pia naomba atusaidie kidogo kuwaelewesha wananchi ni kwa sababu gani ambazo zimepelekea kuondoa hivi na azma hii njema ya kilomita 135 ambazo zinaweza kufungua uchumi wa Micheweni pia ikiwemo basi naamini kwamba tunaweza tukafanya kazi nzuri.

Mhe. Spika, jengine hotuba ya Mhe. Rais ilikuwa inasema kwamba itazipandisha hadhi Hospitali ya Micheweni ya Wilaya ambayo kwa kweli haijafikia ngazi ya wilaya lakini kuitamka tunaitamka ni Hospitali ya Wilaya. Lakini ni pamoja na Bandari ya Shumba Mjini imezungumzwa kwenye hotuba ya Mhe. Rais na ahadi mbali mbali alizozitoa alipofika jimboni wakati wa mkutano wa kampeni wa kuomba kura na wananchi wakaweza kumchagua kwa kura nyingi.

Lakini vile vile, maeneo ya wawekezaji hao ambayo nimeyazungumza, yalizungumzwa kwamba kule kutajengwa viwanda, viwanda ambavyo ukiangalia katika ajira hizi zinazozungumzwa ajira kwa vijana hizi zinaweza zikapatikana kwa kiwango kikubwa pindi maeneo hayo yatafanyiwa kazi kama vile Mhe. Rais alivyoelekeza. Lakini cha kushangaza juzi Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Mhe. Makongoro Nyerere alipofika alielezwa kwamba mpango wa viwanda katika eneo la Micheweni, sasa hivi mpango ule umefanyiwa mabadiliko kidogo na badala yake kunakwenda kufanywa kitu chengine kinyume na kile ambacho wananchi wameelekezwa au wameambiwa na serikali yao kupitia awamu tofauti mpaka Mhe. Rais wa awamu hii.

Kwa hivyo, sasa hivi inavyosemekana sina uhakika kwamba viwanda vitakwenda kujengwa eneo la Mkoani, sasa pale ambapo amesema Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwamba tuwawezeshe kumaliza mipango, wataalam mimi nadhani kwa utaalam huu mdogo. Mhe. Spika, mimi niko na fani ya kilimo lakini nchi hii tunahitaji pia pato letu litokane na uchumi huu au uzalishaji wa mazao ya kilimo na ukweli ni kwamba visiwa vyetu ni vidogo sana na maeneo yetu na *master plan* yetu sijajua imeelekeza katika utaratibu upi. Leo Micheweni ni eneo ambalo liko kame ni ukanda wa maweni hakuna

mazao ya aina yoyote katika eneo lile ambalo limetajwa ni eneo huru. Lakini leo eneo la Mkoani ni eneo ambalo ni *fertile land* lakini vile vile uchumi wetu wa zao la karafuu tunaopata kwa kiwango kikubwa tunapata uzalishaji mzuri kutoka katika maeneo huku ya uzalishaji ambako huko hakuna sehemu za mawe.

Sasa leo inanipa tabu kidogo kwamba eneo lile ambalo halizalishi linaachwa linakwenda kufanywa vitu vyengine, lakini ambalo lina fursa nyingi hata makaazi ya watu huko kuko salama leo tunakwenda kuhamisha mpango huu kwenda kutekeleza mpango wa uanzishwaji wa viwanda katika maeneo tofauti na hayo. Kama hivyo ni sahihi Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri apate muda basi katika mpango huo atembelee Micheweni aje awaeleweshe wananchi nini hasa lengo na dhamira ili aweze kutusaidia kutoa majibu.

Mhe. Spika, lakini vile vile naomba niende moja kwa moja katika kuongeza uzalishaji wa umeme kwa njia ya jua na gesi na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji. Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba kitabu hichi kitatusaidia sana kwa sababu ukitizama Zanzibar tumezungukwa na bahari na katika ukanda huu wa Micheweni bahari kwamba ipo wazi sana na ni sehemu ambayo hata mvua upatikanaji wake umekuwa mgumu sana kwa msimu wa mvua au wa mwaka. Mvua yenye uhakika ni mvua za masika pekee hizo nyengine ni za kubahatisha na hata uzalishaji wetu kwenye masuala ya kilimo umekuwa mgumu kutokana na hali kama hiyo ambayo nimeieleza.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba kulikuwa na majaribio yalikuwa yakifanyika katika eneo lile karibu na Rasi Kiuyu kwa ajili ya kuangalia matokeo ya utafiti sijajua yanaelezaje. Kwa hivyo, pia katika hili kama litafanyika vizuri ni imani yangu kwamba nchi hii tunaweza tukaisaidia kuweza kupata nishati nyengine mbadala ukiachana na ya *ZECO* na nyenginezo.

Lakini vile vile Mhe. Spika, naomba niende katika kuimarisha Sekta ya Uchumi katika Uchumi wa Buluu vikiwemo viwanda vidogo vidogo na vya kati, vikiwemo vya usarifu wa mwani pamoja na shughuli za uvuvi wa bahari kuu na ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki. Mhe. Spika, niseme tu kwamba ufugaji wa samaki mimi sipingani nao ni mzuri sana lakini nilikuwa najiuliza hapa tumekwenda *deep* zaidi kwamba leo sisi tumezungukwa na bahari ni vijiji vichache sana ambavyo havipo chini ya bahari au ni maeneo machache sana. Wale ambao tunafanya kazi za uvuvi sisi takriban sio kazi rahisi aliyekuwa mvuvi ukamwambie atoke baharini aje kwenye nchi kavu kwa ajili ya kwenda kuanza. Kwa hivyo, badala ya uvuvi wanaweza wakaita ni shughuli za kivivu kwa upande wa baharini. Sasa nilikuwa nashauri kwamba mimi nadhani tungetoa kipaumbele zaidi katika masuala ya kuimarisha kutoa taaluma kwa wavuvi wetu angalau kufanya zile hifadhi ndogo ndogo katika maeneo hayo ya bahari. Kwa sababu kwa *nature* ya samaki pindi ikiwa kuna sehemu ambayo hakuna harakati za mara kwa mara za uvuvi, *totally* ni kwamba samaki wanakimbilia katika maeneo yale na kwenda kuzaliana kwa wingi na katika kipindi kifupi unaweza ukakuta kwamba kiwango cha samaki kimeongezeka kikubwa mno.

Sasa mimi nadhani shida iliyokuwepo kwa kukimbia samaki kwenda kina kirefu cha maji ni kutokana na kwamba bahari imeweza kuajiri watu wengi ambao takriban wavuvi hao wote ni maskini hawawezi kwenda mbali, badala yake wote wanakwenda

kusokotana katika eneo dogo la kuvua hatimae unaona kwamba kuna uadimikaji mkubwa wa upatikanaji wa samaki katika maeneo hayo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi kwangu katika Jimbo la Micheweni pindi tukiimarisha Sekta ya Uvuvi kwa kuwatafutia vifaa vya kisasa wavuvi wetu wakaenda wakamudu kuweza kuvua mbali na sio kukataza kuvulia miwani pamoja na gesi. Kwa sababu hizo ni dhana ambazo zinaweza zikawasaidia kuweza kuvua zaidi na kwa maarifa zaidi na usalama wa mvuvi mwenyewe. Kwa hiyo, tukifanya hivyo mimi naamini hatuoni hata sasa hivi tokea tulipoanza na dhana hii ya ufugaji wa samaki fedha nyingi za serikali tunaendeleza kuziumiza. Lakini ukiangalia je, samaki ambao tumezalisha kwa kufuga wamewezaje kwenye soko tunahesabu wameongeza mchango gani katika kuona kwamba wananufaisha wao wavuvi wenyewe au wafugaji wenyewe na nchi kwa ujumla au hata kwenye mtaa husika.

Mhe. Spika, kwa kumalizia najua tayari kuna *alert* imeshaanza kuja naomba univumilie kidogo. Lakini pamoja na hayo, tumeona umetajwa huku ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi Chuo Kikuu cha Taifa. Mheshimiwa sipingani na jitihada hizi lakini ningeomba sana Chuo cha Kiislamu ni chuo ambacho kimekutanisha wanafunzi wa majimboni takriban yote ya Pemba na chuo hiki kinategemewa sana. Mheshimiwa chuo kipo hali mbaya, watoto, vijana wetu pamoja na *performance* tunayoisikia kwamba wanapasisha kwa wingi lakini nataka nikwambie watakaopata bahati waende wakaitizame hali halisi ilivyo. Watoto wanaishi katika mazingira magumu, maeneo ya Micheweni kwenyewe ni kugumu, licha ya hivyo mimi natumia fursa hii kuupongeza sana uongozi wa Chuo cha Kiislamu Micheweni wanafanya jitihada kubwa hususan za malezi na uzalendo wa hali ya juu. Lakini Mhe. Spika, hata pa kukaa wanafunzi kuna *over crowd* nyingi au kubwa jambo ambalo tunaweza tukapelekea kupata matatizo mengine.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wangu ni mfupi na umeshamalizika naomba niunge mkono Hotuba hii ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Mpango wa Maendeleo wa Bajeti ya Mwaka 2021-2022-2023-2024. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mheshimiwa, waheshimiwa naomba sasa nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali na kama muda utaruhusu nitamwita Mhe. Shaib Hassan Kaduara.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji ya Hotuba hii ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo ya Bajeti ya Mwaka 2021-2022-2023-2024. Mhe. Spika, mimi niombe kwa Mhe. Waziri kabla ya kumpongeza kwa kutuwasilishia hotuba hii, hii Hotuba ya Bajeti na bajeti hii na mipango hii tunayoipanga isiwe lile pambo la jeneza, tukalikuta jeneza limepambwa vizuri lakini ukaambiwa ingia ukawa unaogopa kwa sababu mle ndani aliyekuwemo ni maiti.

Mhe. Spika, nimesema hivyo kwa sababu tunapanga mipango mingi, bajeti lakini mwisho wa siku utekelezaji wake inakuwa jambo lile lile linajirejea bajeti zote za miaka yote. Nampa mfano Mhe. Waziri wa barabara ya Wete - Chake Chake, tangu kipindi cha mwaka 2016 naingia Barazani humu barabara ile inakuja na bajeti, tunaipitishia ndio, ndio, tunaipitisha tunaondoka. Mhe. Spika, wananchi wale wapo katika jimbo langu na Jimbo la Mtambwe mpaka Wete, wengi wao ni maskini, nyumba zao za udongo,

tathmini imeshafanyika. Mhe. Spika, kuna sababu gani ya kwamba hadi leo hata kulipwa wananchi wale, wengine nyumba zinaanguka hawawezi kujenga kwa sababu lile eneo tayari wameshatathminiwa, maeneo ya kujenga hawana pale kwa sababu hawajalipwa wakaenda kujenga maeneo mengine. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anawapa wananchi uzito kwenye suala hili.

Mhe. Spika, naomba sana bajeti ya mara hii kama ambavyo imekuja na tutampitishia Mhe. Waziri. Kama imekusudiwa kutengenezwa barabara ile ya Chake Chake naomba japo fidia kwanza walipwe wale wananchi, wakishalipwa tena baadae akitengeneza, usitengeneze wao watakuwa wameshaondoka. Mhe. Waziri inauma kuona bajeti zote zinakuja barabara ya Wete - Chake Chake inazungumzwa lakini hapafanywi kitu. Namuomba sana Mhe. Waziri kwenye suala hili la kuwalipa fidia wananchi lipewe kipaumbele.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la mahanga ya askari vipaumbele vya serikali. Nashukuru sana na hapa naipongeza sana serikali kuona kwamba askari wetu wanajengewa mazingira yaliyo mazuri. Mhe. Spika, askari hawalali, ni kweli wanapumzika lakini katika kupumzika kwao wanahitaji maeneo yaliyo bora. Serikali iliyopita imejitahidi sana sana. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Dkt, Ali Mohamed Shein amejitahidi sana kwenye suala la kuboresha mahanga hususan Kisiwani Pemba. Ukienda kule Kojani KMKM, ukienda kule Kiuyu Mbuyuni kwa Mhe. Shamata Shaame Khamis KMKM, Kisiwa cha Fundo KMKM wamejengewa, Kisiwa Panza wamejengewa, kule Mkoani Makombeni KMKM wamejengewa.

Tunaomba sana na askari wengine ambao wanahitaji kujengewa mahanga haya na wao wajengewe mahanga ili kuona inakwenda sambamba na wale wenzao. Namuomba sana Mhe. Waziri itakapopatikana fedha hiyo, hata kama itakuwa ni kidogo basi kile kidogo kama vikosi vyetu saba vimekusudiwa kujengewa mahanga, japo kikosi kimoja kijengewe ili kuona tusiende hilo pambo la jeneza.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la vipaumbele Taasisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Bila ya elimu hatuwezi kuwa na maendeleo. Mhe. Waziri hapa asubuhi ametujibu kuhusu suala la upatikanaji wa elimu na ubora wa elimu hususan kwa wanafunzi kufanya vizuri.

Mhe. Spika, pale Pemba Madungu skuli ile aliyoisema Mhe. Waziri asubuhi kwamba watoto waende pale kusoma baadae warudi majumbani kwao. Hivi kweli Mhe. Spika, umtoe mtoto Kisiwa Panza aende akasome Madungu baadae arudi nyumbani. Itakuwa pana elimu gani itakayopatikana. Kwa hiyo, naomba sana bajeti hii inayokuja izingatie zile taasisi zote ambazo zimekusudiwa kutekeleza miradi ya kimaendeleo, iweze kutekelezwa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye suala la mabwawa ya samaki imo katika vipaumbele. Naomba sana suala hili la mabwawa ya samaki kwenye uchumi huu wa buluu, tusije tukageuka tukawa kama *MACEMP*, kama wapo watakaokumbuka kipindi cha *MACEMP* zimetumika fedha nyingi sana kwa miradi ile ya *MACEMP*, lakini leo ukienda kuwaangalia wale waliofadhiliwa na miradi ile ya *MACEMP* wamerudi zero, wamekuwa maskini wa kutupwa. Wamepewa nyavu ya kwenda kuvua, yaani nyavu za jarufe lakini ukiangalia huyo aliyepewa hajui hata hivyo kuvua yenyewe avue

vipi. Anakwenda kupewa mtu nyavu ya kwenda kuvua, yeye si mvuvi, atajuaje. Mwisho wa siku mambo yale yote yamefutika, fedha nyingi ya serikali imepotea wala hakuna faida iliyopatikana pale.

Kwa hivyo, naomba sana kwenye mabwawa haya ya samaki, isije tena tukaangaliana kwenye sura kwamba na fulani, Mhe. Yussuf Hassan Iddi anakaa Fuoni akenda akaambiwa akaweke bwawa la samaki hajui hata kufuga samaki. Naomba sana wale walengwa wanaoweza kufuga hawa samaki waweze kujengewa haya mabwawa ya kisasa, wapewe taaluma wapewe uwezo wa kifedha ili waweze kujiendeleza. Isije ikawa tena tunasaidiana kwa sababu na mimi Jimbo langu la Magomeni nipate, ikawa mtu wa Magomeni hajui hata hivyo samaki anavyofugwa, akenda kumwambia mtu afuge samaki. Mhe. Waziri hapo hatutokuja kukubaliana. Tunaomba sana fedha hizi za serikali ziende kwa wale walengwa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende moja kwa moja kwenye masuala ya kuwasaidia vijana kuwawezesha kiuchumi. Mhe. Bakar Hamad Bakar alizungumza hapa, ukasema haina haja ya kufufua makaburi, kipindi kile cha pili pili tulimshika kweli Mhe. Amina Salum Ali na Mhe. Hassan Khamis Hafidh kuhusu masuala yale ya pili pili. Hatutaki tuzungumze tena hayo ya pili pili ndio yameshapita kwa sababu kama imewasha ndio imeshawasha, ndio yameshapita yale pale.

Mhe. Spika, tunalolizungumza ili kuwawezesha vijana basi vijana wale ambao wamekusudiwa kuwezeshwa kiuchumi wapewe taaluma vipi watalifikia soko, vipi watatunza fedha hizi. Yaani Mhe. Spika, unapomuwezesha mtu, umekusudia kumwezesha umwezeshe kweli, umpe mtaji, umwewezeshe kiuwezo kitaaluma ili aweze kufikia katika hizo biashara zake. Lakini ikiwa tutaimba tu nyimbo kuwawezesha vijana, kuwawezesha vijana, itafika mpaka 2045, itakuwa hao vijana wenyewe wameshakonga halafu tena nyimbo ya taifa itakuwa ndio hiyo.

Mhe. Spika, naomba niunge mkono hoja asilimia mia kwa mia. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri tunapokwenda kwenye fedha, tuhakikishe kwamba fedha tunazisimamia vizuri. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali, sasa naomba nimpe mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo, Mhe. Shaib Hassan Kaduara.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kuichangia hoja ya Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza muda mimi nitakwenda kwenye vipaumbele ukurasa wa 23. Tunaishukuru sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kupitia kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi Mhe. Waziri kapita mle mle na hii nimpe pongezi sana.

Mhe. Spika, ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba tunapongeza sana kipaumbele hichi. Bandari ya Mkoani tunapongeza sana serikali. Bandari mpya ya Mkumbuu makofi sana kwa serikali yetu.

Mhe. Spika, kuendelezwa Hospitali ya Wete na kuongezewa hadhi, hii kwa ndugu zetu wa Kaskazini itawasaidia sana. Napenda tuipongeze sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Chama cha Mapinduzi kwa ilani hii.

Mhe. Spika, kipekee naomba sasa kwenye kipaumbele nimwambie Mhe. Waziri kuwa kipaumbele cha barabara ya Wete – Chake Chake na wakati Mkoani tunataka kujenga bandari. Ni bora basi kwa nia njema kabisa ikaanzwa Barabara ya Mkoani – Chake Chake kule kuna lango kuu la uchumi. Kwa nini nisiseme kwamba ya Wete ijengwe tena nina imani kubwa sana kama kilomita 135 ya Wete itakuwemo, lakini sasa ikianzwa ya Mkoani, kuna shida ambayo hawa wa Wete vile vile inawapata kwa usafiri wa Mkoani - Bandarini.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ikianzwa ya Mkoani - Chake Chake itatusaidia sana kwa sababu Wete watapita njia mpya. Pale njia kongwe mle kwenye matatizo mrekebishwe kidogo, wakati na wao wanasubiri kwamba baada ya kumalizika ya Mkoani ije ya Wete. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana suala hili la kipaumbele, badala ya Wete aanze ya Mkoani – Chake Chake.

Mhe. Spika, nije sasa kwenye ukusanyaji shilingi zilizotengwa 16.2 bilioni kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa hizi pesa ni kidogo kukusanywa kwa wao. Mimi naomba nitoe ushauri kwenye hili, ushauri wangu tayari kuna mifumo mizuri ya ukusanyaji, sasa ndugu zetu hawa waende wakajitume sana kwenda kusimamia yale ambayo yamo ndani ya sheria. Kwenye upangishaji wa maeneo tofauti, uuzaji na ununuzi huko mitaani, hivi vitu vinafanyika serikali inakosa mapato na wao hawaendi kusimamia.

Vile vile, kuna ujenzi ambao unajengwa wao vile vile hawapiti. Kuna kamati hii ya *DCU* mimi naipenda sana na ninaiamini sana lakini inakuwa bado haijawa na meno kwenda kule chini. Wenzetu wa Serikali za Mitaa wakishalipwa tu, wakitoa kibali wakishalipwa maeneo mengine hawaendi. Kwa hivyo, mambo mawili, kwanza miji inaharibika, lakini la pili vile vile kuna wengine wanaojenga huko mitaani wanakuwa hawawaoni. Kwa hivyo, mimi ningeomba na nashauri sana hili wenzetu washuke huko.

Mhe. Spika, suala la elimu kwa kweli ukurasa wa 15 kwenye ushauri ningeshauri sana wizara hii kule chini sasa wawasaidie sana kuna watu watakuja kukosa ndoa. Mitaala yao inawa-*keep busy* mpaka wanakosa kuhudumia majumbani waajiriwa wao wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Hebu sasa waangalie vizuri na ikibidi kwamba ule mtaala ndio uko vile basi walimu wetu waongezewe posho au mshahara ili wakafanye kazi hiyo kwa ufanisi zaidi na kule nyumbani basi watafute mtu wa kuwasaidia kazi. Lakini vyenginevyo kwa mitaala ile hususan msingi, ndugu zetu walimu wanaumia sana. Tunawaheshimu sana ni walimu wetu waliotufunza na sisi tulitokea huko chini tukasomeshwa na walimu wale. Kwa hiyo, lazima tutumie mdomo huu na wao tuwasemee sasa. Naiomba wizara husika ilisimamie suala hili.

Mhe. Spika, vile vile, katika vipaumbele kuna suala la dakhalia. Kuna ujenzi wa dakhalia Pemba ningeomba sana awamu iliyopita ilijenga skuli za sekondari nzuri na tunaipongeza sana serikali ya awamu iliyopita kwa ujenzi wa skuli zile za sekondari. Lakini sasa kwa Chake Chake dakhalia iliyokuwepo ni moja, iko katika Skuli ya Fidel Castro na hapo watoto wanalala misikitini kwa sababu imeshakuwa haitoshi kwa upande wao ile dakhalia ya Fidel Castro. Kwa hiyo, kipekee ningeomba serikali watujengee

dakhalia Chake Chake ikiwa ni *centre* pale kuna skuli nyingi za sekondari, serikali waamue tu wajenge ile dakhalia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ujenzi wa machinjio *Alhamdulillah* watu wa Chake Chake sisi tuna chinjio jipya lakini sasa ni shida halifikiki, barabara ni mbovu ambapo unalifika kwa urahisi panahitaji daraja, daraja la tinga tinga. Ningeomba sana serikali chini ya miguu watujengee lile daraja la tinga tinga, lina faida kuu mbili. Kwanza tutakata karibu kilomita tatu kuipata ile barabara kuu kwenda Wesha. Lakini la pili, pale wote ambao wanahitaji kufanyiwa shughuli zile za uchinjaji hawatochinja tena pembeni ya majumba yetu, watakwenda kuchinja pale kwa sababu kule ni shida kufikika. Ningeiomba serikali kupitia wizara inayohusika basi walisikilize na hili ili waweze kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, uendelezaji wa miji, Mji wa Chake Chake kwa Pemba yetu ndio Mji Mkuu na ndio *centre* ya shughuli za serikali kibiashara. Ningeomba sana serikali katika bajeti hii katika hizo *real estate* ambazo wanataka kujenga, kuna eneo mimi naanza kuwaelekeza waende hapo kwa sababu hilo eneo limeshapimwa. Kuna viwanja kumi na moja elfu vimepimwa maeneo ya Mgogoni.

Vile vile kuna eneo la Kopole Mpendae waende basi pale wakatujengee, pazuri, pana mandhari nzuri ya bahari na penyewe wananchi wake hawana shida yoyote iwapo watafanyiwa malipo yao vizuri. Watu wa Mpendae ni watu wema, hawana matatizo, wanapenda mashirikiano na serikali yao. Kwa hiyo, Mpendae Pemba. *(Vicheko)*

Mhe. Spika, Mhe. Shaaban Ali Othman hapa alishavimba kichwa kwa sababu nimemtajia Mpendae. Lakini Mpendae ya Kopole Pemba. Mhe. Spika, kwenye uendelezaji wa hii miji midogo midogo ningeomba sana Mji wa Chake Chake unahitaji kuendelezwa, Mji wa Chake Chake una mandhari nzuri, kuna mabonde kuna usawa. Kwa hiyo, ni mandhari nzuri sana ya kuweka mji wa kisasa katika uendelezaji wake.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, ningeomba basi kama bado serikali itakuwa moja kwa moja haijaamua kwenda kuuendeleza Mji wa Chake Chake watusaidie hata zile barabara za kuunganisha ule mji. Kwenye Jimbo la Chake Chake kuna sehemu ndani ya mji lakini hamfikiki. Kwa hiyo, ningeomba sana serikali wangetutengenezea barabara yetu ile pale ya Mpendae katika Mji wa Chake Chake, wangetutengenezea barabara yetu ile pale ya Ngoma hazingwa, wakaja wakaunganisha na barabara ya Misooni hapa. Misooni watakuwa hawachezei tena bahari kuvuka, wanapita barabara nzuri na hili wataendelea kupata matunda ya Mapinduzi yao matukufu.

Mhe. Spika, baada ya hapo, nikushukuru wewe, namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar. Lakini vile vile sitomsahau Mwenyekiti wangu mstaafu wa vijana, Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango ndugu yangu Jamal Kassim Ali. Ahsante sana mheshimiwa naunga mkono hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Shaib Hassan Kaduara. Waheshimiwa Wajumbe muda tulionao hautoshi kumpa mchangiaji anayefuata. Lakini naomba niwataje wachangiaji watatu watakaoanza jioni tukijaaliwa ili waweze kujiandaa kufika hapa mapema. Wa mwanzo atakuwa Mhe. Omar Said Shaaban ambaye atafuatiwa na Mhe. Juma Makungu Juma na pia ajiandae Mhe. Shadya Mohamed Suleiman. Baada ya tangazo hilo,

waheshimiwa naomba kusitisha shughuli za Baraza hadi saa 11:00 za alaasiri. Ahsanteni.

(*Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na sasa naomba nimwite Mhe. Omar Said Shaaban, atafuatiwa na Mhe. Juma Makungu Juma na Mhe. Shadya Mohamed Suleiman ajiandaye.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kupata fursa jioni hii kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri juu ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo pamoja na Bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kama wengine nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutekeleza wajibu wake kisheria na kikatiba kuleta mpango huu katika Baraza hili tukufu, ili uweze kupata michango ya Waheshimiwa Wajumbe kwa ajili ya kuboresha na kwa ajili ya kuutanua wigo zaidi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimepata fursa na mimi ya kusoma wote na kwa ujumla ni mpango mzuri ambao kama utatekelezwa na upatikanaji wa fedha utakuwa kama unavyotarajiwa, basi bila ya shaka unaweza ukatutoa nchi yetu hapa tulipo na kusogea mbele. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo mipango mingine yoyote ile inahitaji kuchangiwa na kutolewa maoni ili iweze kuboreka zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nitajikita kwenye maeneo kadhaa ambayo mingine yameshazungumza nitaacha lakini yapo mambo ambayo ninaamini kama serikali itayatupia jicho basi mipango hii itatekelezeka na itawezekana kutekelezeka kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, eneo moja ambalo ni vipaumbele alivyosoma Mhe. Waziri ni eneo la utawala bora na katika hili Mhe. Mwenyekiti, nimesoma lakini sijaona serikali ina mpango gani wa hasa kuboresha na kuimarisha Mahakama ya Biashara. Mhe. Mwenyekiti, ili kujenga imani ya wawezaji ambao tunawataka waje ni lazima tuwe na vyombo kama Mahakama ya Biashara ambapo wawekezaji wana uhakika pale ambapo panatokea migogoro yoyote ile ya kibiashara, basi masuala au migogoro hiyo haiwi kikwazo katika utekelezaji wa mipango yao ya uwekezaji na biashara zao. Tusipokuwa na Mahakama ya Biashara imara na Mhe. Mwenyekiti, kwa hili lazima ni-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Mahakama ya Biashara.

Mahakama hii pamoja na kuanzishwa kwa sheria lakini ni kama vile imetelekezwa, kwa sababu haijawezeshwa kuweza kufanyakazi zake kwa ufanisi. Kwa hiyo, niombe serikali katika mipango yake iitupie jicho mahakama hii kwa sababu uwepo wa mahakama hii

utajenga sana imani ya wafanyabiashara, imani ya wawekezaji na kuona kwamba mambo yanapoharibika yanauwezo wa kutatuliwa hapa hapa.

Katika hili hili Mhe. Mwenyekiti, niongezee lazima serikali sasa ije na mabadiliko ya sheria na utungaji wa sheria mpya katika ku-*focus* kuanzisha mifumo ya ushuluhishi wa migogoro mbadala wanaita *alternative dispute resolution*, nimemsikia Mhe. Mwanasheria Mkuu aliwahi kulizungumza *at one point*. Lakini nasema kwamba bila ya kuwepo kwa *alternative mechanism* za kutatua migogoro ikawa kila mgogoro tunapeleka mahakamani ni wazi kabisa utakwamishwa uwekezaji na ukikwamisha uwekezaji utakwamisha maendeleo na hata hayo mapato ambayo tunayarajia hayataweza kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili hili eneo jengine la mazingira ya uwekezaji nimesoma mpango lakini sijaona mkakati mahususi wa serikali kuhakikisha kwamba urasimu katika upatikanaji wa mikataba ya ardhi *lease* unaondolewa, yaani kwa maana unarahisishwa sasa. Mhe. Mwenyekiti, uzoefu unaoenesha na sisi wengine ambao tumekuwa tukifanya mambo haya kwa muda mrefu ni kwamba, wawekezaji katika kitu ambacho kinawakimbiza hapa kwetu ni urasimu mrefu wa kupata *land lease* unaaza katika uhaulishaji wa ardhi, lakini pia katika kupata saini ya waziri katika kuipata hiyo *lease* yenyewe. Kwa hiyo, nimeona kuna jambo limezungumzwa la uhaulishaji wa *land bank* nafikiri hili litasaidia sana katika kuhakikisha kwamba changamoto hii inaondolewa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulichangia ni kuitizama upya katika mpango mahususi kabisa *ZIPA* Rais ameizungumza Mhe. Waziri ameizungumza na wadau wameizungumza. *ZIPA* inahitaji *over holly* kwa maana ya kuwawezesha watendaji. *Over holly* kwa maana ya kuhakikisha kwamba kwanza wanafahamu uwekezaji na kwa kuweka watendaji, lakini pili inarahisha inakuwa inaleta ile maana halisi ya kuitwa Mamlaka ya uwekezaji. *ZIPA* inatoza kile wanachokiita *service fee* kwa wawekezaji.

Lakini wakezaji wengi wanalalamika wanasema ni vyema mambo wakawa wanayafanya nje ya *ZIPA* yanakwenda urahisi zaidi kuliko yakifanywa kupitia *ZIPA* yanakwama sana. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, niiombe serikali itupie sana *ZIPA* na katika mipango yake hii ya miaka mitano basi ihakikishe kwamba ina *over holly ZIPA*.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni suala la elimu, elimu nimeona mpango lakini sijaona uki-*emphasize* sana kwenye *technical education* au *technical skills*. Mhe. Mwenyekiti, kama tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda kama tunakwenda kwenye uchumi wa mafuta hakuna namna ambavyo watu wetu watanufaika ikiwa wote utawasomesha masomo ya sanaa. Kama tunataka kweli watu wetu wawe- *key layers* kwenye sekta hizo basi tuekeleze sana kwenye vyuo vya ufundi tuhakikishe kwamba watu wetu wana *technical skills* za kuweza kuajiriwa kwenye sekta hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la miundombinu hasa ya usafirishaji wengi tumekuwa tukisema na tumeona maendeleo na umalizaji wa jengo jipya la *Airport*. Yote inasema kwamba katika kuhakikisha kwamba tunapata watalii wengi zaidi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunawezaje kupata watalii wengi zaidi na kuwa *assurance* ikiwa hatuna *airline* yetu wenyewe na hili wala hatuhitaji kwa sababu sio jambo la Muungano tunaweza kwa kushirikiana katika dhana ile ile ya *PPP* kwa kushirikiana na wawekezaji

tukaanzisha *airline* yetu. Utafikiti unaonesha kwamba asilimia arubaini ya matumizi ya mtalii yanakwenda kwenye tiketi.

Sasa kama tunakuwa na *airline* yetu wenyewe na kwa kushirikiana na wawekezaji wengine sasa tuna *airport* tunajenga na *airport* nyengine Pemba muda sasa wa kuanza kutafakari kuwa na Zanzibar *airline* ambayo itawachukwa watalii popote walipo kuwaleta Zanzibar moja kwa moja. Bila ya hivyo, asilimia arubaini au kila shilingi mia ya mtalii shilingi arubaini tutakuwa tunapeleka kwenye mashika ya ndege.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nimemaliza. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Omar Said Shaaban kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Juma Makungu Juma atafuatiwa na Mhe. Shadya Mohamed Suleiman na Mhe. Maryam Thani Juma ajiandae.

**Mhe. Juma Makungu Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi.

Lakini awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *"Subhana huu Wataala"* alieendelea kuturuzuku uhai na uzima kwa kuweza kuendelea na majukumu yetu kama ambayo tulivyojipangia.

Kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri Afisi ya Rais Fedha na Mipango kwa namna ya uandaaji lakini pia na uwasilishaji ambao katuwasilishia leo.

Mhe. Mwenyekiti, sitokuwa na mengi lakini hayo machache naomba nianze na ukurasa wa 3. Ukurusa wa 3 kuna mahala pameandikwa hatua nyengine zilizotumika katika kuimarisha mapato ya serikali na kusaidia kurahisha za kibiashara ni pamoja naa zikaorodheshwa hapa shughuli sita. Lakini moja sikuiona ambayo mimi ningeshauri ni vyema ingekuwepo ambayo ni hawa wafanyabishara wa magari. Kwa sasa wenzetu wanatakiwa kulipa asilimia arubaini ya bei halisi ya ununuzi wa gari hiyo huko walikoinunua, wakati hapa katika i(2) kunasema:

"Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT* kwa vifaa vya uvuvi ikiwemo boti kubwa za kuanzia urefu wa mita kumi na nane na zaidi, mashine za boti pamoja na vifaa vyengine vya uvuvi vinavyoingia nchini".

Kutokana na hali hiyo, nashauri kwa sababu haya tumeona yamechangia sana uchumi wetu. Ushauri wangu pia na wafanyabiashara baada ya kuwatoza asilimia arubaini ya tozo tungepunguza tungefikiria namna ya kupunguza *atleast* asilimia thalathini kwa sababu wafanyabiashara wakaweza kufanya biashara kwa wingi na serikali ikapata hizi asilimia thalathini mara nyingi kuliko arubaini chache, kufanya hivyo inawezekana uchumi wetu ukazidi kukua.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 25 katika muelekeo wa matumizi kumeoneshwa hapa mwaka 2021/2022 kunategemewa kutumia trilioni moja milioni mia tano na sita nukta mbili halkadhalika 2022/2023 trilioni moja bilioni mia saba tisini na moja nukta sifuri na 2023/2024 ni trilioni moja bilioni mia tisa na arubaini na nane nukta mbili. Hapa ukilinganisha mwaka wa fedha wa 2021/2022 fedha zake ni kidogo kuliko

mwaka wa fedha ambao tunaenda nao huu ambao ni trilioni moja bilioni mia tano sabini na tisa nukta mbili.

Ukitizama tuko nyuma kwa takribani bilioni sabini na tatu. Sasa suala langu limekuja hivi kwa nini wakati 2021/2022 zimekuwa kidogo kuliko 2022/2023 zimekuwa kidogo kuliko 2023/2024. Lakini 2020/2021 zimekuwa nyingi kuliko 2021/2022 inawezekana ikasemwa ni *Corona* lakini huko mbele pia hatujajua inakuwaje lakini mpango wake ninaoenekana fedha kukuwa kila siku na tafauti mwaka huu ambao tunaenda nao ni mkubwa kuliko mwaka ujao kwa namna ambavyo imewasilishwa hapa.

Sasa ninpepata jawabu kwa nini 2021/2022 fedha zake zikawa kidogo za makadirio ukilinganisha na mwaka ambao tunaenda hivi sasa. Nimeuliza swala hili zaidi kwa sababu ya ukurasa wa 13 Mhe. Mwenyekiti, kabla ya *paragraph* ya mwisho kuna sehemu imeandikwa matarajio haya kukusanywa jumla ya Tanzania shilingi milioni mia saba sitini na tisa nukta saba bilioni ifikapo Juni 2021 ni kutokana na mikakati iliyowekwa na serikali juu ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya serikali ni kama ifuatavyo, zikawekwa njia hapa tatu njia hizi mimi zimenifurahisha sana na ndio maana suala langu nikali *pause* kwa nini sasa mwaka ujao fedha ziwe kidogo kuliko mwaka wa fedha huu ambao tunakwenda nao wakati tayari tunaenda kuanza rasmi matumizi ya mfumo wa utoaji wa risiti za *electronic* ambazo hutoa taarifa juu ya mwenendo wa mauzo halisi ya fanyabiashara ifikapo mwezi wa Machi 2021.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama ukurasa huu huu wa 23 kwenye njia hizi hizi tatu ambazo zimeanishwa ya (b) inasema:

"Taasisi ya kodi yaani *TRA* na *ZRB* kuendelea na zoezi la ukaguzi ili kodi stahiki iweze kulipwa".

Hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo wenzetu wa *TRA* na *ZRB* ambapo ni wakusanyaji wakubwa wa hizi kodi siku wa Jumapili wanapumzika hapa kidogo kuna shida kupumzika ni haki ya binaadamu. Lakini kwa nini tusiweke utaratibu mzuri wa kwamba kila siku wakawepo kazini namna ya kupumzika ikawa kama wenzetu Polisi au Madaktari siku yoyote unaweza ikenda Polisi na ukapata huduma Jumapili, Jumatatu na halkadhalika hospitali siku yoyote unaweza kwenda kupata huduma na hawa kwani ni taasisi muhimu sana basi ingekuwa vyema siku ya Jumamosi na Jumapili wakaendelea kufanyakazi kwa namna ambavyo watajipangia.

Kwa nini nasema hivyo, kwa sababu wenzetu *TRA* wana utaratibu iwapo biashara au bidhaa mwenye mali kashindiwa kutoa kwa muda wanaweka *storage* na wanapoweka *storage* wanachaji mpaka siku ya Jumamosi na Jumapili siku ambazo wao hawapo kikazi. Lakini kichaji wanakuwepo hata ukitamani ukaondoe deni laki kwa siku ile ya Jumapili hupati na hii siku ya Jumatatu haiwi na *excuse* kwamba Jumapili hatukuwepo na ulikuwa unataka kulipa kwa hiyo wacha tuitoe haipo na Serikali hii ya Mapinduzi Zanzibar toka ilioasisiwa kwake kwa Mapinduzi mwaka 1964 awamu zote saba na sasa tuko awamu ya nane imekuwa ikijipambanua kwamba haimuonei mtu na ndivyo ilivyo inatenda haki na usawa.

Kutokana na hali hiyo, nashauri sana serikali kupitia Wizara hii ya Fedha kwamba zile siku za Jumapili ambazo *TRA* hawapo ile *storage* wangeifuta mwananchi wasimchaji

kwa siku ile mbayo hawapo. Lakini la pili ikiwezekana basi pia wafanye kazi siku ya Jumapili kusudi mwananchi akitaka kulipa aweze kulipa bila ya usumbufu na bila ya kusubiri siku ya pili yake Jumatatu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kwenye kipengele cha (c) kwenye ukurasa huu wa 13 kuwa na bei elekezi kwa ajili ya usaminishaji wa bidhaa zinazoingia nchini. Hapa ningepata ufafanuzi kwa baadhi ya mfano wa bidhaa zenyewe ni zipi hizo kwa Mhe. Waziri kusudi tukapata uelewa wa pamoja.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa namna ambavyo kama nilivyotangulia kusema hotuba hii imekaa vizuri ukiachia hayo niliyoyaona na baada ya kupata ufafanuzi bila shaka nitakuwa nimeridhika na naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Juma Makungu Juma kwa mchango wako. Sasa naomba kumwita Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, atafuatiwa na Mhe. Maryam Thani Juma na Mhe. Shaaban Ali Othman ajiandae.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya maendeleo ya Hali ya Uchumi Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2021/2022, 2022/2023, 2023/2024.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa pumzi zake na uhai wake nikweza kusimama laasiri hii nikiwa mzima na mwenye afya.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake ametulia kwa makini unatamani asimalize vile kuisoma hii hotuba Mhe. Mwenyekiti ahsante hongera sana Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anatoa hotuba yakem pale nilikuwa namsikiliza kwa kina sana naomba kwanza nianze mchango wangu huu kwenye ukurasa wa 16. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niweze kusoma kwa ufupi tu kukariri maneno haya ya Mhe. Waziri wakati anaeleza hotuba yake pale mbele.

"Mhe. Spika, ilishauriwa kwamba posho na stahiki za walimu zilipwe sambamba na *voucher* za mishahara, ili kuondoa malalamiko ya kila sikuynayojotokeza kwa walimu wa maandalizi na msingi. Sambamba na hilo maposho ya walimu wa TUTU yatafutiwe utaratibu maalum wa kuingizwa kwenye hesabu zao binafsi". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme kwanza naungana kwa hili kwa sababu kila siku tunasema hakuna kazi nzito kama kazi ya walimu na mara nyingi Mhe. Mwenyekiti, tunawasikia walimu wakilalamika jinsi ya maslahi yao kwa hivyo nisema kwamba na mimi hapa naunga mkono kwa asilimia mia niendelee kusema kwamba kazi ya uwalimu ni kazi ya wito haina malipo isipokuwa wao watalipwa na Mwenyezi Mungu tena nawaomba waendelee kuwafundisha watoto wetu kwa moyo thabiti.

Mhe. Mwenyekiti, napata hofu kidogo hapa kwenye walimu wa tutu Mhe. Waziri, amesema posho unajua ukisika posho kidogo unashtuka. Mhe. Waziri nikwambie hapa kidogo ipo shida kwenye walimu wa TUTU, nazungumzia walimu wa tutu kwenye mkoa wangu hususan katika Wilaya ya Mkoani, wakati walimu hawa wanaelekezwa Mhe. Waziri waliambiwa wenye Baraza la Mji watalipwa na Baraza la Mji wenye Manispaa watalipwa na Manispaa, wenye Halimashauri watalipwa na Halmashauri lakini ninavyokwambia Mhe. Waziri hapana kitu hapa hapana malipo.

Nimesema nazungumzia Wilaya ya Mkoani kuna hawa walimu wa TUTU katika mwaka wamelipwa mara mbili tu na tena fedha wenyewe waliyolipwa ni aibu kuizungumzia hapa kwa hivyo, nikuombe sana mhe. Waziri hapa pana shida lazima pafanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba sasa niende kwenye ukurasa wa 21. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa ushauri serikali yangu kwamba vipaumbele bora tuweke vipaumbele vichache tuweze kutekeleza vile vichache ambavyo tumevianisha kuliko kuainisha vipao mbele chungu nzima siku ya siku tunatenda kile vinge ninakuwa havimalizi. Kwa hivyo, niombe sana serikali yangu tuliangalie hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuipongeza sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na jemedari Dkt. Husein Ali Mwenyi kwa jinsi anavyochapa kazi na sisi tunaendelea kumuombea Mwenyezi Mungu tunaendelea kuiombea nchi yetu ili mapato yaongezeke kwa wingi. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, bila ya fedha haya yote tuliyooredhesha hapa yatakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuipongeza serikali kwa kuendelea kuwa na ujenzi wa kiwanja cha ndege Pemba ni jambo zuri sana tunaendelea kuiombea serikali iweze kutufanyia mambo mazuri ambayo Mhe, Rais alituahidi wakati wa kamapeni zake.

Vile vile, nikiangalia katika vipaumbele, bara bara ya Mkoani Chake Chake siioni, wakati barabara hii Mhe. Rais wakati wa kampeni alizungumzia barabara hii lakini kwenye vipaumbele sioni, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Mkoani ndio kwenye hospitali kubwa Abdalla Mzee mgonjwa anapozidiwa Micheweni, Wete, Chake Chake anapelekwa Mkoani lakini ukiangalia barabara si rafiki kwa matumizi ya mgonjwa tumfikirie mgonjwa yule mpaka afike kule inakuwaje. Lakini kama haitoshi Mhe. Mwenyekiti sasa hivi tumo katika ujenzi wa bandari ya Mkoani na tumesema kwamba tunataka kufanya viwanda vidogo vidogo sasa bila ya kuwa na barabara viwanda hivi vitakuwa vipi.

Kwa hivyo, naiomba serikali yangu katika vipaumbele bandari ya Mkoani imeanishwa hapa lakini Mhe. Mwenyekiti niseme kwamba imeanishwa 2021/2022 - 2023/2024, naiomba sana serikali katika hili bandari ya Mkoani waipe kipaaumbele, ili iwe ya mwanzo katika kutekelezwa ili tuweze kufanikisha yale mema mazuri ya wananchi wetu aliyotuahidi Mhe. Rais wakati wa kampeni yake. Kwa maana hiyo, naamini ikishamaliza bandari ya Mkoani na hivi viwanda vidogo vidogo vikaweza kuwepo, basi ninaamini tatizo la ajira kwa wananchi wetu litapungua kwa asilimia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoanza kusema mwanzo kwamba mchango wangu ni mdogo, baada ya hayo machache na mimi niseme kwamba naionga mkono hutuba hii kwa asilimia mia ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Shadya Mohamed Suleiman kwa mchango wako. Sasa naomba kumwita Mhe. Maryam Thani Juma, atafuatiwa na Mhe. Shaaban Ali Othman na Mhe. Bihindi Hamad Khamis ajiandae.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kitabu hichi cha hutuba ya Muelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo ya Bajeti. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha kwa kutuwasilishia kitabu hichi katika Baraza letu hili leo. Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye vipaumbele vya mwaka 2021/2022, 2022/2023.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenye ukurasa wa 22 kwenye ujenzi wa Hospitali ya Wete kwa kuipandisha hadhi ya Mkoa. Kwa kweli, hili kwanza napenda nipongeze sana kwa sababu muda mrefu tulikuwa tunaambiwa kwamba Hospitali ya Wete itajengwa lakini hatima yake hatuioni, naamini kwamba kwenye mwelekeo huu na vipaumbele hivi imo kwenye mpango na hospitali hii itajengwa. Lakini Mhe. Mwenyekiti tumesema kwamba tunajenga hospitali na baadae tunapandisha hadhi hospitali hii kuwa ya mkoa, mimi nataka niseme kwamba tunaipandisha hadhi hospitali ya Wete kuwa ya mkoa, lakini tukiangalia bado vifaa tiba hatujawa nayvo kwenye hospitali zetu.

Kwa mfano, tukiangalia Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Wete kipindi cha nyumba kilikuwa na matatizo ya *X-ray* matatizo ya *Ultra sound* na matatizo ya vifaa tiba mbali mbali na mengineyo ambayo tulikwa hatuyajui lakini naamini ni tatizo kwa Hospitali ya Wete. Lakini sasa tunajenga na baadae tunapandisha hadhi hospitali hii, lakini tushazingatia hivi vifaa tiba ambavyo vinahitajika kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Mwennyekti, Hospitali ya Abdulla Mzee Mkoani, hospitali ile imepandishwa hadhi lakini mwisho wa siku juzi tu hata mimi mwenyewe nilikuwa na mgonjwa lakini alipofika pale aliambiwa akafanye vipimo Hospitali ya Micheweni na tukiangalia Hospitali ile tayari imeshapandishwa hadhi imekuwa ya Mkoa hatuoni kwamba hili inakuwa ni tatatizo.

Kwa hivyo, tunaomba sana muangalia haya mambo, muanglie kwamba vifaa tiba vinaitajika kuwepo tukipandisha hadhi hizo hospitali basi na hivi visiadimike mara kwa mara nasema Mhe. Mwenyekiti hili ni tatizo ambalo linatokea kwenye hasa Hospitali yetu ya Wete mara *Ultra sound* mbovu mara *X-ray* haifanyikazi mara vifaa nyengine haviko katika hali nzuri, almradi kesi nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile baada ya hivi vifaa tiba tujue kwamba au muzingatie kwamba madawa yanapatikana madaktari wetu wanakuwepo wa kutumia vile vifaa, ambavyo vitakuwepo katika hospitali ile au tnatarajia kuweka pale ambapo tutaopandisha hadhi tukizingatia kwamba hatua hivi vifaa tiba.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la ujenzi wa barabara ya Wete Chake Chake kwa vile suala hili linazungumzwa mara kwa mara Mhe. Mwenyekiti lakini na mimi nataka nigusie kidogo. Tumeona kwamba sasa tunataka kujenga barabara lakini kama alivyosema Mhe. Suleiman Makame Ali pale wananchi bado hawajijua kwamba sisi leo kijumba changu ni kibovu mimi nataka nihame nijenge sehemu nyengine kupisha ujenzi wa barabara, lakini mwisho wa siku ule uwezo hana wakusema mimi naondoka naenda kujenga sehemu kwa kuacha barabara hii inakuja kujengwa, na

ukizingatia tatizo hili ni tatizo kubwa ambalo linatokea sehemu nyingi wakati wa utengenezaji wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanatulalamikia sisi tunaamini huu ujenzi utatunufaisha sisi wananchi ambao tuko katika maeneo lakini mwisho wa siku ujenzi huu unatupa hasara wananchi wanalalamika sana kutokana na kwamba barabara zinatengenezwa, lakini wahusika hawapati haki zao za msingi, wale wahusika ambao tunawatarajia vitu vyao vipigwe tathmini na wapate haki zao basi wanakuwa hawapati haki zao kwa mujibu wa hali halisi ya vile vitu vilivyo.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri kabla utengenezaji wa barabra hii haijaanza mufanye tathmini ya watu amabo hawajalipwa zile fidia walipwe zile fidia zao kwa mujibu wa thamani ya nyumba zao zilivyo na vipando vyao vilivyo ili isije ikatokea athari nasema tena isije ikatokea athari iliyotokea Jimbo la Gando. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha kama unatambua kwamba Jimbo la Gando ilitokezea ujenzi wa barabara ya Wete Gando, lakini mwisho wa siku kuna watu ambao hawa wanastahiki kulipwa fidia wakafanyiwa tathmini nyumba zao lakini mwisho wa siku hadi leo wanadai haki zao hawakulipwa, hili inakuwa ni tatizo kwa sababu wanaitia dosari serikali yetu kila mmoja anaelekezea serikali yangu haikunilipa. Kutokana na hali hiyo, natoa ushauri kwamba na hapo tutakapotengeneza barabara ya Wete Chake hili lisije likatokea, kwa sababu ni tatizo kwa serikali yetu ni tatizo pia kwa wananchi ambao tunawaomba kura inapofika wakati wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la utalii kwa wote Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwamba utalii ndio *key* ya uchumi wetu wa Zanzibar hili jambo ambalo liko wazi. Miongoni mwa kazi kubwa zinazofanywa *tours* ni kuutangaza huu utalii *tours operators* wanautangaza utalii hata kuliko serikali yetu. Lakini tukiangalia kwamba bajeti hii tunaoenda nayo fedha zilizotengwa ni ndogo haziendani kwenye uhalisia wa sekta hii muhimu. Hivyo, naiomba sana serikali kwenye eneo hili la kukuza utalii walibinafsishe katika kuutangaza huu utalii kwenye *tours operators* tulizonazo, lakini pia hizi kamisheni yetu ya utalii wazisimamie hizi *tours operators* na kuona kwamba wanautangaza utalii kwa kiasi kikubwa kama ambavyo inaonekana hivi sasa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kwa siku hizi za baadae Mhe. Mwenyekiti hii mada imenipotea, lakini baada ya hayo naomba sana kuunga mkono hutuba hii asilimia thamanini. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Maryam Thani Juma kwa mchango wako. Sasa naomba kumwita Mhe. Shaaban Ali Othman atafuatiwa Mhe. Bihindi Hamad Khamis na Mhe. Panya Ali Abdalla ajiandae.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshkuru Mwenyezi Mungu, lakini pili nikushkuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi jioni ya leo kuwa sehemu ya wachangiaji wa hutuba hii ya muelekeo wa hali ya uchumi mpango wa maendeleo na bajeti kwa mwaka huu ulioanishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba wa hutuba hii ya leo naanza kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wa Mhe. Jamal Kassim Ali Waziri wa Fedha na Mipango, lakini pili nimpongeze yeye mwenyewe binafsi Mhe. Waziri kwa uandaaji na uwasilishaji wa hutuba ambayo kimsingi niungane na kaka yangu Mhe. Omar Said Shaaban kwa kunukuu maneneo yake kwamba ikiwa haya yaliyoandikwa, fedha zilizotajwa zikikusanywa na zikiilekezwa katika maeneo husika basi malengo ya serikali na mimi naungana nae kwa kusema yatatimia kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitajikita zaidi katika ukurasa wa 22 na 23 wa hutuba hii na nianze katika kipengele hichi cha tano cha kuimarisha utawala bora. Napongeza sana Mhe. Waziri amelezea kwa kina lakini kwa hisani yangu katika kipengele hichi Mhe. Nataka niweke msisitizo sana yote yaloelezwa katika kitabu hichi msingi wake uko hapa. Suala la utawala bora Mhe. Rais kwa nyakati tofauti amekuwa akipigia kelele baadhi ya vitendo vya udhalilishaji, rushwa, ubadhirifu, na mambo mengine yanaofanana na hayo. Sasa tunapokwenda kwenye uchumi mkubwa matumaini yangu eneo hili likimarishwa vizuri basi fedha za serikali zinazoelekezwa huko zitatumika kwa nidhamu na heshima lakini nchi yetu itatawalika katika misingi ya busara hekama na utamaduli ule tuliozoea wa Wanzanzibari.

Sasa katika hili naomba sana Mhe. Waziri muweke mkazo mkubwa sana katika kuvijengea uwezo vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi yetu ikiwemo Jeshi la Polisi lakini kuijengea uwezo mkubwa mamlaka yetu ya kupambana na kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar *ZAECA* sambamba na kuijenga uwezo wa kitaalamu na umahiri mkubwa mahakama zetu zote ikiwemo, na uwepo pia uwanzishwaji wa Mahakama ambayo Mhe. Omar Said Shaaban ameileza kwa manufaa ya uchumi wa Zanzibar Mahkama ya kibiashara. Lakini pia ofisi ya Mwanasheiria Mkuu wa Serikali tunakwenda kwenye *contract* kubwa ambazo zina *interest* na nchi kwa hivyo lazima kuijengea uwezo ofisi hii nimekuwa nikipiga kelele sana na leo naisema kwamba ina umuhimu wake mkubwa sana.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie kwa sababu imezunguzwa kwa mnasaba wa hii hutuba na waziri aliyeko mbele manake ni Waziri wa Fedha, nataka nizungumzie kipengele hichi cha *Diaspora* ambao hata wezetu wa kamati wamejaribu kukishauri ama kuishauri serikali. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe watakubaliana na mimi kwamba Mhe. Rais amefanya na anaendelea kufanya jitihada kubwa za kuwasogeza karibu ndugu zetu wa Zanzibar ambao wako nje nchi kwa maana *Diaspora* na lengo kubwa ni kujaribu kuona mchango wao wa ku *boost* uchumi wa nchi yetu.

Sasa katika eneo hili ushauri wangu tunmekuwa kama nchi bado hatuna mfumo ulioimara na thabiti wa kuweza kukusanya kodi kupitia fedha zinazptumwa na ndugu zetu wa *Diaspora* kuja kwa ndugu zao nchini. Mhe. Mwenyekiti, katika hili niombe serikali iandae utaratibu na *right track* ambayo itawezdesha kuzitambua ni kiasi gani zinaingia na namna ya kutoa kadi yake ili pato la serikali ama uchumi wa nchi yetu uimarike pian kupitia ndugu zetu hawa. Lakini sambamba na hilo nilishawahi kupendeleza na leo napendekeza tena kuimarishwe basi kwa kitengo cha utafiti chini ya idara hii *Diaspora* ili kuweza kuwabaini ndugu zetu ambao wako nje ya nchi na wamesambaa duniani kote.

Mhe. Mwenyekiti, utakubaliana na mimi wajumbe wataniunga mkono katika hili Zanzibar ina hazina kubwa ya wazanzibari ambao wamesambaa kote duniani, na ukijaribu kufanya tathmini kubwa walioko huku wako matajiri wakubwa ambao wanazisaidia nchi wanazoishi katika kukuza chumi zao. Sasa eneo bado hatujalifanyia tafiti ya kutosha, tunao *Diaspora* na tamasha lililopita nafikiri walifika 300. Lakini lengo sio kuwa na namba kubwa ya *Diaspora*, lengo ni kuwa na *Diaspora* ambao wanaweza ku-*boost* uchumi wetu hasa uchumi wa sasa uchumi wa buluu.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali katika eneo hili ifanye tafiti na tathmini ya kutosha kuwatambua watu hawa ambao ni *very potential* kuja kuisaidia nchi yetu katika eneo hilo.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la uwekezaji limezungumzwa hapa katika kipengele hiki cha 7(iv)(b) ujenzi wa makaazi ya wananchi *real estate*.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa *real estate* kwa kwetu hapa naona upo, tunasema ni zile *strategic investment* ambazo wenzetu wa *up town living* wamefanya Bakharesa, lakini wenzetu wa *CPS* nao wamefanya na ipo miradi mingine. Lakini nilichokuwa nataka nikiseme Mhe. Mwenyekiti, wawekezaji hawa wanapoanzisha hizi *real estate* fedha nyingi sana wanakuwa wameiweka ardhini, mwisho wa siku wanatamani kukiona kile wanachokizalisha waweze kukiuza ili faida na pato la serikali liingie. Lakini ukienda mbali zaidi wawekezaji hawa wamekuwa wamekumbwa na changamoto kubwa sana ya kuomba baadhi ya *incentives* ambazo mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa nyumba zao wangetamani waziuze, lakini wanaonunua sasa wanatamani kuwa na uhakika angalau basi wa makaazi ya pale eneo ambapo wamenunua.

Kwa hivyo, niiombe sana serikali kwenye hili suala la *resident permit* limezungumzwa sana na kimekuwa ni kilio kikubwa sana cha wawekezaji, tuliangalie kwa mnasaba wake ili tuone tunawasaidia wawekezaji kuuza zile rasilimali zao, lakini pia upande mwengine tuangalie na sisi kama nchi tunanufaika vipi katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho kwa leo. Nalielekeza katika kipengele hiki cha 5(f) kuendelea na ujenzi wa nyumba za viongozi wakuu wa serikali na hapa ndipo msingi wa hoja yangu kwa leo ulipo, muda ukisha niongeze hata dakika mbili ili niweze kumalizia.

Mhe. Mwenyekiti, yameelezwa mengi. Lakini kwenye hili mimi nina *concern* moja kwanza kabla sijasema lile nililokusudia. Katika ujenzi huu wa nyumba za viongozi wakuu wa serikali. Mhe. Mwenyekiti, nataka niishauri serikali ama niiombe sana, kumekuwa na utitiri wa nyumba nyingi sana za viongozi katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Lakini nyumba hizi ukijaribu kufuatilia tafsiri yake haiji. Nyengine utakuta zimekodishwa, nyengine zimemilikiwa kiholela, nyengine tu watu na mabavu yao wameamua kujimilikisha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naiomba serikali na katika azma ile ile ya kuokoa fedha za serikali, badala ya kujielekeza katika kujenga nyumba nyengine, tungezifanyia tathmini hizi zilizopo ziko wapi, ziko ngapi, hali yake ikoje, ili basi tutumie fedha kidogo kuzikarabati na lile lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa badala ya kutumia fedha nyingi kujenga nyumba mpya. *(Makofi)*

Lakini kwa umaalum wake katika hili Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu kubwa niliyokuwa nataka niizungumze. Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama hili suala limezungumzwa, lakini naomba tu nilizungumze kwa hisia.

Mhe. Mwenyekiti, katika ujenzi wa nyumba za viongozi wakuu wa serikali sijaona katika hotuba ya Mhe. Waziri, ujenzi wa ofisi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa nini nasema hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mtakubaliana na mimi ofisi ya sasa ya Mhe. Rais kwa maana ya Ikulu ya Zanzibar iko katika eneo la Mji Mkongwe. Historia inatuonesha kwamba majengo mengi yaliyokuwa katika uhifadhi wa Mji Mkongwe ni majengo chakavu na ni ya muda mrefu, ikiwemo ofisi ile. Tayari tumeshashuhudia baadhi ya matukio na majanga mbali mbali ya kuporomoka na kuanguka kwa majengo hayo.

Sasa mimi niiombe serikali ione utaratibu mpya wa kutenga eneo na sio eneo tu na fedha maalum kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ofisi mpya ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nalisema hili kwa sababu limeanguka jengo la Beit-Al-Ajab, lakini usije ukategemea siku moja kuta moja likadondoka pale halafu tukabaki salama. Kwa hivyo, tahadhari ni bora ichukuliwe mapema, utaratibu huu ufanyike.

Mhe. Waziri nikuombe sana suala hili lipe kipaumbele cha aina yake, kwa sababu eneo liliopo ofisi, kwanza tu ukiangalia madini chumvi yatokanayo na upepo wa bahari peke yake ni chachu ya kudhoofisha uimara wa majengo yale. Sasa ukweli usiopingika ni jengo la zamani, usione lina ng'ara kwa rangi nyeupe lakini linakwenda kwenye uchakavu. Kwa hivyo, nikuombe sana ulipe umuhimu, lakini sambamba na hilo makaazi ya Mhe. Rais pia yana haja ya kuangaliwa upya yaliopo Migombani ni ya zamani tunapaswa tuendane na usasa uliopo na mabadiliko makubwa ya maendeleo ambayo dunia inashuhudia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo, niendelee kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa hotuba nzuri. Lakini kwa sababu nimesimama hapa, walionipa sababu ya kusimama ni wananchi wa Jimbo la Mpendae nawaomba niwashukuru sana ten asana. Imani yangu tutaendelea kushirikiana katika kulijenga jimbo na maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Shaaban Ali Othman kwa mchango wako. Sasa naomba kumwita Mhe. Bihindi Hamad Khamis atafuatiwa Mhe. Panya Ali Abdalla Mhe. Hassan Hamad Omar ajiandae.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii, Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022, 2022/2023, 2023/2024.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii nikasimama hapa mbele ya Baraza la Wawakilishi nikaweza kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kwa hotuba yake ambayo ameisoma na inamuelekeo kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye uchangiaji pamoja na vipaumbele ambavyo vimetajwa kwenye hotuba hii. Niende kwenye maeneo ya umwagiliaji maji.

Kwa kweli hapa bajeti ambazo zimepita kwa awamu iliyopita kwa kweli ilikuwa mabonde haya ambayo ni Bonde la Makwararani na bonde jengine ambalo limetajwa liko Pemba ni historia ndefu.

Mhe. Mwenyekiti, tunakoelekea sasa hivi tunaelekea kwenye uchumi pamoja na maendeleo ya wananchi. Huu ni utitiri mwingi ambao umo kwenye kitabu hiki kwa vipaumbele, lakini hiki ni kipaumbele muhimu ambacho kinagusa wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naelekeza kwa serikali bonde hili la Makwararani ni bonde la muda mrefu sana na lina historia ndefu, kama nilivyoeleza kwenye hotuba ya Mhe. Rais kwamba bonde hili lilianza mwaka 1992. Kulikuwa na *irrigation* lakini miundombinu iko lakini wananchi wa eneo lile sasa hivi wamerudia kulima maeneo yale. Kwa hivyo, naiomba serikali mpango huu ambao utaanza basi wakutane na wananchi, kwa sababu jambo lolote lile lazima mshirikiane na wananchi ndipo litakapofanyakazi vizuri na kuendelea mbele na maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Nikiendelea mbele niende kwenye ujenzi wa machinjio. Kama tunavyojua awamu iliyopita kuna utiriri wa machinjio. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri afanye anavyoweza kushirikiana kwenye wilaya zetu, ili kila wilaya kuwe na chinjio moja ambalo litakuwa ni *center* ya chinjio ya kwenye wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nije kwenye ujenzi wa Ofisi za *ZAECA*. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli najua kuwa kuna ofisi za *ZAECA* zimejengwa hata Pemba ipo Kinyasini, lakini maadili ya wafanyakazi wa *ZAECA* una haki za binadamu na kumjali Mzanzibari, na kujali heshima ya kiongozi pale wanapokwenda kumfuatilia mwananchi yeyote yule heshima inatakiwa iwepo na utu uwepo wa binadamu, ili aweze kufuatiliwa vizuri mwananchi yule asiwe na malalamiko.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri suala hili aliangalie sana na awaangalie wafanyakazi wa *ZAECA* tunajua kwamba kuna maadili ya uongozi na kuna maadili ambayo yamewekwa juu ya kumfuatilia mtu kwenye utendaji wa watu ambao wanafuatilia mambo ambayo ni ya *ZAECA*.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende kwenye vipaumbele vya Hospitali ya Wete. Kwa kweli kwa sababu mimi ni Mwakilishi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, ni lazima nizungumze kuhusu vipaumbele vya Hospitali ya Wete. Kweli hospitali hii kipaumbele chake kikubwa ni kujenga majengo lakini kunatakiwa kuwe na wafanyakazi na wataalamu. Hili ni suala moja wapo ambalo linahitajika kwenye serikali ili kusimamia hayo.

Vile vile, naomba kuzungumzia kuhusu vipaumbele vya viwanja vya michezo na viwanja vya sherehe. Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Waziri ni kweli tuna viwanja vingi sana ambavyo kwenye hotuba ya Rais kuna viwanja vimetajwa na tumechangia. Kwa

kweli kwenye Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna kiwanja hicho kimoja cha Kishindeni. Mkoa wa Kusini Pemba tunacho kiwanja kikubwa cha Gombani.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana kwa heshimana taadhima maeneo yapo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na sisi tujengewe kiwanja ambacho ni kikubwa ili kiambatane na sherehe na michezo mbali mbali ambayo vijana wetu wakuze vipaji vyao na maendeleo kwa ujumla. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele, nije kwenye barabara. Zimetajwa barabara kwa kweli barabara yetu ya Wete - Chake Chake ni lazima niizungumze nayo ipewe kipaumbele na serikali, ili iweze kuijenga mwanzo hata kufikia malengo ambayo tumekusudia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hotuba hii naipongeza na hivi vipaumbele kwa kweli tunavikubali, lakini utiriri ni mwingi sana wa vipaumbele. Utekelezaji na Mhe. Rais mwenyewe amesema utekelezaji ndio maisha bora ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, na mimi niwapongeze wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwa kuweza kunifikisha hapa na mimi nikaweza kusimama leo nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.*(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru Mhe. Bihindi Hamad kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. bi Panya Ali Abdalla, atafuatiwa na Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Juma Ali Khatib ajiandae.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kuwepo hapo saa hizi, na wale wenzetu Mwenyezi Mungu aliowapa mitihani ya maradhi mbali mbali tunamuomba awaondoshee, ili wapate tahfifu waweze kuja kushirikiana na sisi katika shughuli zetu mbali mbali. Pia waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awarehemu kwa rehema njema, awasamehe makosa yao na kuwafutia madhambi yao na kuwajaalia waingie katika kundi lake la waja wema.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niungane na wenzangu wote ambao wamechangia hotuba hii, kwa kweli wamechangia hotuba hii vizuri sana, lakini michango yao imetokana na kitabu chenyewe kwamba nacho ni kizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii basi kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote, kwa kazi kubwa na nzuri ya kuweza kutuletea kitabu hiki ambacho ni Hotuba ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti. Kwa hivyo, hiki ni kitabu kizuri kama walivyochangia wenzangu na mimi nasema napongeza kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 12 ambao unaonesha matarajio ya mapato, niende katika kifungu cha 8(1) mapato ya ndani. Nikienda katika kifungu (a) kinasema:

Kifungu cha 8(1)(a)

> “Kuanza rasmi matumizi ya mfumo wa utoaji wa risiti za kielekroniki ambazo hutoa taarifa juu ya mwenendo wa mauzo halisi ya mfanyabiashara ifikapo mwezi wa Machi 2021 baada ya kukamilika kipindi cha majaribio”.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niipongeze sana serikali kwa hatua hii. Hiki ndicho kilio chetu kila siku, tunaposema mapato yanavuja, mapato bado hayako rasmi. Kwa hivyo, hili ni moja ambalo serikali ikiweza kufanikiwa juu ya hili, maana yake ni kwamba wakwepa kulipa kodi tutawagundua kiurahisi sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika kifungu cha (c) hapo pia kinaonesha kwamba;

Kifungu cha 8(1)(c)

> “Kuwa na bei elekezi kwa ajili ya uthaminishaji wa bidhaa zinazoingia nchini”.

Mhe. Mwenyekiti, pia hiki ni kifungu muhimu sana, kwa sababu kifungu hiki ndicho kinachotutaka sisi tuweze kuwaenzi hao waleta hizo bidhaa, ili na sisi tuweze kuyapata hayo mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tu tuzingatie utitiri wa kodi tusije tukaweka utitiri mkubwa wa kodi au kodi kuwa kubwa kuliko thamani ya bidhaa iliyokwenda kununuliwa na ikaja hapa ikawashinda wafanyabiashara wetu, na tukaweza kuuwa biashara zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tukilizingatia hilo basi tunaweza tukaingiza mapato haya kwa wingi na tukaweza kunufaika katika nchi yetu, na hata ile dhana ya Mhe. Rais ambayo inasema, “Yajayo ni Neema” basi inaweza ikafikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hii. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti hotuba yake ni nzuri sana nayo imeonesha uelekevu mkubwa katika kuielekeza serikali ambapo iweze sasa serikali kujipanga katika yale ambayo wameweza kuyawasilisha. Tena niseme tu ameeleza pale Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuwa na mpango wa muda mfupi na muda mrefu ni jambo muhimu sana katika serikali, hii ndio inaweza kuendesha mipango yetu katika usahihi.

Pia kuwa na *coordination* katika mawizara yetu ni jambo ambalo linakosekana na ndilo linalotugharimu sana, inawezekana wizara hii ina mradi huu na wizara hii ina mradi huu, wote unakusudia kupeleka maendeleo kwa wananchi. Lakini kwa kutokulijali hilo maana yake tunaweza tukaitia serikali hasara kubwa.

Kwa mfano, tulikuwa tunajenga mkongo ule wa serikali ambapo pale pale kuna barabara inataka kupita. Mkongo ule mimi nilisimama mwenyewe binafsi nikauliza mbona hapa mnapochimba ni karibu sana, wakasema haa! Tunachimba kina kirefu. Lakini mwisho wake unakuja kuona ujenzi wa barabara unapoingia panakokolewa pale na ile miundombinu yote inaharibika, maana yake ni kuingizia hasara serikali. Kwa hivyo, napenda serikali lazima iwe na *coordination* ya kuweza kuunganisha na kuweza kujali kila mmoja kwa wakati wake na kwa mradi ambao unapeleka huduma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa huu wa 21 ambao unasema kuimarisha sekta kuu za uchumi. Mhe. Mwenyekiti, sekta kuu za uchumi mimi napenda sana

kuisemea hii sekta ya umwagiliaji na wenzangu wameizungumza sana. Tukiwa na kilimo hiki cha umwagiliaji maana yake tunatengeneza kwamba tutakuwa na mpango wa chakula, tutakuwa tunajiridhisha kupitia chakula na tutakuwa tunapanga hasa kujiwekea akiba ya chakula, kwa sababu kilimo cha umwagiliaji tunaweza tukalima mara tatu katika mwaka mmoja. Mimi msisitizo wangu nataka pale yanapolimwa yale mabonde tuhakikishe hakuna bonde ambalo linawachwa, kwa sababu mara utasikia huyu halimi, hapa pana kichaka na hapa pamelimwa. Ambaye halimi basi aweze kumuazima mwenzake hata kama ni kwa mkataba, lakini tuhakikishe mabonde yale yanalimwa yote.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni muhimu sana elimu ya kuwa na utunzaji sasa wa chakula. Elimu hii lazima tuwape wakulima wetu, tuangalie mtihani huu mfupi ambao umeweza kututokezea wa Mwenyezi Mungu ametuletea hii Covid 19. Tumshukuru sana Mwenyezi Mungu wameweza kuwapatia hekma viongozi wetu Marais wetu na kupitia hotuba hii nataka nimpongeze sana Mhe. John Pombe Magufuli ambaye kwa kushiriana na mwezake Rais wetu ambaye amestaafu Dkt. Ali Mohammed Shein waliweza kujenga ujasiri na wakaweza kuondosha ile *lock down* lakini kungelikuwa na *lock down* sisi tungekufa kwa njaa kabla Corona haijatugusa, kwa sababu hatuna utamaduni wa kujiekea chakula cha hakiba kwa hiyo, msisitizo wangu ni huo naomba sana serikali kuangalia uekaji wa chakula cha hakiba.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikienda katika kifungu cha (f) kuna Uimarishaji wa Vituo vya Amali. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitegemea sana hasa mtazamo wangu ulikuwa unaona hivi Vyuo vya Amali kama ndio mkombozi wetu. Lakini naiombe na niishauri serikali sana Vyuo vya Amali vipo na tunavyo lakini bado havina nyezo au dhana za kufundishia ili tukaweza kupata ule mfumo wa kuwapata watu watakaoweza kujitegemea ile elimu watakayoipata kwamba tayari itakweza kuwawezesha wao kujitegemea, wanasoma kwa *theory* lakini *practical* hamna vifaa. Kwa hiyo, naomba sana serikali iwekeze huko ili ile dhana nzima ya Mhe. Rais kwamba yajayo ni neema tupu iweze kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia kifungu h kinasema kuna ujenzi wa viwanja vya michezo na sherehe Mhe. Mwenyekiti, niseme serikali imejipanga na mimi nasema kama walivyosema wezangu tukifakiwa kuyafanya haya maana yake tumeweza kupiga hatua moja kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, viwanja vya michezo kama vitajengwa kwa kweli vikundi mbali mbali vya sanaa vitaweza kufaidika kwa sababu wataweza kukodi kumbi hizo sasa na kufanya sanaa zao na wao watanufaika kupitia sanaa zao lakini na serikali itanufaika nayo kuapata mapato.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie mchango wangu kwa kwenda katika ukurasa wa 19 ambao una shabaha na malengo ya uchumi kwa mwaka 2021/2023. Kwa kweli, shabaha ya kwanza ni kuwepo kwa amani na utulivu. Mhe. Mwenyekiti, amani na utulivu ndio jibu la mambo haya yote ambayo tunayajadili hapa tukiweza kufanikiwa kuitunza amani yetu tutaweza kufanikiwa, tukadumisha utulivu katika nchi yetu maendeleo yataweza kufikiwa kwa kasi na haraka sana.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali ijikite katika mambo haya yote ambayo wameyaweka hapa uwajibikaji katika kazi, kuendeleza, kuwajengea uwezo wafanyakazi ,kuimarisha utawala bora na kuondoa ubadhirifu wa mali za umma, wizi, rushwa, pamoja na uzembe tukiyafanya haya Mhe. Mwenyekiti tutaweza kupiga hatua kubwa

kabisa katika nchi yetu na naamini kwa usimamizi wa Jemedari wetu Mhe. Rais wetu Dkt. Hessein Ali Hassan Mwinyi tutafika mbali kwa sababu amejitoa katika kuona anahakikisha Wazanzibar wenzake wanafikia mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo napenda nichukue fursa hii kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja namuomba Mwenyezi Mungu atuelekeze katika dira yetu hii ambayo tumeikusudia ili tuweze kufikia yale yote ambayo tunayatarajia, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe, Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru Mhe. Bi. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Hamad Omar atafuatiwa na Mhe. Juma Ali Khatib na Mhe. Issa Haji Ussi ajiandae.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kupata nafasi hii kutoa mchango wangu. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri alivyotuletea Hotuba hii ya Muelekeo wa Bajeti kwa jinsi aliyoipangilia uzuri na matumaini kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza mchangio wangu katika ujenzi wa bandari ya uvuvi Mpigaduri, Mheshimiwa nazungumza tena kwa mara nyengine kama kusema ni kitu chengine na utendaji ni kitu chengine. Lakini adhima iliyotajwa humu *In Shaa Allah* kama Mwenyezi Mungu atatufanikishia mambo mazuri na wananchi wetu watakuwa na haiba kubwa sana katika kufurahia mambo haya, Mwenyezi Mungu atujaaliye. *(Makofi)*

Lakini niseme kwamba 2010-2015 hapa tulikuwemo ndani ya Baraza hili bandari ya Mpigaduri ilitajwa sana kujengwa na mpaka leo haijajengwa inakuwa kama ndoto, sasa imeekezwa katika bandari ya uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, katika kujenga bandari ya uvuvi ni pamoja na ujenzi wa masoko lazima masoko yetu kama bandari ya uvuvi imejengwa na masoko yetu yawe mazuri. Leo mpaka sasa hivi Zanzibar hii tunauza samaki chini mnada unaendelea chini ambapo *bacteria* wamejaa, lakini wenzetu kule Tanzania Bara *Alhamdulillahi* Soko la Kimataifa la Samaki Feri samaki wanapangwa katika meza wapo katika sehemu nzuri mlaji anafurahia lakini huku unakuta hali jinsi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea katika mchango wangu kuna ujenzi wa barabara huu ujenzi wa barabara ni endelevu kama ulivyotajwa hapo kama kuna kilomita 235 itajengwa barabara Unguja na Pemba, lakini katika mchango wangu najikita barabara za Pemba. Mhe. Mwenyekiti, itakuwa ni jambo la aibu na fedheha kama barabara hii itakyokuja kujengwa Pemba kutoka Chake kuekea Wete kama haijapitia njia kongwe, viongozi kama mnavyoona safari za Pemba piteni njia kongwe muone mukisha mtajifunza kwa sababu barabara ya njia Kongwe imeka kama bao la kete ukitoka kishimo hiki unaingia kishimo hiki ni aibu na fedheha tena kwa vile ilivyo.

Tunaomba kama kuna uwezaji wa barabara basi mimi katika mchango huu naomba tuanze na barabara hii ya Wete kupitia njia Kongwe inasikitisha, wananchi wamekata tamaa katika barabara hii kwamba ni jambo la 2018-2019 imefanya *evaluation,* makisio yaliyofanywa pale na wananchi kufungua *account bank* kwa kuanza ujenzi wa barabara ile. Lakini *Wallahi* mpaka leo ukipitia kwa wananchi wanakwambia barabara haijengwi hata siku moja, tunakuomba Mhe. Waziri, nguvu zako zote zielekeze ujenzi wa Chake wa barabara kuelekea Wete lakini kupitia njia Kongwe afadhali mimi naona njia ya

kutoka Wete kwenda Chake Chake kupitia Melitano kuelekea Kianga mpaka Wete inapitika sio kama hii wanapata usumbufu wananchi wetu. Ukiangalia barabara hii ya njia kongwe ndiko kwenye mazalio ya karafuu nyingi kwa upande wa kaskazini.

Halafu ndiko kunako kilimo cha ndizi, mihogo na mambo mengine kadhalika mambo haya yapo sana. Kwa hivyo, Mheshimiwa tunaomba hili ulichukue na ulifanyie kazi kwa nguvu zako zote na Mwenyezi Mungu atakupa uwezo mkuibwa sana *In Shaa Allah. (Makofi)*

Lakini jambo jengine, ni habari ya mambo ya afya ya Ujenzi ya Hospitali ya Wete. Ujenzi wa Hospitali ya Wete ni jambo zuri ijengwe, lakini mtakapojenga hospitali lazima tuwe na huduma za kutosha maana majengo yapo lakini huduma hazipo. Kwa mfano, leo Hospitali ya Mkoa ya Mkoani *Wallahi* kipimo cha damu hamna, unawakuta wananchi wetu wanakwenda kufanya vipimo vya damu pale Chake *X-ray* inakwenda Micheweni hili jambo si zuri sana lazima tuzingatie. Maana yake kama nilivyozungumza awali kama kusema jambo jengine utendaji ni kitu chengine kama hivyo haya yote ni malengo mazuri yakufikia tunakokwenda na *In Shaa Allah* Mwnyezi Mungu atujaaliye tufike.

Jambo jengine niseme mambo yote haya yatafanikiwa ambapo kwamba tutajikita katika miundombinu ya umeme na maji. Bila ya miundombinu ya umeme na maji hatutafikia malengo kwa sababu mambo haya ya nishati ndio yatakayotufikisha kufanya maazimio yote yaliyopangwa katika shughuli yetu.

Nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 41 kuna vitu vilivyopangwa hapa mafungu yaliyopangwa kwanza Uimarisahaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu, umepangwa bilioni 2 lakini hapo ukienda katika kilichopatikana ni sifuri. Vile vile, ukienda kwenye mambo ya kuimarisha  Taasisi ya Viwango Zanzibar kilichopangwa ni bilioni 3 lakini ukiangalia ni sifuri sasa tutafika huko tunakokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba kilichopangwa *In Shaa Allah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kwa jitihada zetu sisi binaadam tujaribu kukipata ili yale maazimio  yetu yaliyofanikisha hapa yapatikane. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nazungumzia hicho kitu sana kutoa mchango wangu mfupi lakini nasisitiza sana barabara ya kutoka Chake kwenda Wete kupitia njia ya kongwe wananchi wetu hawana faraja hata kidogo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa mchango wangu mfupi lakini wenye tija. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru Mhe. Hassan Hamad kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Juma Ali Khatib, atafuatiwa na Mhe. Issa Haji Ussi na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

**Mhe. Juma Ali Khatib :** Ahsante sana Mhe.Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo kukutana hapa tukiwa wenye afya na wazima sote na nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wetu wa Fedha kijana Mhe. Jamal Kassim Ali kwa hotuba yake nzuri, hotuba ya muelekeo wahali ya uchumi mpango wa maendeo na bajeti kwa mwaka 2021, 2022, 2023 na 2024 akiwa Waziri wetu wa Fedha kijana mwenye nguvu mzalendo hotuba yake ni nzuri na mimi

namuunga mkono na kwa kweli serikali imetuletea mpango mzuri huu ambao kuwa unatia moyo nakuleta matumaini ya wananchi wa Unguja na Pemba.

Serikali yetu imejitahidi sana kuendeleza Sekta ya Utalii lakini tusiutupe uti wa mgongo wa Zanzibar ambao ni zao la karafuu. Kwa kweli, dunia Mhe. Mwenyekiti, inakumbana na changamoto nyingi sana za maradhi, kwa hivyo, sisi tuhakikishe kwamba ule uchumi wetu wazao la karafuu tunauendeleza kuulima na kuwahamasisha wakulima wetu. Kwa mara kadhaa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiwasaidi wakulima wa zao la karafuu kwa kutokushusha bei ya karafuu, pamoja na kwamba duniani soko la karafuu limeshuka lakini mara zote serikali imekuwa ikiwalinda wakulima wetu wa karafuu.

Kwa hiyo, nataka kumuomba Waziri wa Fedha pamoja na Kaimu Waziri wa Biashara na Viwanda waendelee na kazi hii ya kuwalinda wakulima wetu. Kwa kweli, hivi sasa wamekuwa na wasi wasi hasa wanaposikia kwamba bado karafuu haijapanda bei, lakini wao wanajukumu kwanza nataka kuishauri serikali waanzishe mfuko maalum utakao wasaidia *ZSTC* kuwalipa wakulima wa karafuu pale wanapokwenda kuuza karafuu zao, kusiwe na kukopwa mtu akisha kupimwa analipwa pesa zake. Naipongeza sana serikali kwa sababu bei wanayotoa ni shilingi 14,000 waendelee nayo. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka kuwaomba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, waendeleze juhudi zilokuwepo kwa kupanda vitalu vya mikarafuu kwa kuviimarisha kwa mfano, tunashamba kubwa la Makuwe Pemba, hili shamba Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo kubwa sana hivi linahitaji lipandwe vitalu vya mikarafuu na bahati nzuri wale wanaolitunza hili shamba wanachukua bidii kubwa sana ya kupanda vitalu vya mikarafuu na vitalu vyake vimenawiri na nataka kuwamomba kwamba watumie mvua hizi zinazokuja sasa hivi waendeleze kupanda vitalu vya mikarafuu.

Mhe. Mwenyekiti, hata samba la Weni pia kitalu chake ni kizuri, shamba la Konde kitalu chake ni kizuri, lakini kuna shamba la Wingwi Kilindi mimi nataka kuishauri serikali kwamba kile katalu cha pale kimegatuliwa kimepelekwa katika Serikali za Mitaa. Sasa kwa kweli yale mashamba yote ya miche ya mikarafuu na miche ya minazi iliyoko chini ya Wizara ya Kilimo miche yake Mhe. Mwenyekiti, imenawiri na kustawi vizuru sana. Lakini vile vilivyogatuliwa miche yake imedhoofu na imedumaa sasa nataka kuimba serikali ifanye kila linalowezekana hivi vitalu virudi Wizara ya Kilimo kwa sababu pesa za serikali zisipotee wako wafanyakazi wanalipwa pesa za kutosha mishahara na maposho lakini hawana utaalam wa kuvitunza vile vitalu vya mikarafuu.

Kwa hiyo, ni bora virudi Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, wana wataalam waliyobobea watu wenye wenye kujitolea zaidi kwa hivyo, tutakapo viimarisha vitalu hivi Mhe. Mwenyekiti, tutapata mikarafuu mingi. Mpango wa serikali ni kupanda miakarafuu isiyozidi 1,000,000 kwa hivyo, tukilifikia lengo hili Mhe. Mwenyekiti, kila mwaka naamini zao letu la mikarafuu litaendeleza.

Lakini vile vile, nataka kuwaomba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, waendele na jitihada za serikali zilizokuwepo za kuyafichua na kuyatafuta mashamba ya mikarafuu ambayo bado kuna watu wachache wameyaficha na kuyahodhi hii ni mali ya serikali kipindi kilichopita mashamba zaidi ya 3,000 yalifichuliwa ambayo kuwa yakuwa yamefichwa na haya ni mashamba ya serikali wapo baadhi ya masheha si waaminifu wametumia nafasi zao vibaya kuyahodhi na kuyaficha mashamba haya ya

serkali. Kwa hivyo, Wizara ya Kilimo, nawaomba mkae myatafute wapo wasamaria wema wananchi wenye uchungu na wenye uzalendo na serikali yao watumieni hao watakuonyesheni.

Bahati nzuri Makamu wa Pili wa Rais anafahamu kadhia hii kwa sababu yeye alipokuwa Mkuu wa Mkoa alishiriki kinaga ubaga katika kuyatafuta na kuyafichua mashamba ya serikali na alifanikisha kazi nzuri. Kwa hivyo, nataka kumuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais asichoke aendelee kwa sababu anafaham kazi pale ilipoishia na ripoti anaijua sisi tunataka mali za serikali zirudi serikalini sio watokee watu wachache wahodhi mali za serikali.

Mhe. Mwenyekit, serikiali ina malengo makubwa na mazuri sana kwa wananchi wake. Kwa hivyo, sisi tunapoona kuna watu bado wanahodhi mali za serikali tutasema tukiwa kwenye Chombo hiki na tutaseme hata tukiwa nje ya Chombo hiki. Mhe. Mwenyekiti, katika hii kuimarisha uchumi wetu mimi napenda niishauri Wizara ya Fedha na Wizara ya Biashara na Viwanda kuwa katika ujenzi wa Viwanda. Mhe. Mwenyekiti, hapo zamani kulikuwa na viwanda vingi na vizuri na vyenye tija na vijana wengi walipata ajira mimi nikiwa mmoja wapo katika miaka hiyo. Mhe. Mwenyekiti. mimi nilibahatika kufanyakazi kule Amani lakini kulikuwa na watu wengi zaidi ya elfu moja naa kule waliajiriwa.

Kwa hivyo, ni vyema viko baadhi ya Viwanda tukivirejesha tutapata tija kwa serikali yetu kodi zitakusanywa vijana watapata ajira na uchumi wetu utaendelea kukua. Kwa Mfano, Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na Kiwanda cha Hodhari kikitengeneza flana, nepi na taulo sasa hivi tunaweza tukateneza taulo na vitu vengine kama pempasi badala ya hizo nepi. Lakini kulikwa na Kiwanda cha *Aluminium* tunaweza tukakifufua hichi Mhe. Waziri wa Fedha kiwanda hiki kilikuwa kikitengeneza masufuria mazuri kuliko yaliyotengezwa Dar-es-Salaam na Kiwanda cha *Aluminium* na kikitengeza vitu jamii ya sinia, sahani za mabati kwa hivyo, tukikirudisha Mhe. Mwenyekiti, tunaweza kupata tija kwa serikali yetu. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na kiwanda cha kutengeza waya za umeme na vifaa vya umeme na switch nakadhalika mpaka *plag* zile, *cutout*, lakini Mhe. Mwenyekiti, kiwanda hiki cha Zanzibar kilikuwa ni kiwanda bora kwa Afrika Mashariki na kati na wataalam bado wapo kwa hivyo, wapo vijana walikwenda kusomea mimi nawafaham wako mamenaja bado wapo hai serikali naiomba ikae ijipange ifufue kiwanda kama hiki, Kiwanda cha Vifaa vya Umeme.

Mhe. Mwenyekiti tukilikuwa na Kiwanda cha Mafuta ya Nazi na Samli kwa hiyo, tunaweza tukapanda minazi kwa wingi ambayo kuwa ndio lengo la serikali na mimi napongeza tuendelee kupanda minazi na baadae tuweze kupata minazi kwa wingi turudishe ile haiba ya Zanzibar ya kutengeneza mafuta ya nazi, mafuta bora. Lakini tulikuwa Kiwanda cha Samli kilikuwepom na kuna vijana serikali ipoenda kuwasomesha wataalam.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nashauri pia tufikiriae kufufua Kiwanda cha Viatu sasa hivi tunaagiza viatu kutoka nje lakini tulikuwa tunatengeza viatu hapa, wananchi walikuwa wanavaa tena vya kila aina. Vile vile, nataka kusema kwamba kulikua na Kiwanda cha

Sabuni za kuogea, tukitengeneza za tiba na hiba na sabuni za kufulia, zile sabuni za vipande na zile za tambi.

Mhe. Mwenyekiti, hii itamsaidia Mhe. Waziri wa Fedhana Mipango na itaisaidia serikali yetu katika kuimarisha uchumi na maendeleo na katika kutimiza malengo ya Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika Hotuba yake "Yajayo Yanafurahisha" na kweli *Ahamdulillah* tumshukuru Mwenyezi Mungu na tunamuombea.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kulikuwa na Kiwanda cha Ushoni. Kiwanda hichi, serikali ilikuwa inaagiza vitambaa kutoka nje. Yanatengeneza mashati mazuri, nguo nzuri za watoto na watu wazima na ilikuwa zinatiwa *label* ya karafuu nyuma ya shati na gauni ilikuwa inatiwa *label* ya karafuu au mnazi, halafu kulikuwa kuna kama na kisiwa cha Unguja na Pemba. Hizi nguo zilikuwa ni nzuri na zilikuwa zinauzwa nje Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kuishauri serikali, vitu kama hivi tutatimiza lengo la vijana wetu kupata ajira na vijana wetu kupata kazi. Mimi sina mengi ya kusema naunga mkono hoja hii. Kwa sababu lengo la serikali ni zuri na dhamira yake ni njema. Ahsante na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, Nakushukuru Mhe. Juma Ali Khatib kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Issa Haji Ussi atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Asha Abdalla Mussa ajiandae.

**Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu):** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane na wenzangu katika kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa Hotuba yake hii ya Muelekeo wa Bajeti ambayo ameiwasilisha. Ni imani yetu kwamba mawazo na maandiko haya ambayo ameyawasilisha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango yanakwenda kutafsiriwa katika ule mpango wa serikali, ili kuona namna gani tunatoka hapa tulipo, tunaelekea katika safari nzuri ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa sababu nyingi lakini mosi na kubwa zaidi ni namna ya uandalizi wenyewe wa *document* hii ya mpango kwa namna ulivyowasilishwa lakini na namna ambavyo umeandaliwa. Mimi mwenyewe ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti kwa kiasi fulani na sisi kuna michango yetu kama kamati na mawazo yetu yameweza kuwasilishwa katika kufanikisha mpango huu wa serikali. Kwa kuwa nyumba yenyewe hii ni ya demokrasia na ni ngome kwa wananchi wa Zanzibar, hatuna budi na sisi kuitoa michango yetu katika kufanikisha azma ya kujenga nyumba ya Zanzibar, Nyumba ya maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ukiutizama mpango, kama ilivyo desturi. Ni mpango ambao una *category* mbili. Kuna *category* ya miaka mitatu muelekeo na kuna *category* ya mwaka mmoja katika muelekeo wa muda mfupi katika utekelezaji wake. Mchango wangu kwa sehemu kubwa nitajikita katika kipande hichi cha pili cha muelekeo wa utekelezaji katika kipindi cha mwaka mmoja ingawa kuna mambo mawili matatu nitayasemea katika kipindi hiki cha muelekeo wa kipindi cha miaka mitatu.

Mhe. Mwenyekiti, moja ambalo ninataka niseme katika kipande hichi cha muelekeo wa miaka mitatu ni suala zima la mfumo wetu wa elimu. Dhamira ya serikali tumeisikia, mipango pamoja na jitihada za serikali tumezisikia na tumemuona Mhe. Rais kwa

busara na hekima zake kubwa ameweza ku-*convey* kongamano kubwa ambapo wadau mbali mbali wa elimu wameweza kutoa mawazo yao. Matarajio yetu ni kwamba serikali imeweza kuyachukua na kwenda kuyafanyia kazi.

Katika hili kuna eneo mahsusi ambalo ninataka niliseme nalo si jengine ni eneo la *vocational training*. Tumechangia baadhi ya wajumbe hapa, kwenye suala la *vocational training* bado tuna tatizo. Wahitimu wetu wanaohitimu katika Vyuo vya Mafunzo ya Amali, sisi wenyewe tukijipima tunakiri kwamba bado tuna mapungufu makubwa *either* katika mfumo au usomeshaji au nadharia inaizidi yale mafunzo ya vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba tu kuishauri serikali, tuna haja ya kutizama kwa jicho maalum, namna gani ya kuweza kuboresha mfumo na utaratibu mzima katika eneo la *vocational training*, kama tutaweza kuhamasisha vijana vizuri na mfumo tukiubadilisha ukikaa vizuri, suala la elimu ya mafunzo kwa maana ya mafunzo ya elimu ya amali nina uhakika inaweza kuwa msaada mkubwa sana katika kuisaidia serikali na jamii katika suala zima la ajira. Nalisema hili, kwa sababu ya lile ambalo tumeliweka katika malengo ya muda mfupi kwa maana ya utekelezaji wa mwaka huu kwenye suala zima la ajira kwa vijana katika program nambari saba, ambayo tunategemea katika kipindi cha bajeti inayokuja litasomwa.

Mhe. Mwenyekiti, ili tuende na utaratibu wa kupata ajira. Maana yake tuna haja ya kufanya maandalizi mazuri na kwa bahati mbaya ukisoma vipaumbele vyengine vingi vinakupa mashaka kidogo juu ya namna ya kutengeneza hizo fursa za ajira. Kwa kweli, fursa za ajira ukisoma na Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi sote tumekuwa mashahidi hapa. Tumeipitia Hotuba ya Mhe. Rais namna gani ambavyo ameji *commit* katika suala zima la ajira. Tumeahidi kuwa tutayatekeleza na tutayapatia fursa ajira zisizopungua laki tatu, muda wetu ni kipindi cha miaka mitano. Sasa ili tuweze kufikisha hesabu hiyo tunalizimika kutengeneza mikakati mizuri na suala la ajira haliishii tu ajira ya serikali ni pamoja na sekta binafsi pamoja na miradi.

Ushauri wangu ni kwamba, kwenye hii miradi ambayo serikali tunaikusudia kuifanya kwa kipindi cha mwaka mmoja au kipindi hichi cha miaka mitatu. Kwa hivyo, ni lazima tutafute na tubuni miradi ambayo itatoa nafasi kubwa kuweza kuwawezesha vijana wetu kuweza kupata fursa za ajira. Imani yangu ni kwamba, kama miradi ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa *airport* pamoja na bandari Mwenyezi Mungu akijaalia vikiakisi na kuanza ku-*take floor* bila ya shaka tutaweza kupata fursa kubwa ya kusaidia kwenye suala zima la ajira. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ambalo nilitaka kuishauri serikali ni suala zima linalotokana na mpango wa serikali katika suala la umwagiliaji. Mradi wa umwagiliaji, nadhani kuna nafasi za serikali tutizame na upande wa pili. Tunalima kwa mfumo wa mazoea, tutakwenda kwenye mradi wa umwagiliaji tutalima kwa mfumo wa mazoea.

Wakati tunafanya ziara, tuliambiawa robo eka, mtu alikuwa anazalisha viroba vya kilo 50, viroba saba na sasa anazalisha viroba 12 mpaka 15. Kutokana na hali hiyo ndani ya mwaka mmoja ana uwezo wa kulima mara mbili, ukifanya hesabu na kukaa na wachumi wametuambia. Ili tukiuke hapa tulipo na tutoke kwenye dimbwi la umasikini kwa maana ya kwamba ule ufukara, tunatakiwa tuwe na kipato kinachozidi *dollar 900* kwa mwaka. Sasa ukichukua hichi ambacho kinalimwa na mkulima na ukikitia kwenye thamani ya

fedha hakiwezi kufika huko ambako tunatarajia katika uchumi wa kati ambao tunakusudia tufike kama ambapo tupo, ili tuweze kwenda juu zaidi.

Sasa, nadhani kama serikali tufikirie na tutafute eneo moja dogo tufanye *feasibility study* kwa maana ya kwamba majaribio ya ukamilifu wake, tujaribu kuwahamasisha wananchi wetu kutizama na *angle* ya pili katika kilimo cha biashara hasa kwenye matunda na mboga mboga.

Kilimo hichi cha mpunga kumekua ni kilimo cha mazoea kwa maana ya kwamba mtu analima ili apate chakula kwa ajili ya kula. Lakini thamani anayoipata bila ya shaka ni ndogo kuliko ambacho angeweza kukipata kama angejaribu mazao mengine katika kulima.

Mhe. Mwenyekiti, suala la tatu ni kuwa dhana ya serikali ni kubwa sana kwenye suala zima la uchumi wa buluu. Imani yangu ni kwamba serikali tutatumia nguvu, maarifa, fedha na mipango ili kulifanikisha hili na tufike kwenye kuisaidia jamii yetu hasa suala la uimarishaji wa uchumi wa buluu kwa nadharia ile pana ambao watakwenda katika upande wa *marine*, ambao watakwenda katika upande wa gesi, mafuta na kwengineko. Sasa kwenye mpango, tunakwenda na utaratibu mwengine mpya wa kuanza kufuga samaki kwenye mabwawa. Kwa upande wangu nadhani kwa akili za kawaida kwa mtu wa mtaani tungetumia nafasi kubwa ya kuwashawishi watu wetu kwa kuwawewezesha nyenzo na kuweza kuikabili ile bahari tungekuwa tumepata nafasi nzuri zaidi ya kuwasaidia kuliko kuwashawishi kuanza kufuga samaki.

Mhe. Mwenyekiti, nalisema hili kwa akili ndogo tu kwa maana ya kwamba, ukichukua samaki ambao wanakwenda kufungwa kwa sehemu kubwa watakua ni samaki wa maji baridi. Tukishazalisha samaki, tunakwenda kwenye tatizo jengine la soko kwa samaki wenyewe. Watu wengi wa Zanzibar chakula chetu ni samaki wa maji ya chumvi. Kwa hiyo, nadhani hili tuna haja ya kulitizama vizuri, namna ya kuwawezesha wenzetu waweze kufika maji makubwa na wavue vizuri ili wapate kipato kingi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka kuishauri serikali ni suala zima la kuendelea na Mfuko wa Miundombinu. Nilikuwa naiomba serikali, tumeona makusudio yanayokusudiwa kukusanya fedha ni takribani bilioni 49 ambazo zitatokana na mfuko wa miundombinu. Nilikiwa naiomba tu serikali iweze kutizama vizuri kama kuna uwezekano wa kutengeneza *opportunity* nyengine katika eneo hili la mfuko wa miundombinu, ili kuongeza patononeke kidogo zaidi ya hichi ambacho kinalengwa kwa ajili ya kusaidia baadhi ya miradi ambayo itaweza kuleta tija na faida kubwa sana kwa wananchi wetu. Ipo baadhi ya miradi nina uhakika tukipata fursa kubwa ya fedha katika vyanzo vya ndani basi inaweza ikawa kichocheo kikubwa sana katika suala zima la upatikanaji wa fedha haswa kwa baadhi ya miradi hii midogo midogo.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho ambalo lipo katika kipindi cha miaka mitatu, ningeweza pia kuishauri serikali ni suala zima la uendelezaji wa juhudi za uhifadhi wa Mji Mkongwe na mambo ya kale.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili ni eneo ni kubwa sana na ni eneo mtambuka. Maeneo ya mambo ya kale nadhani yamekuwa *started* nchi nzima, yapo vijijini ambapo nadhani wizara na serikali kwa ujumla tuna haja ya kuyafuatilia vizuri kwa ajili ya kuweka

kumbukumbu ikibidi na kuyaendeleza. Lakini kwa upande wa Mji Mkongwe nadhani umefika wakati wa serikali kutizama vizuri kama ambavyo inafikirika vizuri zaidi suala zima la Mji Mkongwe katika kutoka hapa ambapo tupo, matumizi yake na ambayo yataweza kuleta tija na faida kubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, wapo baadhi ya watu wengi ambao wanaishi Mji Mkongwe na wanaishi katika nyumba ambazo zimejengwa kwa muda mrefu. Inawawia vigumu sana haswa kwenye suala la ukarabati na ugumu unakuja zaidi kutokana na masharti, miongozo na maelekezo yanayotokana na sifa ya mji wenyewe. Sasa ukiwatizama baadhi ya watu kipato chao ambao wanakaa Mji Mkongwe masharti, miongozo na maelekezo wanayopatiwa kwa ajili ya kuhifadhi Mji Mkongwe inawawia vigumu sana katika kukarabati. Hivyo, nadhani kama vile serikali ambavyo inafikiria basi umefika wakati wa kutangaza utaratibu maalum kwa ajili ya eneo la Mji Mkongwe, ili tuweze kupunguza kadhia ya majumba kuanguka, changamoto ya ukarabati wa majengo lakini pia kuongeza fursa za watu ambao wanataka kuwekeza kwa uwekezaji wa kiwango cha kati.

Kwa kweli, naamini kama kuna watu wengi ambao wanaweza kuwekeza mahoteli, hoteli za kati za nyota ya nne, tatu, mbili ambao kwa maeneo ya Mji Mkongwe inawezekana ikawa ni maeneo mazuri na yenye tija na maslahi mapana kwa taifa letu. Kuendelea kuachia watu kuishi na sote tukiwa tunajua kwamba baadhi wa walio wengi wanashindwa kuzitunza mzigo huu taendelea kurudi serikalini. Baada ya kuwa ni sehemu ya kuzalisha fedha itakuwa ni sehemu ya kutumika fedha. Jambo ambalo sidhani kama litakuwa na afya na maslahi mapana na nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu nipongeze tu juu ya mpango huu mkubwa, mzuri ambao naamini kama utatekelezwa vizuri na hii michango ambayo tumeitoa Waheshimiwa Wajumbe serikali ikizingatia tunaweza tukawa tuna mpango mzuri utakaoweza kusaidia nchi yetu katika kufanikisha suala zima la maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitamke tu kwamba nauunga mkono mpango huu kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante na nakushukuru Mhe. Issa Haji Ussi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassana Juma, atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Suleiman Haroub Suleiman ajiandae.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango juu ya hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo katika Bajeti ya mwaka huu tunaokwenda nao.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyotangulia wenzangu, nataka nimpongeze sana kijana wetu, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kadri alivyoweza kuwasilisha mpango wake kwa ufasaha mkubwa. Mpango ambao unatupa matumaini makubwa kama ilivyoonesha katika ziara zake Mhe. Rais na katika hotuba zake mbali mbali na hata huo mpango bado unaendelea kutupa taswira kwamba Zanzibar inayokuja itakuwa ni ya neema tupu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mpango huu, kwanza nisije nikasahau nawashukuru sana wananchi wangu walionileta hapa wa jimbo langu la Shaurimoyo. Nawashukuru kwa kuendelea kuniamini, kuweza kuwatumikia katika Baraza lako hili tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mpango huu, kuna mambo mengi ambayo yameelezwa na kitu ambacho nilichofurahi sana, kwamba katika yale malengo au yale yaliyokusudiwa yameelezwa mambo mbali mbali ambayo moja kwa moja yatatusaidia katika kuboresha maisha yetu.

Mhe. Mwenyekiti, unajua wananchi wetu wa kawaida haswa wa kwetu nga'mbu kule unapomwambia kuna uchumi wa kati, uchumi wa juu sijui uchumi wa nini wao hawaelewi sana, hizi *terminology* ni za kitaalamu zaidi. Lakini wananchi wetu wanataka kujua je, katika bajeti ya mwaka huu, katika mipango ya serikali je mfukoni mwangu itaongezeka shilingi ngapi katika shughuli zangu za maisha ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kuna eneo moja hapa sikuliona sasa nitamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aje atuambie namna gani ya kuweza kukuza mitaji ya wajasiriamali wadogo wadogo haswa katika mikopo ya wananchi wadogo wadogo.

Katika eneo hili serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wanawake, Jinsia na Watoto huwa wanatoa mikopo mbali mbali. Lakini na mimi nilikuwa naomba tuongeze kitu hapa. Hebu wenzetu wajaribu kufanya utafiti. Ukiangalia mikopo mengi inayotoka inakwenda kwa watu ambao pengine hata miradi hawana alimradi inakuwa wamejikusanya watu watano mpaka sita wanaomba fedha na wanapewa pesa, halafu hata urejeshaji wake unakuwa kidogo una changamoto.

Ushauri wangu hapa, ungelifanyika utafiti. Kuna vijana wengi na kina mama ambao wamejiajiri wao wenyewe hivi sasa. Lakini tatizo lao mitaji yao inakuwa midogo katika kuziendeleza zile biashara zao. Sasa nadhani wangejaribu kutafutwa wale, wakaongezewa mitaji, kwa sababu mitaji ile ikaongezewa wanaweza kuimarisha mitaji yao na biashara zao na wao vile vile wakapata kuongeza au kuajiri na watu wengine kwa ajili ya kuongeza kipato.

Sasa eneo hili nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia mpango huu wangejaribu kuangalia sana, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu hii bajeti moja kwa moja nao inawagusa ndani ya mifuko yao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo nilisema juzi lakini leo narejea tena kulisema nilipongua nimechangia hotuba ya Mhe. Rais. Suala la elimu ya juu, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti mipango ya serikali hii ya awamu ya nane lazima watoto wasome kweli kweli, kwa sababu unaposema kwamba unaleta viwanda unapoleta viwanda uchumi mkubwa wa gesi na mafuta lazima tuwaandae vijana katika suala zima elimu tatizo tulilokua nalo Mhe. Mwenyekiti, pamoja kwamba wanafunzi matokeo yao mitihani yao inakuwa kidogo hawafanya vizuri lakini hawa ambao wanaofanya vizuri, tuna wanafunzi wengi sana sasa hivi wa vyuo wanashindwa kupata mikopo hasa hii ya elimu ya juu na hasa ukiangalia wale wanaopata *scholarship* za nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, unapomlipia wanafunzi asilimia 50 au 60 ile 40 bado wananchi wetu wengi wanashindwa kuhimili kuweza kutoa fedha ile kwa ajili ya ku-*support* watoto wao. Sasa hili moja katika kujenga taifa ambalo la kizazi ambacho cha maendeleo lazima tuhakikishe kwamba serikali yetu tuongeze bajeti katika mfuko wa elimu ya juu lakini vile vile kuweza kupunguza ile asilimia ya mwananchi na yeye kuchangia ikiwezekana tuende asilimia mia moja (100). Kwa hivyo, fedha zile baadae atakuja kuzilipa naamini vijana wetu wengi hasa watoto wa wanyonge wataweza kusoma elimu za juu, ili kuja kuleta tija katika taifa letu katika kuja kutumikia wananchi wenzao.

Nimefurahishwa sana na katika mpango ambao umekusudiwa malengo na mkakati wa serikali kuhusu kuimarisha suala zima la maji safi na salama. Mhe. Mwenyekiti, katika jambo linalotugombanisha na wananchi majimboni suala la maji. Mhe.Mwenyekiti, tunashukuru sana ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inatupatia fedha za mfuko wa maendeleo, lakini fedha zile za mfuko wa maendeleo ukingalia asilimia kubwa tunachimba visima vidogo vidogo vya maji. Leo naamini serikali yetu ikiweka miundombinu ya maji wataalamu wetu wakaweza kufanya kazi vizuri mimi naamini maji yakitiririka kila pahala katika maeneo yetu chuki baina ya wananchi na wawakilishi wao lakini vile vile na sisi tutapata kushughulikia mambo mengine ya maendeleo jambo ambalo litaweza kutuletea tija kubwa sana kwa hapa nchi yetu. *(Makofi)*

Sasa hili kwa kweli pia nisema niweze kulisema ili sasa kuhakikisha kwamba linatusaidia katika maeneo yetu. Jengine hili suala lipo kidogo nje ya huu mpango lakini nafikiri Waziri wa Tawala za Mikoa yupo. Kuna tangazo ambalo linatuhusu sisi wakaazi wa mjini, ambalo limetoka katika kipindi hichi kwamba Baraza la Manispaa wanatangaza kwamba wananchi wanatakiwa walipe shilling elfu tatu kila nyumba ya usafi na maduka shilingi elfu sita sasa mimi kwa bahati mbaya sijawahi kuja kuchangishwa hiyo elfu tatu lakini sisemi nidaiwe hapana.

Sasa kama kuna utaratibu huu mpya wa kuchangishwa nyumba zote za mjini kwa pesa za usafi shilingi elfu tatu wala sio tatizo, kwa sababu kwanza serikali manispaa yetu itakusanya fedha nyingi lakini fedha zile zitarudi kuja kutoa tena ajira kwa watu wetu. Changamoto iliyojitokeza sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, na hili nikasema niliseme kwa sababu tayari wananchi wangu wamekuja kunilalamikia. Tunavyo vikundi vya usafi wa mazingira katika maeneo yetu, vimejitolea sana zaidi ya miaka 10 sasa hivi. Walikuwa wamepata tenda katika masoko mfano kama mimi soko la Saateni kuna kikundi changu cha wakina mama ambao wao walikuwa wanasafisha mtaro bila ya kulipwa.

Wanasafisha mitaa bila ya kulipwa wamesafisha soko juzi wameshakuja kunyang'anywa na sijua na mradi wa *Green Waste*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, leo tunaleta kampuni wakati tayari kuna watu wanataka usafi kwanini wasiwekewe masharti ya kuwa ajiri wale ambao tayari wameshazoea kuzoa taka jua na mvua. Leo zinakuja kampuni wanaletwa watu hata kuzoa taka hawajui wale watu wetu wanaachwa mitaani sasa hivi wanarudi kuja kupiga virungu kwa waheshimiwa, kwa kweli sio jambo zuri sana. Wakati watu wanaweza kujitolea, watu wamefanya kazi ya mfano kwa muda mrefu katika jimbo ambalo lilikuwa katika hali ya usafi sana ni jimbo la Shaurimoyo kwa sababu wananchi wamejitolea tunavyo vikundi vya usafi lakini sasa hivi wameshanyang'anywa kazi wanapakata mikono sijui waende wapi.

Sasa hili nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri ulifanyie kazi kwa sbabu ni moja kati ya jambo ambalo limeshapunguza hiyo ajira katika hizo ajira laki tatu mimi jimboni kwangu zishaanza kupungua zimechukuliwa na Kampuni ya *Green Waste*.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika mchango wangu, kuna suala zima la bima ya afya katika malengo katika mpango Mhe. Mwenyekiti, katika jambo ambalo limelipigia kelele sana muda mrefu sana suala la bima ya afya. Mhe. Mwenyekiti, lazima tukiri wakati umefika bila ya bima ya afya sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, kwa jinsi tunavyovaa wazanzibar hatuwezi kutibu watoto wetu. Sisi tunazaa tunajitahidi na ndio udume sisi kwetu ile uwe kidume ukishaowa baada ya mwaka mmoja unaulizwa vipi huko mshakuwa wangapi.

Sasa leo bila ya bima ya afya Mhe. Mwneyekiti, tutaendelea kulaumu serikali yetu, tutaendelea kulaumu Wizara ya Afya lakini kwa mkakati na mpango huu na mimi nawaombea sana Mhe. Mwenyekiti, kama kuna sheria basi katika Baraza hili linalokuja basi iletwe hiyo sheria ili kuwe na bima ya afya ya jamii, ili sasa kila mwananchi aweze kuwa na bima ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda Dar–es–Salaam sasa hivi zamani *Hindu Mandal* pale. *Hindu Mandal* pale zamani humkuti mtu kama mimi lakini leo sasa hivi ukienda wamejaa watu, mtu kalala kitandani pale kajiachia anapata tiba ndio bima ya afya. Kwa hiyo, hata ile bima ya afya ingawa wengine wanasema inaleta matabaka lakini bima ya afya inaondoa matabaka, kwa sababu mwananchi anaweza akatibiwa katika hospitali ambayo tajiri yeyote anaweza akatibiwa. Sasa mpango huu naomba sana serikali yetu mimi nawapongeza sana waulete kwa haraka, ili tuweze kuupitisha wananchi wetu waweze kupata afya nzuri.

Jambo jengine nililovutiwa sana serikali kuweka katika huu mfumo wa *e-system*, yaani *e-payment, e-tax, e-health* na kadhalika. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati tuliwahi kupata safari ya Mombasa. Tulikwenda tukatembelea bandari ya Mombasa tukazungumza na uongozi wa Shirika la Bandari wakatuambia zamani Shirika la Bandari lilikuwa linapata ruzuku kutoka serikalini lakini baadae walivyobadilisha mfumo wa *e-tax, e-payment* kila kitu kinakwenda katika *system.* Wamesema walipunguza ule mlolongo wa mtu kwenda kulipa maana yake mfanyabiashara alikua na ile fomu yake ina mihuri karibu tisa kutwa nzima anakwenda anagonga mihuri tu anatoka hapa anakwenda hapa.

Lakini, waliporekebisha ule mfumo ya *e-port* pale Mhe. Mwenyekiti, eneo moja tu uankwenda na ushapeleka *BL* yako ile kila taasisi imeshakusanya chake ndani ya masaa sita wanasema tayari umeshamaliza matokeo yake sasa hivi shirika la Bandari la Kenya sasa hivi wanaweza kupata mikopo ya moja kwa moja bila ya kupitia serikali kuu, na badala yake kupitia *European Union* na mashirika mengine ya kimataifa. Kwa kweli, hivi sasa bandari zao wanajenga wao wenyewe, kwa sababu ule mfumo umeweza kusaidia sana.

Sasa na hapa nimeona mabadiliko ya Shirika la Bandari nilikuwa na huo mfumo serikali yetu ifanyie kazi na kama wanataka kujifunza sio vibaya waende pale Kenya wakajifunze kwa wenzao namna gani wanavyoweza kuboresha mapato ya Shirika la Bandari na kuweza kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika suala la afya. Serikali yetu tumejitahidi sana katika kuongeza bajeti mpaka ikafika katibu bilioni 12 kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Kitu ambacho bado kinashangaza unakwenda katika baadhi ya hospitali zetu hasa za vijijini na katika vituo vyetu vya afya unakwenda unaambiwa dawa hii hapana nenda kanunue hili bado.

Hapa kwa kuwa tuna mkonge huu wa taifa mimi nadhani hili la suala la *e-health* liweze kuekewa mpango wake maalum, ili sasa kujua bohari kuu kule anajuwa katika ule mgao unaotoka sio kama kuna mgao wa kila mwezi kupelekewa kitu aina fulani hapana. Ili sasa waweze kujua kwamba kila kituo kina upungufu wa dawa aina gani waweze kusambaziwa katika kipindi gani ili wananchi wetu wasisumbuke. Leo Mhe. Mwenyekiti, utakuta walinzi wanagombana hospitali ya Mnazi Mmoja wanagombana na wananchi, mwananchi anakwenda katika kituo cha afya hapati huduma anakwenda Mnazi Mmoja wakati Mnazi Mmoja ni hospitali ya Rufaa, je kama katika kituo chake kule alipo angepata ile huduma angehangaika kwenda Mnazi Mmoja. Asingekwenda, sasa hili linatokana na upungufu au ukoserfu wa dawa katika vituo vyetu vidogo vidogo vya afya.

Mhe. Mwenyekiti, naona unanitazama niambie basi dakika ngapi bado ili na mimi niweze kukamilisha. Mhe. Mwenyekiti, limetajwa suala la Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo. Heh! Ama kweli! mpaka mfuko wa jimbo munataka kuupeleka kwenye mipango ya Halmashauri. Mhe. Mwenyekiti, mfuko wa jimbo ni fedha maalumu zimeombwa na Waheshimiwa Wawakilishi kuondoa changamoto ndogo ndogo katika maeneo yao. Leo fedha hizi mkisema ziende zikapangiwe kwenye Halmashauri mtawagombanisha Waheshimiwa na wananchi wao. Wakati mwengine unakwenda unaambiwa skuli paa linavuja pale huku Halmashauri washapanga mpango wao wa mwaka mzima pale unafanya nini hakuna.

Wakati mwengine unakwenda kule sehemu nyengine unaambiwa kisima pampu imeugua Mhe. Mwenyekiti, hizi fedha ziacheni kama zilipo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais waendelee watu wako kuja majimboni pamoja na *CAG* kuja kuangalia matumizi na marejesho ya fedha hizi. Serikali kuu muna vianzio vingi vya mapato muna mipango yenu mingi kabisa, sisi huko hatuingii. Kwanza sisi wawakilishi sio madiwani, Bara wenzetu kule wabunge ni madiwani sisi wawakilishi sio madiwani sasa pesa zetu munazipeleka manispaa zikafanye nini.

Mhe. Mwenyekiti, tuachieni sisi wenyewe tutazisimamia na tutazitumia kama tunavyozitumia sasa hivi na sio kama tunatumia pesa zenu tu za mfuko wa jimbo tunaongezea na zetu nyingi mara kumi kuliko hata hizo zenu. Sasa hili Mhe. Waziri wa Fedha hizi naomba tuachie hapa kipengele hichi kifute wala hakifai huku.

Mhe. Mwenyekiti, tuje katika suala la kodi la vileo. Katika jambo ulilonifurahisha Mhe. Waziri wa Fedha ingawa najua wengine watakasirika. Kuongeza kodi ya vileo, tena kama umekusudia kuongeza kwa asilimia 40 tunakwamba uongeze asilimia 100. Sasa hivi ulevi umekuwa tena hauna mwenyewe kila mtu analewa mpaka watoto wadogo wanalewa. Mhe. Mwenyekiti, kodi ya vile iongezeke leo kuna baa kila pahala siku zote Mhe. Nadir Abdullatif analalamika. Hapo kwake akitoka nje tu tafrani kuna baa sita zimejipanga. Mimi nafikiri kodi ya vileo hii ikiongezeka watapiga kelele lakini itakuwa tija kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Wenzetu kule Bara walipiga marufuku viroba sasa hivi hukuti viroba sasa hivi kidogo walau watu wanakewa kwa heshima. Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nimalize usinipigie kengele namalizia dakika mbili tu.

Mhe. Mwenyekiti, katika la mwisho kabisa hapa mumeeleza katika ukurasa wa 19 shababaha na malengo makuu ya taifa letu. Kwanza amani na utulivu, utawala bora, kupiga vita ubadhilifu wa mali ya umma na kuendeleza wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, katika jambo ambalo limeitangaza Zanzibar kwa muda mfupi sana saula zima la utawala bora, suala zima la uwajibikaji, mimi tunawapa nguvu tunampa nguvu Mhe. Rais wa Zanzibar, tunampa nguvu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar endeleeni kupambana na wabadhirifu wa mali ya umma sisi tupo nyuma yenu na Mawaziri wetu tumeona. Wengine kidogo bado hatujaona kashikashi zenu wako mawaziri tunaona wazi wazi wantangaza wabadhirifu wengine bado munawaonea haya.

Mhe. Mwenyekiti, msisubiri tukaja tukawaibuwa hapa tunataka nyinyi kwanza katika wizara zenu muanze kusafisha ili sisi tuje tumalizie iyo kazi iliobakia. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakupongeza sana kwanza kwa utulivi wako na kunistahi mnadhimu sasa hivi hukunipigia kengele naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, ambae ndio Mnadhimu na kweli nakuheshimu tokea ulivyopata unadhimu basi na mimi nakuheshimu maana najua huko mbele tunakokwenda kazi itakuwepo kweli kweli. Sasa naomba nimuite Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Suleiman Haroub na Mhe. Hassan Hafidh ajiandae.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenifikisha hapa nikiwa katika hali ya uzima. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi kwa kumteua Mhe. Waziri wa Fedha makini ambae ameweza kuandaa hotuba hii ya mulekeo ya hali ya uchumi na mpango wa maendeleo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021 mpaka mwaka 2024.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane na wajumbe wenzangu ambao wamechangia hotuba hii na wamechangia kwa mambo mbali mbali ambayo yamewagusa wananchi wetu lakini pia na mimi nitagusia mambo machache ambayo yapo katika hotuba hii ambayo nimeyaona.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watu wake ambao wameandaa mpango huu, kwani mpango huu umezingatia vigezo vya ugawaji wa rasilimali fedha ambazo imezingatia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa mwaka 2020 – 2025 lakini pia umezingatia maeneo ya vipaumbele vya mpango wa maendeleo, pia umezingatia maagizo maalumu ya serikali kwa mujibu wa vipaumbele vya taifa. Mhe. Mwenyekiti, pia kabisa wamezingatia programu na miradi ya mikakati ambayo yakitaifa. Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wangu mimi sitochangia mengi lakini nitagusia mambo machache. Kwanza kabisa nigusie suala zima la mwenendo wa uchumi wa Zanzibar ambao umefanyika kwa kipindi cha miezi sita Julai - Disemba 2020.

Mhe. Mwenyekiti, serikali ilifanya hatua mbali mbali ambazo zilitumika katika kuimarisha mapato ya serikali na kusaidia kurahisisha shughuli za kibiashara na shughuli hizi au hatua hizi ni pamoja na kupunguza kiwango cha kutoza kodi ya ongozeko la thamani yaani *VAT* kutoka asilimia 18 hadi kufikia asilimia 15.

Kwa kweli, katika hatua hizo mbali mbali mimi nitagusia katika hatua ya kufuta tozo la ada zote kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa masokoni, mamalishe na waanika madagaa na Juakali, ambacho walichokuwa wanatozwa shilingi 1000 hadi shlingi 2000 kwa siku na wanachotakiwa kulipa katika mamlaka ya serikali za mitaa, wafanyabiashara hao walitakiwa kulipa kiwango kimoja cha ada ya shilingi elfu 30 kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, japo kuwa serikali imechukuwa hatua hii lakini bado changamoto ipo inaendelea kwa wafanyabiashara hawa. Kwa mfano, ukienda maeneo ya Darajani utaakuta wafanyabiashara wanaofanya biashara katika *parking* pale kwa siku wanalipa shilingi elfu 4 ukifanya mahesabu kwa mwezi wanatozwa shilingi kama laki moja na ishirini na kwa mwaka wanatozwa kwa mfanyabiashara mmoja zaidi ya shilingi milioni moja na laki nne.

Sambamba na hilo, ukija katika maeneo ya hoteli hususani maeneo ya Kiwengwa utamkuta mfanyabiashara kwa mwezi anatozwa shilingi elfu sita za ada ya usafi, pia ukiangalia wanatozwa ada ya leseni zaidi ya shilingi elfu sitini. Kwa hiyo unamfanya mfanyabiashara huyu kwa mwaka anatozwa zaidi ya shilingi laki moja nakuendelea. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, jambo la kuzingatia kwamba wizara husika ihakikishe kwamba wafanyabiashara hawa nao wananufaika na tozo hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye suala zima la vipaumbele vya serikali muelekeo wa hali ya uchumi na mpango wa maendeleo ya bajeti kwa mwaka 2021 – 2024. Mhe. Mwenyekiti, nimeona imeshauriwa kwamba vitengo vinavyohusika na manunuzi viwe makini, vichaguwe wakandarasi wa miradi wa ujenzi wenye uwezo wa fedha na taalumu kwa lengo la kuleta miradi yenye ubora na viwango.

Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono kwa asilimia moja kwa suala hili kwa sababu kwamba hivi vitengo vya manunuzi vitumie zile taaluma ambazo au watumie maadili ya ununuzi au ununuzi wa vifaa hivi, kwa sababu tunaona kwamba miradi mingi haina viwango. Kwa hivyo, tuhakikishe kwamba wizara husika au taasisi husika inasimamia kuhakikisha kwamba lengo lililotakiwa hapa linafikiwa kwa wakati.

Vile vile, naunga mkono ushauri wa bajeti kwamba kuongezeka kwa bajeti ya ustawi wa jamii, ili waweze waratibu wanawake na watoto waweze kusimamia kesi za uzalilishaji kwa ufanisi zaidi. Tunafahamu katika maeneo yetu kuna waratibu wanawake na watoto ambao hawa wanasimamia shughuli nzima za uzalishaji wanawake na watoto, kwa kweli suala hili ni suala nyeti na suala ambalo linatuumiza hususan sisi wanawake kwa ujumla, kwa sababu wanawake na watoto ndio tunaodhalilishwa zaidi.

Kutokana na hali hiyo, tumpongeze sana Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kuanzisha Mahakama ya kesi za uzalilishaji

wanawake hapa Zanzibar, naamini kwamba wahusika wa maeneo haya wa Mahakama watatenda haki ili kuhakikisha kwamba suala hili linaondoka kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, pia nije kwenye suala zima la ajira ambalo amesema suala zima la ajira kwa vijana lifanyiwe kazi ili kufikia lengo la Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajira laki tatu zilizoahidiwa, suala la ajira kwa vijana ni suala kubwa hapa kwetu Zanzibar na suala hili lipo kwenye ajira ya serikali lakini pia kuna ajira za binafsi.

Nikiendelea na mchango wangu, nikija kwenye suala zima la ajira za serikali tuangalie basi kila wizara na taasisi husika ipo haja sasa serikali iangalie au ifanye uhakiki wa wafanyakazi ambao wapo wanaotakiwa kustaafu basi wastaafu kwa wakati, lakini pia kuna wafanyakazi hewa ambao hawa wanaziba nafasi ambazo vijana wetu walitakiwa wapate nafasi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya uhakiki wa wafanyakazi ambao wapo tunaamini kwamba kuna wafanyakazi ambao wanatakiwa wastaafu, lakini pia kuna wafanyakazi hewa, lakini pia kuna wafanyakazi ambao wanafanyakazi kwa mikataba naamini kwamba likizingatiwa hili basi vijana wetu wanaweza kupata ajira nyingi zaidi kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini kuna suala zima la kuwawezesha hawa vijana na kujiajiri wenyewe kuna mifuko mbali mbali ambayo tulipitisha katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ukiwemo mfuko wa *Khalifa Fund*.

Vile vile, kila mwaka hapa tunapitisha bajeti ya ajira kwa vijana ambapo pesa hizi zinatolewa na serikali kwa ajili ya kuwawezesha vijana kupata ajira. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba wizara husika ihakikishe kwamba vijana hawa wanapatiwa fedha hizi kwa ajili ya kufanya kazi zao, ili waweze kujiajiri wenyewe. Tumeona hapa kwamba katika ukurasa wa 32 kuna vijana wamewezeshwa kwa ajili ya ruzuku ambayo imetolewa kwa vikundi sabini na tano vya ukulima wa mboga mboga, ambavyo wamejengewa *green house* na katika maeneo ambayo wamejengewa ni eneo la Pangatupu na maeneo ya Pangeni.

Kwa kweli, niseme kwamba katika maeneo haya ni kweli *green house* imejengwa lakini bado changamoto iliyokuwepo *green house* hizi zimejengwa kwa muda mrefu lakini mpaka sasa hazijaanza kufanya kazi.  Naiomba taasisi au wizara husika ihakikishe kwamba *green house* hizi zinaendelezwa, ili vijana wetu na wao waweze kujiajiri wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la uimarishaji wa upatikanaji wa maji safi na salama ambao wajumbe wenzangu wamelichangia kwa kina, wasema kwamba kuimarishwa upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini kuwa watachimba visima na wataendeleza visima ambavyo vipo. Tunafahamu kwamba suala la maji safi ni suala muhimu kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma sisi wawakilishi wa majimbo tunapata tabu sana kwa wananchi wetu kuhusiana na suala la maji. Kutokana na hali hiyo, tunaomba sana serikali yetu sikivu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba suala hili linapewa kipaumbele kikubwa zaidi kuhakikisha visima vile ambavyo vimechimbwa viendelezwe na ile miundombinu ambayo ipo katika maeneo ya visima ambavyo vipo, basi vihakikishwe kwamba vinazingatiwa, ili wananchi wetu wapate huduma hii ya maji safi na salama.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba kwa haya machache na mimi niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa mchango wako sasa naomba nimuite Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Said Saleh Salum ajiandae.

**Mhe. Suleiman Haroub Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia kwa hotuba hii iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusiamama kwenye Baraza lako tukufu  ningekuomba uniruhusu nitoe pongezi na shukurani kwenye maeneo tofauti.

Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujaalia leo hii kuwepo hapa na tukiwa na afya na usima wa siha  lakini pia tupo katika hali ya amani na utulivu, lakini kipekee naomba nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu uliopita, lakini pia naomba nimpongeze kwa juhudi zake na bidii zake ambazo anaziendeleza hivi sasa na tunaziona kwa vitendo si kwa maneno kama vile watu walivyokuwa wakisema.

Lakini pia naomba nimpongezi kwa uteuzi wake kwa wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mhe. Hemed Suleiman Abdalla, Mawaziri, Mwanasheria Mkuu na baadhi ya watendaji waliokuwa tayari wameshateuliwa, lakini pia niwapongeze wananchi wa jimbo la Kiembesamaki na wana CCM kwa ujumla kwa kuniwezesha leo hii kuingia hapa kuja kuwasemea kwa niaba yao lakini pia nawaahidi kwamba sitowaangusha. *(Makofi)*

Naomba sasa nielekee katika hotuba hii Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa kamati ya bajeti na nilikuwa ni mmoja wa miongoni ambao tulishiriki uundaji wa mpango huu au mwelekeo huu, wengi wameshazungumza tayari na kuna mengi tayari tumeshazungumza huko nyuma lakini mimi  nataka niengezee kidogo tu.

Kwanza kabisa tuende kwenye ukurasa wa 20 kwenye mwalekeo wa mpango wa maendeleo mwaka 2020/2022 - 2023/2024 hapa kuna dira nzima inayoonyesha kwamba kufikisha katika kiwango cha juu cha uchumi wa kati kupitia mihimili mikuu minne ambayo ni mageuzi ya kiuchumi, maendeleo ya rasilimali watu na huduma za kijamii, kuimarisha miundombinu na utawala bora. Mhe. Mwenyekiti, kusema ukweli katika suala hili ambalo linahusisha masuala ya huduma za kijamii ni vizuri zaidi watu wakaziona mfano huduma za afya tuseme ukweli sasa hivi kuna uhaba wa madawa, kuna uhaba wa vitendea kazi katika vituo vya afya. Lakini pia katika sekta ya elimu kuna uhaba wa walimu wa kuweza kutoa ufaulu mzuri lakini pia kuna uhaba wa vitendea kazi, sasa ningeomba sana katika mwelekeo wa mpango huu kujikita zaidi kwenye masuala hayo ya huduma za jamii.

Lakini pia kwenye suala la maji safi na salama ningeomba sana Mhe. Waziri wa Fedha akaa na Mhe. Waziri wa Maji kwa naiaba ya Seirikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona

vipi kadhia hii ya maji inaweza kutatuka katika nchi yetu. Lakini pia nchi yoyote kutokuwepo na amani utulivu na miundombinu mizuri basi pia hata suala la maendeleo inakuwa vigumu kutokezea, ningeomba sana tuendelee kutunza amani yetu, utulivu wetu, umoja wetu na tuendelee kuboresha miundombinu ambayo ni chakavu.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kidogo kukazia kwenye sekta ya utalii kutokana na janga kuu la Corona Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana kumshauri Waziri wa Fedha kwamba tuongeze sekta ya ziada tukiachana na sekta ya utalii ambayo ndio tunaitegemea kama ni kiinua mgongo chetu kwa Zanzibar, kwani mfano mzuri hivi sasa tunahangaika na masuala ya ajira kwa sababu ya mripuko wa maradhi haya baadhi ya hoteli kati kati hapa zilifungwa watu wakawa hawana ajira tokea hapo soko la ajira limekuwa gumu Zanzibar na duniani kote, lakini ningeomba sana tuongeze sekta ya ziada tukiacha sekta ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kuchangia suala la *OC* matumizi haya ya fedha liko katika ukurasa wa 27 katika mchanganua mzima wa matumizi kama ifuatavyo, lakini hapa kwenye *OC* mafungu ningeomba sana Mhe. Waziri wa Fedha sehemu hii itumike vizuri sana maana hapa kuna watu wanatumia fedha za serikali kinyume na utaratibu, wanajua kwamba mwaka wa fedha unaishia Juni, kwa hivyo kuanzia Mei hapa tunajua jinsi gani ya kuweza kupiga. Kwa hivyo tungeomba kwamba *OC* ziwe zinaangaliwa kwa uwazi na watu waweze kujua kwamba zimetumika vipi.

Nikiendelea na hapo ningeomba sana kuna baadhi ya miradi tusiipe uzito sana kama ilivyoainishwa humu, moja mradi wa umwagiliaji mradi huu mpaka sasa hivi Pemba haujaguswa asilimia sururi lakini kwa maeneo ya Unguja Cheju bado mradi huu haujakamilika, maeneo ya Kibokwa Kaskazini Unguja bado haujakamilika, lakini pia muda wa mradi huu kuweza kukamilisha mlengo yake basi pia hautotosha. Hivyo basi ningeomba zaidi baadhi ya miradi kabla ya kuanzia kazi ingekuwa vizuri zaidi tungeifanyia utafiti kwanza na kuweza kuifanyia kazi.

Lakini kwa kuhitimisha ningeomba kusema maneno mawili madogo sana mambo yote haya ambayo tunataka hapa kiukweli ni mazuri sana na hotuba hii ni nzuri sana, lakini hotuba hii haitokuwa nzuri na yale tuliyosema ***yajayo kwamba neema tupu*** au ***yajayo yanafurahisha*** basi hayatokuwepo kama ufuatiliaji na usimamizi hautokuwa mzuri. Hivyo basi naishauri serikali kupitia taasisi tofauti masuala ya ufuatiliaji, masuala ya usimamizi kupitia miradi tofauti na mipango tofauti iweze kusomwa vizuri na ufuatiliaji uwe mzuri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Suleiman Haroub kwa mchango wako sasa naomba nimuite Mhe. Hassan Khamis Hafidh atafuatiwa na Mhe. Said Salehe Salim na kama muda utaturuhusu basi Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed ajiandae.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini pia namshukuru sana mnadhim kwa kuniambia nionjo nafasi *microphone* hii namba 53 ya Mhe. Mnadhim.
Kwanza kabisa nachukua fursa hii ya kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uzima lakini sote kwa pamoja kukutana hapa, kwa kweli mwelekeo huu wa bajeti wa 2020/2021 uliowasilishwa leo na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango

Zanzibar ameuwasilisha kwa madaha na ameuwasilisha vizuri namshukuru, lakini tunamshukuru zaidi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kumchagua Mhe. Jamal Kassim kuwa Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa jimbo la Welezo kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kuwa Muwakilishi wao wa Jimbo la Welezo, katika mwelekeo huu namshukuru sana Mwenyekiti na Kamati nzima ya bajeti, kadhalika kuna msemo mmoja kwa wazee unaosema bila ya kuwa na pesa hatuwezi kufanya jambo lolote la maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, mpango huu hautokamilika utekelezaji wake bila ya kuwa na pesa ya kutosha ili tuweze kufanya mipango yetu tuliyoipanga.

Mhe. Mwenyekiti, kupata pesa hizo kwa nchi nyingi duniani hutegemea mambo matatu makuu naomba niyataje.

1) Jambo la kwanza kunategemea kuweka mazingira bora ya uwekezaji, mazingira bora ya kufanya biashara, ili nchi iweze kufanyika biashara, nchi iweze kuwekeza hasa katika sekta ya viwanda kwa lengo la kupata kodi pamoja na ajira kwa wananchi wake.

2) Lakini kadhalika Mheshimiwa lazima nchi ijikite katika kuhakikisha inafanya kila liwezekanalo inakusanya kodi ya kutosha ili nchi iweze kutekeleza majukumu yake iliyojipangia.

3) Jambo la tatu Wazungu wanasema lazima nchi iweze kukata matumizi yaliyokuwa sio ya lazima au matumizi ya hanasa kwa kizungu tunaita *(Structure Adjustment Program*), ili nchi iweze kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana hotuba hii napenda kuishauri serikali mambo kadhaa yafuatayo kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, nchi yoyote duniani maendeleo yanaanza na elimu tukitaka tusitake nchi yetu elimu yetu hasa ya skuli za serikali iko chini, biashara ya kuuza elimu Zanzibar na kuwa na *Private School* imeengezeka na inaimarika kila siku hili ni kutokana na kwamba elimu yetu ya skuli za serikali haiko vizuri inakabiliwa na changamoto nyingi, biashara kuu za elimu inaendana na Zanzibar na si wengi wakwezi na wakulima wenzangu tunaoweza kuinunua elimu katika skuli za *private*.

Mhe. Mwenyekiti, mtoto mmoja kumpeleka skuli kama inaitwa FEDHA inaweza kugharimu milioni tano kwa mwaka, skuli nyengine ndani ya Zanzibar hii elimu yake inauzwa dola elfu saba mpaka elfu nane mtu una watoto watatu au wanne utaweza wapi. Ombi langu Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii ijikite zaidi kuimarisha sana suala zima la elimu katika skuli zetu za serikali, skuli za serikali mpaka hivi sasa ingawaje bado unaweza kujenga hoja lakini hazifanyi vizuri na skuli zinazofanya vizuri ni skuli za *private* ambazo elimu yake inauzwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niipongeze sana bajeti hii kwa kuzingatia sekta ya afya asikwambie mtu bado sekta ya afya kwa upande wa Zanzibar hasa Hospitali yetu ya

Mnazi Mmoja bado iko chini, kuna uhaba wa madaktari, uhaba wa vifaa tiba, uhaba wa wataala na vitu vya kitaalam, kwa mfano maradhi ambayo Zanzibar mtu anaweza kupoteza maisha maradhi hayo hayo nchi za wenzetu zilizoendelea anaweza akahuwika na akaishi, hii ni ushahidi tosha Mhe. Mwenyekiti, kwamba bado tuna kila sababu ya kuimarisha afya yetu, ili tuweze kuendelea na tuishi ndani ya nchi yetu bila ya wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti wenzetu wa Cuba baada ya uhuru tu na baada ya Mapinduzi matukufu wao walikuja na msemo wa kusema afya kwanza, niliposhuka tu Cuba jambo la kwanza nilikwenda kuonyeshwa jinsi gani walivyoimarika katika kuimarisha afya yao. Namuomba sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na watendaji wote kwa jumla tuimarishe sekta nzima ya afya, ili tuweze kuishi ndani ya nchi yetu kwa amani na salama.

Mhe. Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nane kwa kuja na wazo la kujenga bandari ya Mpigaduri na bandari ya Mangapwani, hii yote ni kuonesha jinsi gani Zanzibar sasa inataka kujikita kuendelea katika ile inayoitwa dunia ya nchi zilizoendelea. Mhe. Mwenyekiti, naamini ujenzi wa bandari hii utaleta ajira kwa vijana lakini pia utaiweka Zanzibar kujulikana *national and international* kwamba kuna nchi inaitwa Zanzibar, kama nilivyosema juzi Zanzibar ni *"Motherland of Africa and Motherland of East Africa.*

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ukiendelea mwelekeo huu umezungumza barabara kama unavyojua Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu barabara nyingi hasa barabara za ndani ni mbovu hazipo kabisa hasa ukizingatia Mkoa wa Magharibi ambapo kunaishi watu wengi wa Zanzibar, naipongeza sana mwelekeo huu wa bajeti kwamba pia neno la barabara limeongelewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika maeneo ya uwekezaji *National Park* Zanzibar ina mpango wa kujenga maeneo ya viwanda kila wilaya na kwa kuanzia tayari Serikali ya Awamu ya saba ilianza kujenga eneo la kiwanda cha Namangwe Pemba, lakini kuna Nungwi na Dunga inafuatilia, nimeona imetajwa katika mwelekeo huu. Kwa kweli, naipongeza serikali kwa kuja kuendeleza wazo hili ambalo linalenga kuleta zile ajira laki tatu ambazo kazisema Mhe. Rais, nchi yetu lazima tuwe na viwanda uwezekano wa kuwa na viwanda upo lakini lazima tuweke miundombinu katika maeneo haya ya viwanda ili wananchi wetu na wa wenzetu waweze kuwa rahisi kuja kuwekeza katika maeneo hayo.

Kuna msemo unasema "bila ya kuwa maeneo rafiki ya viwanda hakuna mtu atakayeweza kuja kuwekeza" Hivyo na lazima maeneo hayo yawe na miundombinu, nchi kama Ethiopia na Ghana wamefanya hivyo sasa hivi Ethiopia ni miongoni mwa nchi ambayo unaweza kusema inaendelea kwa viwanda, ukiona viatu vizuri vinatoka Afrika basi vinatoka Ethiopia, kwa sababu wamejikita katika kuweka mazingira mazuri katika maeneo ya viwanda.

Mhe. Mwenyekit, pia Mhe. Rais katika mwelekeo huu wameongelea umeme ni kweli ili tuendelee lazima tuwe na umeme imara, umeme wa kutosha na umeme wa kuaminika.

Mhe. Mwenyekiti, naipogeza sana hotuba hii kwmaba umeelezea kuimarisha umeme leo, ili nchi yetu iweze kuendelea katika suala zima la kuekeleza katika suala la viwanda, bila ya kuwa na umeme bora, umeme imara hakuna mtu ataweza kuja kuekeza.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana lakini Mhe. Rais amekuja na wazo jengine jipya la kuendeleza zana nzima ya uchumi wa bluu, naipongeza sana katika hutoba imejikita sana kuhakikisha inajogolea katika uchumi wa bluu.

Mhe. Mwenyekiti, kweli samaki sisi kama nilivyosema juzi tunaagizia kutoka nje ya nchi tunakula samaki marehemu, wakati nchi yetu imezungukwa na bahari lakini sisi samaki tunaokula ni marehemu samaki hujui wamekufa lini, hujui wamewekwa lini marehemu samaki hao hatujui tuna madhara gani tunaokula, lakini tunao uwezo wa kula samaki walio hai walio vizuri ndani ya nchi yetu na kuacha kula marehemu samaki. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Rais kwa kuja na hii *idea* ya wazo la uchumi wa bluu kwa sababu utatupelekea kutokula marehemu samaki.

Nikiendelea na mchango wangu, naomba kuzungumzia machinjio ya mifugo nchi yetu kuna machinjio mbali mbali ya mifugo lakini cha kushangaza kwamba machinjio hayatumiki, kutokutumika kwa machinjio haya kunapeleka watu wengi kuiba wanyama wetu kama mfano ngómbe, mbuzi na kwenda kuwachinja katika maeneo yasiyojulikana.

Mhe. Mwenyekiti, imefika wakati kwanza bila ya kujenga machinjio mapya kuhakikisha kila mtu anayetaka kuchinja ngómbe au mbuzi anachinja katika maeneo yaliyotengwa na serikali, mheshimiwa mpango huu ni mzuri wa serikali lakini hautekelezwi mheshimiwa hatimaye unatuletea athari kwa wafugaji wetu, sisi wafugaji wa wakwezi na wakulima tunapenda kufuga ukimfuga ngombe kesho anakuja kuibiwa anakwenda kuchinjwa, hii tu ni kwa sababu maeneo ya machinjio yaliwekwa hayatumiki.

Kwa kweli, nchi za wenzetu zilizoendelea huwezi kumchinja hata kuku au ndege bila maeneo maalum yaliwekwa kwa kuchinjia. Mhe. Mwenyekiti, ni mpango mzuri lakini tusiendelee kujenga bila ya kuimarisha tuliyonayo na kuyatumia tuliyonayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimefurahi katika mpango huu umeongelea katika kuchukua hatua maalum katika kuimarisha zao kuu letu la karafuu. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme leo watu wote wasikie. Zanzibar inalima karafuu na karafuu zetu ndio karafuu bora, karafuu zenye hadhi, karafuu zetu ndio karafuu mtu yoyote *Indonesia*, *Madagascar*, *Comoro* wamejaribu kulima karafuu. Lakini hawawezi kukamilisha matumizi ya karafuu zao bila ya kuchanganya na karafuu za Zanzibar, hii yote ni kuonesha jinsi gani karafuu za Zanzibar zilivyo bora. Kwa hiyo, naipongeza serikali na kuiomba serikali ijikite katika kuendeleza na kuimarisha zao zima la karafuu kwa wananchi wetu ili zao hili liendelee kuwa Zanzibar ni *leading country* kwa kuzaliza karafuu.

Mhe. mwenyekiti, nakuona unataka kuwasha taa lakini bado muda wangu wa dakika nne nimeona.

Mhe. Mwenyuekiti, kama nilivyosema bila ya kuwa na afya bora naipongeza serikali kwa kuandaa ujenzi wa Hospitali ya Binguni yote hii ni kutaka kuimarisha na kuona jinsi gani nchi yetu mambo ya sekta ya afya yanaimarika. Mhe. Mwenyekiti, ni aibu

unajisikia vibaya unapokwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja pale hospitali ya rufaa lakini ukaambiwa kipimo hichi hakuna, dawa hii hakuna, wenda Al-Rahma kipimo hichi mpaka unapata wasiwasi unaogopa.
Vile vile, lakini humu nataka pia kuona kuimarisha usafi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mwenyekiti, si siri Hospitali ya Mnazi Mmoja chafu lazima tutenge bajeti maalum ya kuisafisha, unaweza ukatoka nyumbani kwako huna maradhi lakini ukafika Mnazi Mmoja kwa sababu ya uchafu wa hosiptali ile yale maradhi ukayapatia pale.

Mhe. Mwenyekiti, tumemsikia Mhe. Rais wetu alitembea kwa miguu akasema usafi ni kitu muhimu. Naomba sana pia Hospitali ya Mnazimmoja iwekewe bajeti maalumu ya kwamba kuhakikisha inasafishwa. Mhe. Mwenyekiti, nchi za wenzetu ukienda hospitali inanukia lakini Hospitali ya Mnazi Mmoja ukienda inanuka kwa sababu ya uchafu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kukushukuru sana, naomba kuwashukuru wananchi wa jimbo la Welezo, naomba kukushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia bajeti hii Mwelekeo wa Uchumi na Mipango wa Maendeleo wa Bajeti 2021/2022 - 2023/2024.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naunga mkoni hotuba ya bajeti hii na naomba sana Mwenyezi Mungu ibariki Zanzibar, Mwenyezi Mungu ibariki Tanzania nakushukuru sana mheshimiwa ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Said Saleh Salim na nilisema kama muda utaruhusu nitampa Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed.

**Mhe. Said Saleh Salim:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi na vilivyomo kwa kutujaalia kuwepo tena leo katika Baraza lako tukufu na tukichangia hotuba hii muelekeo wa hali ya uchumi.

Lakini pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuchagulia viongozi wachapa kazi akiwemo Waziri wetu wa Waziri Fedha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nimpongeza sana Mwenyekiti wangu wa kamati Mhe. Saada Mkuya Salum kwa kutuwasilishia ripoti kwa umahiri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze kwa suala la barabara katika Jimbo langu la Tumbe kuna barabara ambayo ishawekea ahadi zaidi ya mara mbili na viongozi waliopita akiwemo Mhe. Rais Mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein, katika awamu yake ya mwanzo aliweka ahadi kutengeneza barabara ya Finya/Kicha awamu ya pili na mpaka sasa hivi barabara haipitiki.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri mwenye Wizara ya Mawasiliano basi angalau aje aitembelee hii barabara aone kwa jicho lake jinsi gani ile barabara haipitiki kabisa haipitiki, kwa hiyo naomba hii barabara iwe ni miongoni mwa barabara ambazo zitawekwa kipaumbele katika awamu ya mwanzo.

Jambo jengine nizungumzie masuala ya uzalishaji wa karafuu kwa kawaida wananchi na wadau wa karafuu zinazaliwa kila baada ya miaka miwili au zaidi na inapofika wakati wa karafuu wananchi wanakuwa mitaji hawana tena. Kwa hiyo, naiomba wizara kwamba wananchi iwawezeshe kuwapatia mitaji kwa wakati, ili waweze kuchuma zao hili wakiwa na mitaji ya uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine naomba nichangie katika masuala ya ushuru mimi naomba serikali inagalia vizuri viwango vya ushuru hasa ushuru tunaotozwa wananchi wa Pemba. Ushuru wananchi wa Pemba tunasokotwa watu hawa wa mamlaka za kutonza ushuru wanatusokoto sana, unavyotoa mzigo bandarini Unguja unalipia na unakoshusha unalipia ni jambo la kushangaza sana. Kwa mfano, unavyotoka Mkokotoni kuingia Tumbatu ukifika Tumbatu mzigo hulipii tena ila ukifika Pemba unalipia wakati tuko nchi moja hii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tuna pahali tumekosea pale tunapotoka Pemba ukiulizwa unakwenda wapi ukasema nakwenda Zanzibar kumbe unaende Unguja, sasa hii imesababisha sisi tuonekane kama tuko nchi nyengine katika suala la ushuru. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana jambo hili mtuhurumie sana vitu vyote viko bei mara mbili ya Unguja kule Pemba. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nielekee katika Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika eneo hili hatuko vizuri kwa sababu wananchi wanakuwa hawapewi elimu kwa baadhi ya mambo, kwa mfano watu wetu wa Mabaraza ya Mji wao zaidi kuchukuwa mapato, lakini ile dhamana yao ya kuwaelimisha wananchi, kwa kweli masuala ya ujenzi ukifika baadhi ya sehemu ni uchafu mtupu, kwa sababu watu wa mapato wa Halmsauri au Mabaraza ya Miji wao wanachojua ni kutoza kodi, lakini ushauri kwa wananchi wajenge vipi hawawashauri isipokuwa wao wanawapeleka mahakamani kwa maana hawajatoa kodi, lakini vipi mtu ajenge hawawashauri.

Sambamba na hili kwenye suala la ujenzi wa masoko pia sijui hapa mamlaka hazikai pamoja wakati wa kujenga masoko kwa wananchi wakajadili au kuna tatizo gani sijajua, kwa maana kule Pemba masoko mengi yamejengwa pesa za serikali zimetumika lakini masoko hayatumiki ipasaavyo. Kwa mfano, Msuka kuna soko bandarini ni zaidi ya miaka kumi hilo soko lishakuwa bovu na halijatumiwa hata siku moja pesa za wananchi zimekwenda malengo hayakufanikiwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hili jambo liangaliwe pahali zilipoingia pesa za serikali lazima zitumike kwa malengo yaliokusudiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la mazingira ni suala limekuwa kikwazo hasa katika jimbo langu la Tumbe maeneo ya Wapape, Bandarini Tumbe na hata katika Jimbo la Konde maeneo ya Bandarini Msuka maji yanachukua maeneo ya ardhi kwa kasi kubwa sana. Kwa hiyo, naiomba wizara inayoshughulika na mambo ya mazingira basi iangalie suala hili kwa kupanda miti, kwa sababu ardhi yetu tunaitumia sisi binadamu na maji yanachukua yake sehemu, ili tupunguze kasi na katika jimbo langu la Tumbe ipo Jumuiya ya Mazingira ambayo imeanzwa hata mimi na Mhe. Mbunge tushasaidia vifaa kwa ajili ya upandaji miti na usafishaji wa mazingira namuomba waziri mwenye wizara hii basi anitafute tushirikiane tuliangalie suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako sasa mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo naomba nimwite Mhe. Fatma Ramadhani Mohamed.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nipende kukushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii japo mambo machache, naona waheshimiwa wengi washagusia lakini mimi nipende kugisa mambo machache.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati ndugu yangu Mhe. Jamal Kassim Ali kwa hotuba yake nzuri iliyogusa kila nyanja lakini hatuna budi na sisi kutoa mchango wetu japo kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza katika vipaumbele vya 2021/2022 katika kipaumbele namba 15 kuna huu Usimamizi wa Matumizi na Manunuzi, serikali inapofanya maamuzi ya kununua vifaa mbali mbali napenda nishauri mambo machache.

Naiomba serikali iangalie sana kwa mfano tuliponunua meli yetu ya MV. Mapinduzi II hatukuzama kama hakuna wataalamu wa kuindesha meli hiyo ambapo ikasabisha matatizo makubwa. Kwa hiyo, naomba serikali inapofanya mpango wake wa manunuzi wa vifaa mbali izingatie hili na pia ipeleke watalaamu nje ya nchi, ili wakasome ili tupate kuviendesha vyombo vyetu kwa usahihi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 33 katika suala zima la elimu Mhe. Waziri hapa amegusia kutakuwa kujengwa skuli za tatu za ghorofa katika maeneo ya Mfenesini, Gamba na Kifundi kwa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, naomba suala hili la elimu pia tuangalie katika Skuli ya Mbuzini ambapo wanafunzi wanasomo chini ya mti watoto wale jua/mvua linawapiga. Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali iangalie kwa jicho la huruma watoto wale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipotembelea katika ziara yangu katika kuteleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi machozi yalinitoka. Kwa hiyo, naomba serikali iangalie kwa jicho la huruma watoto wale iweze kufanyiwa ukarabati majengo ya skuli yao ambayo ni nguvu za wazazi wao. Wazazi wao tayari wameshajenga mabanda mawili lakini bado hayajaezekwa naishauri serikali ifanye juhudi.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, pia mimi nitaenda suala zima la maji. Suala hili la maji Mhe. Waziri wa Maji tuliangalaie kwa jicho la huruma kina mama wanapata tabu sana kuhusu suala zima la maji, mwanamke anaamka asubuhi anafanya biashara ya maandazi lakini ndani hakuna maji hajui aanze lini aache lipi. Pia linasababisha watoto wetu wadogo kupata hizi ajira za maji mtoto anaacha kwenda skuli baadaye anabeba madumu ya maji anaona hii ni ajira nzuri inayompatoa pesa.

Kwa hiyo Mhe. Waziri wa Fedha na Mhe. Waziri wa Maji mukae kwa makini kuliangalia suala zima hili la maji ili kuepukana na usumbufu, pia kuepukana na wawakilishi wetu wa majimboni kukosa kura. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed kwa uwasilishaji wako na machano wako.

Waheshimiwa wajumbe muda ulibaki kwa sasa hatuwezi kupatia mchangiaji mwengine ni dakika tano tu zilizobaki. Kwa hiyo, niwaombe sana kesho *In sha Allah* tukijaaliwa tuje tuendelee wale waliobaki ambao wameleta na nadhani watapata nafasi ya kuchangia hotuba hii au mpango huu wa mwelekeo kwa vizuri zaidi.

Waheshimiwa Wajumbe, napenda kuchukuwa nafasi hii kuwashukuru kwa utulivu wenu lakini kwa michango yetu pia ambayo mumeitoa na kumpatia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango nawashukuru sana, na naomba niakhirishe kikao hichi mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 17 Februari, 2021 saa 3:00 asubuhi)*